EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

UCHANGANUZI WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAGAZETI YA KISWAHILI NCHINI KENYA: MFANO WA GAZETI LA TAIFA LEO

Na:

JAMES OMARI ONTIERI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA LUGHA NA ISIMU YA CHUO KIKUU CHA EGERTON

CHUO KIKUU CHA EGERTON
NJORO, KENYA

JUNI 2005

EULIB
063656

PL8707.172.O55

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi _____ Tarehe 16.06.05

James Omari Ontieri

IDHINI

Tasnifu hii inawasilishwa katika Chuo Kikuu cha Egerton kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Lugha na Isimu kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo.

Sahihi _____ Tarehe 20/6/2005.

Dkt. John N. Kimemia

Sahihi _____

Tarehe 17-06-05

Dkt. Francis O.Aswani

HAKI ZA KUHIFADHI

© James Omari Ontieri 2004

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupigisha chapa, kutafsiri au kuitoa kazi hii kwa njia yoyote ile bila idhini kwa maandishi kutoka kwa mwenyewe au/na Chuo Kikuu cha Egerton.

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa: Mzee Benedicto Omari na Mama Hellen Nyang'ara Omari pamoja na mke wangu Joyce na watoto wetu Sylvia na Sheila.

SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na utulivu wakati wote nilipokuwa nikitaalamia shahada hii ya uzamili. Aidha, nawashukuru kwa njia ya kipekee wasimamizi wangu: Dkt. J. N. Kimemia na Dkt. F.O. Aswani kwa kuniongoza na kunielekeza nilipokuwa nikiishughulikia tasnifu yangu. Moyo wenu mweupe na juhudi zenu zimechangia pakubwa kukamilika kwa kazi hii. Mungu awabariki daima.

Namshukuru mwalimu Gwachi Mayaka kwa kunipa ushauri kuhusu kazi yangu wakati wote nilipohitaji msaada wake. Himizo lake nilipoelekea kutamauka lilinipa msukumo wa kujizatiti ili kuihitimisha kazi niliyoianza – kwani aanzaye jambo na asilikamilishe, ni sawa na asiyeanza.

Na kwenu walimu wangu: Dkt. C. Kitetu; Dkt. S. K.Beja; Dkt. F. Tchai; Bw. Muindi (wa Idara ya Lugha na Isimu), na Bw. G. Kabira (wa Idara ya Sayansi ya Tarakilishi), nawashukuru sana kwa kunivuvia hekima ambayo imekuwa nyota iliyoniongoza katika kuikamilisha kozi yangu. Nitawakumbuka daima kwa kujitolea kwenu katika kunifundisha kozi anuwai na kunielekeza nilipohitaji msaada wenu, hususan nilipokuwa nikifanya utafiti wangu.

Naomba pia kuwataja na kuwashukuru walimu wafuatao kwa kukubali kuisoma kazi yangu katika hatua mbalimbali na kunishauri: Dkt. J.O. Onyango; Bw. W. Nabea ; Bi. A. Juma; Bw. J. Marani; Bw. E. Mohochi; Bw. S. wa Ngero (Chuo Kikuu cha Egerton) na Ndugu Obuchi Moseti (Chuo Kikuu cha Mashariki mwa Afrika, Baraton). Ushauri wenu ulikuwa mchango mkubwa ambao ulinisaidia kuziba mapengo ambayo yangetokea katika kazi yangu.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu: Eucabeth Mong'are, Virginiah Njau, Carren Nyandiba, Dennis Mudhune, Gilbert Ongaki, Joseph Ngugi, Paul Ng'ethe na Stephen Kimani kwa ushirikiano walioonyesha tulipokuwa tukitaalamia somo hili la Kiswahili pamoja. Umoja wetu hatimaye umetuwezesha kuogelea mpaka mwisho wa bahari.

Nanyi wandani wangu Kirioba T., Andima G., Mutai J., Mutai H., Barasa M., na Kinyanjui J., nawashukuru kwa kunihimiza na kunisaidia kwa hali na mali nilipoelekea kupungukiwa. Maulana mwenye utajiri mkubwa, awajalie vikapu vilivyojaa kutokana na ukarimu wenu.

Siwezi kuwasahau wafanyakazi katika maktaba mbalimbali walionisaidia wakati wa utafiti wangu kama vile Bi. Nancy Ng'etich na Bi. Khadija Said, wa maktaba ya umma ya

wilaya ya Kericho. Endeleeni na moyo huo ili wasomi wengi wanufaike kutokana na huduma zenu mufti.

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa taasisi zifuatazo: Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa nafasi ya kusomea shahada hii ya uzamili chuoni humu; Halmashauri ya Mikopo ya Elimu ya juu (HELB) kwa kunipa mkopo ulioniwezesha kugharamia masomo; mwajiri wangu (Tume ya kuwaajiri walimu nchini Kenya), kwa kunipa likizo ya muda wa miaka miwili kwa ajili ya masomo yangu huku nikiendelea kupokea mshahara.

Kwa wazazi wangu, nawashukuru kwa kunipeleka shuleni na kunionyesha umuhimu wa elimu maishani. Namshukuru mke wangu mpendwa Joyce na wanetu Sylvia na Sheila kwa kunipa mazingira tulivu katika kipindi chote nilipokuwa masomoni. Mungu awanyunyizie baraka zake aushini mwenu. Katu sitawasahau ndugu zangu kwa kuniombea na kunitakia kheri nilipokuwa chuoni.

Pia, natoa shukrani kwenu Bw. na Bi. M. Chege kwa kunipigia chapa kazi hii na hata kuniruhusu kuitumia tarakilishi yenu palipozuka haja. Mchango wenu uliopelekea kukamilika kwa kazi hii, hauna kipimo. Mungu awabariki daima.

Mwisho, nawashukuru enyi nyote mlionisaidia kwa njia moja au nyingine nilipokuwa nikiishughulikia kazi yangu. Kwa hakika haiwezekani kuwataja nyote – Mola aendelee kuwajalia matendo mema maishani mwenu.

IKISIRI

Magazeti ni chombo muhimu katika usambazaji wa habari kote ulimwenguni. Gazeti la *Taifa Leo* linalochapishwa nchini Kenya lina umuhimu wa kipekee kama chombo mahsusi cha kuwasilishia ujumbe kwa Wakenya wengi kwani huandikwa kwa Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa; yenye matumizi mapana na inaeleweka miongoni mwa wananchi wengi. Hata hivyo, utafiti umeonyesha kuwa matumizi ya lugha yenye upungufu wa ufasaha katika uandishi wa makala yachapishwayo katika gazeti hili, ni jambo mojawapo linalopelekea gazeti hilo kutosomwa na watu wengi. Utafiti huu umechunguza matumizi ya lugha katika *Taifa Leo* huku makosa mahsusi yanayojitokeza katika makala teule yakitambulishwa na kujadiliwa. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Katika utafiti huu, nakala thelathini za gazeti la *Taifa Leo* zilizochapishwa kati ya 1999 na 2003 zilichanganuliwa ili kugundua jinsi ambavyo lugha imetumiwa kuwasilishia ujumbe kwa hadhira. Mtindo wa sampuli shelabela na ile iliyoazimiwa ulitumiwa katika kuteua nakala zilizochanganuliwa. Njia ya utafiti ya upekuzi wa kimaktaba ilitumiwa ambapo mbinu ya uchanganuzi umbo-maana ilizingatiwa katika kukusanya data. Data iliyokusanywa ilipangwa kulingana na nadharia tete za utafiti na kuchanganuliwa kwa kuzingatia umara-tokezi wa makosa katika vipengele vya lugha vilivyochunguzwa. Uchanganuzi umeonyesha kuwa kuna makosa mengi katika vipengele mahsusi vya lugha vilivyochunguzwa mathalan: Sarufi, Msamiati, Methali, Nahau na Tamathali za Usemi. Tunatumai kuwa matokeo ya utafiti huu, yatawafaa waandishi na wachapishaji wa magazeti, hususan *Taifa Leo,* katika juhudi za kuchunguza mbinu zao za uandishi kwa mujibu wa makosa yaliyotambulishwa ili kuimarisha mawasiliano. Matokeo haya huenda pia yakachangia katika kuweka misingi ya utambulishaji na uchanganuzi wa makosa katika Kiswahili na hivyo kuwanufaisha walimu na wanafunzi katika viwango mbalimbali vya mafunzo katika harakati zao za kuepukana na makosa yatokeayo katika uandishi. Aidha, ustawishaji na uenezaji wa Kiswahili kama lugha ya taifa nchini Kenya, utasukumwa mbele.

YALIYOMO

UNGAMO ii

HAKI ZA KUHIFADHI iii

TABARUKU iv

SHUKRANI v

IKISIRI vii

ORODHA YA MAJEDWALI xi

ORODHA YA GRAFU xii

VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA xiii

ISTILAHI ZILIZOTUMIKA xiv

SURA YA KWANZA 1

UTANGULIZI 1

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Suala la Utafiti 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti 3

1.4 Nadharia Tete 3

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Upeo wa Utafiti 5

SURA YA PILI 6

MAPITIO YA MAANDIKO 6

2.1 Utangulizi 6

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada 6

2.2.1 Lugha kama msimbo wa mawasiliano 6

2.2.2 Matumizi ya lugha katika vyombo vya habari 8

2.2.3 Methali na Nahau 11

2.2.4 Tamathali za Usemi 13

2.2.5 Sarufi na Msamiati 14
2.3 Misingi ya Nadharia 17
SURA YA TATU
MBINU ZA UTAFITI 20
3.1 Utangulizi 20
3.2 Njia za utafiti 20
3.3 Mahali pa utafiti 20
3.4 Uteuzi wa sampuli 20
3.5 Vifaa vya utafiti 21
3.6 Ukusanyaji wa data 22
3.7 Uchanganuzi wa data 23
SURA YA NNE 24
MATUMIZI YA LUGHA KATIKA GAZETI LA TAIFA LEO 24
4.1 Utangulizi 24
4.2 Sarufi 24
4.2.1 Matumizi ya sentensi zisizokamilika 24
4.2.2 Ukosefu wa upatanisho wa kisarufi 29
4.2.3 Makosa katika mnyambuliko wa maneno 33
4.2.4 Upungufu katika mpangilio wa maneno katika sentensi. 36
4.2.5 Makosa ya kitahajia 39
4.2.6 Makosa ya uakifishi 43
4.2.7 Matumizi ya viambishi isivyostahiki 45
4.2.8 Kujirudia katika sentensi 47
4.2.9 Matumizi yasiyofaa ya vihusishi 49
4.2.10 Makosa katika matumizi ya viunganishi 51
4.2.11 Miundo changamano 54
4.3 Msamiati 58
4.3.1 Matumizi ya maneno yasiyofaa 59
4.3.2 Matumizi ya maneno ya jozi bainifu isivyostahiki 59
4.3.3 Matumizi ya maneno yenye maana finyu 60
4.3.4 Kutohoa maneno pasipo haja 61
4.4 Methali na Nahau 63
4.4.1 Methali 63

4.4.2 Nahau 66
4.5 Tamathali za Usemi 68
4.5.1 Matumizi ya TZU isivyostahiki 68
4.6 Muhtasari wa matokeo 71
4.7 Hitimisho 73

SURA YA TANO 74

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 74

5.1 Utangulizi 74
5.2 Hitimisho. 74
5.2.1 Malengo na makisio ya utafiti. 74
5.2.2 Vikwazo 77
5.3 Mapendekezo 78

MAREJELEO 81

KIAMBATISHO A: TANBIHI 92

KIAMBATISHO B: GTL JUMATATU, MEI 6, 2002 96

KIAMBATISHO C: GTL, IJUMAA, OKTOBA 3, 2002 99

KIAMBATISHO D: TAIFA JUMAPILI, MEI 30, 1999 107

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Makosa yaliyopelekea sentensi kutokamilika 28

Jedwali 2: Kasoro zilizosababisha kutokuwa na upatanisho wa kisarufi katika sentensi..... 32

Jedwali 3: Kasoro katika unyambuaji wa maneno 36

Jedwali 4: Umara-tokezi wa makosa yahusuyo mpangilio wa maneno katika sentensi.. 38

Jedwali 5: Uainisho wa makosa ya kitahajia na umara-tokezi wake..... 42

Jedwali 6: Makosa ya uakifishi 45

Jedwali 7: Makosa yanayohusu matumizi ya viambishi..... 47

Jedwali 8: Makosa yahusuyo kujirudia katika sentensi 49

Jedwali 9: Matumizi yasiyofaa ya vihusishi 51

Jedwali 10: Makosa yahusuyo viunganishi..... 54

Jedwali 11: Makosa yanayohusu miundo changamano..... 56

Jedwali 12: Umara-tokezi wa makosa katika vipengele anuwai vya kisarufi..... 57

Jedwali 13: Msambao wa makosa yahusuyo msamiati..... 62

Jedwali 14: Makosa katika vipengele vinavyohusu matumizi ya methali..... 65

Jedwali 15: Makosa yaliyotokeza katika matumizi ya nahau 68

Jedwali 16: Makosa yahusuyo matumizi ya tamathali za usemi..... 70

Jedwali 17: Makosa katika vipengele anuwai vya lugha vilivyoshughulikiwa..... 71

Jedwali 18: Msambao wa makosa katika makala mbalimbali yaliyochanganuliwa 73

ORODHA YA GRAFU

Grafu A: Makosa katika vipengele mbalimbali vya kisarufi 57

Grafu B: Makosa katika vipengele mbalimbali vya msamiati 62

Grafu C: Makosa katika vipengele mbalimbali vilivyoshughulikiwa..... 72

VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

BR	–	Barua
G T L	-	Gazeti la Taifa Leo
HDT	–	Hadithi
HK	–	Habari Kuu
Mh.	-	Mhariri
MYW	–	Makala ya watoto
SPSS	-	Utaratibu wa kitarakimu wa sayansi za kijamii katika tarakilishi.
SYT	-	Sauti ya Taifa
SYW	-	Sauti ya Wasomaji
T Z U	-	Tamathali za usemi
TAH.	-	Tahariri
Wah.	-	Wahariri

ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

Hadhira - Wapokeaji ujumbe kupitia kwa GTL.

Matini - Wales (1989), anasema kuwa neno hili kikawaida hutumiwa kwa maana ya mwambatano wa sentensi au matamko yanayoingiliana kimuundo na kimaana. Anaendelea kuelezea kuwa dhana hii hutumiwa sana katika isimu na umtindo kurejelea mkusanyiko wa sentensi au matamko, ulio na muumano wa kiisimu na mshikamano wa kisemantiki. Katika uchunguzi huu, neno hili limetumiwa kwa maana ya makala yaliyoteuliwa kwa uchanganuzi kutokana na jumla ya yale yanayochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo*.

Mawasiliano- Upitishaji na upokeaji wa ujumbe kupitia kwa GTL.

Tungo – Kauli iliyodondolewa kutokana na makala yachapishwayo katika GTL kwa ajili ya uchanganuzi.

Tungo lemavu – Sentensi iliyodondolewa kutokana na makala ya GTL ambayo ina zaidi ya kasoro moja na hivyo kuwa vigumu kuichanganua kwa kuzingatia umbo maalum la lugha.

Uchanganuzi umbo-maana - Mbinu ya utafiti ambayo inahusisha usomaji wa maandishi kwa kina na kuchambua vipengele mbalimbali vya lugha kwa mujibu wa utafiti wetu. Kwa mujibu wa utafiti wetu, makala teule ya GTL yamechanganuliwa kwa kuzingatia mbinu hii.

Urundikaji – Urudufishaji wa umbo fulani au maumbo yanayokurubiana kimaana katika sentensi madala ya kutumia umbo moja tu ili kutosheleza haja ya mawasiliano.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Mawasiliano kupitia vyombo vya habari ni sehemu muhimu katika maisha ya kisasa. Vyombo vya habari, mathalani runinga, magazeti, redio na filamu, hutekeleza jukumu kubwa katika kuelekeza namna tunavyoutumia wakati wetu na jinsi tunavyoishi maisha yetu, (Baran na wenziwe : 1984). Ujumbe unaowasilishwa na vyombo hivi hunuiwa kuifikia hadhira pana. Mara nyingi huwa ni vigumu kwa chanzo cha ujumbe kupata mwitikio kutoka kwa wapokeaji ili kuimarisha mawasiliano kulingana na haja. Mawasiliano ya aina hii yameleta mabadiliko katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa (Wood: 1983).

Ni nadra muda mrefu kupita kabla ya mwanadamu kutaka kujua mambo yanayoendelea katika mazingira yake na pia kote ulimwenguni. Hivyo, mawasiliano ya jinsi hii huwa kiungo muhimu ambacho ni sehemu ya maisha ya mja yeyote. Maendeleo katika usambazaji wa habari katika karne iliyopita, yamehakikisha kuwa ujumbe unawafikia watu wanaonuiwa kwa wakati mfupi iwezekanavyo.

Magazeti, kama njia inayotumiwa katika mawasiliano, yana jukumu kubwa na la kimsingi katika jamii kwa kuwa husheheni habari za kina, kinyume na redio na runinga ambapo habari muhimu hutolewa kwa muhtasari. Wainwright (1972:4), anasema hivi kuhusu magazeti:

> *"...Magazeti ni hifadhi, vyombo vya rekodi. Huweza kurejelewa na kupitiwa kwa njia ambayo haiwezekani katika habari za redio na runinga. Magazeti huweza kueleza matukio kwa urefu, kuongezea ujumbe wa kindani, kutoa maoni ya kimamlaka kutoka kwa watu wanaotajika na wanaoweza kugundua mikondo inayofuatwa na visa fulani vinavyoelezwa katika habari...."*(tafsiri hii na nyingine zote zinazofuata ni zetu).

Maelezo haya yanafanana na maoni ya Mbugua (1997), ambaye anasema kuwa magazeti ni msimbo muhimu wa mawasiliano miongoni mwa vyombo vya habari vinavyotumiwa katika ulimwengu uliostaarabika.

Katika miaka ya hivi majuzi, maoni kuhusu umuhimu wa magazeti yanapolinganishwa na vyombo vingine vya habari, yametolewa na Ogechi (2002). Mtaalamu

huyu anasema kwamba, faida mojawapo ya magazeti ni kuwa ujumbe unaweza kudurusiwa mara kadhaa kabla ya kusambazwa; ni rekodi ya kudumu ambayo inaweza kuhifadhiwa.

Nchini Kenya, magazeti ya mwanzo yalianza kuchipuka katika mji wa Mombasa kuanzia mwongo wa mwisho wa karne ya kumi na tisa hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini. Ni katika kipindi hiki ambapo wamishionari, wafanyabiashara na wakulima wazungu (masetla) walianza kuingia Afrika Mashariki. Chimbuko la magazeti linahusishwa na makundi hayo matatu ya wageni pamoja na serikali ya kikoloni iliyofuatia. Mazingira hayo ya uchapishaji yalipelekea kuanzishwa kwa magazeti ya kampuni ya uchapishaji ya *Nation* na Mstahiki Aga Khan. Gazeti la *Taifa Leo* liliasisiwa mnamo 1959 ilhali lenzake *Daily Nation* likaanzishwa 1960.

Magazeti yachapishwayo kwa lugha ya Kiswahili yanaweza kuchukua nafasi kubwa kama vyombo vya kuwasilishia ujumbe nchini Kenya. Hali hii inatokana na jukumu la Kiswahili kama lugha ya taifa. Asemavyo Chimerah (1998), lugha hii inaeleweka na kutumiwa na watu wengi katika miktadha mbalimbali katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wazo kwamba Kiswahili ni lugha ya matumizi mapana miongoni mwa Wakenya limesisitizwa pia na Kimemia (2001). Whiteley (1969:1), naye anasema hivi:

> *"... Kiswahili kimekuwa lugha ambayo imejulikana Kwa mapana, hufundishwa, hujadiliwa na huzungumzwa zaidi barani Afrika kuliko lugha nyingine yoyote ...."*

Anaendelea kueleza kuwa kuchaguliwa kwa Kiswahili kama lugha inayotumiwa na watu wengi barani Afrika, kumetokana na hali kwamba lugha hii haiambatanishwi na kabila lolote ingawa inatambuliwa kuwa ni mojawapo ya lugha za Kibantu. Hata hivyo tarakimu zinaonyesha kwamba usomwaji wa *Taifa Leo* ni wa kiwango cha chini unapolinganishwa na ule wa magazeti ya Kiingereza, hususani *Daily Nation*. Ingawa Kiswahili ni lugha ya taifa na huzungumzwa na idadi kubwa ya Wakenya, kinaya kinachojitokeza ni kwamba magazeti yaandikwayo katika lugha hii, hayasomwi na watu wengi kulingana na tarakimu zilizotolewa na kampuni ya magazeti ya *Nation* (2004). Tarakimu hizo zinaonyesha kuwa *Daily Nation* husomwa na watu takriban milioni tano na laki saba kila siku ilhali *Taifa Leo* ina wasomaji milioni moja kwa siku. Aidha, katika kuzungumzia hali ya usomaji wa magazeti ya Kiswahili miongoni mwa wasomi nchini Kenya, Onyango (1990), anasema kuwa wasomi wengi hawapendi kuyasoma magazeti hayo kwa kuwa yana upungufu wa lugha sanifu.

1.2 Suala la Utafiti

Matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo* (kuanzia sasa GTL), yana kasoro mbalimbali. Tasnifu hii imejikita katika kuchunguza kasoro zinazojitokeza katika maumbo ya lugha ambayo yametumiwa kuwasilishia ujumbe kupitia kwa gazeti husika. Onyango (1990), anasema kwamba magazeti yaandikwayo kwa Kiswahili yana upungufu wa lugha sanifu, jambo ambalo hata huwafanya wasomi wengi wa Kiswahili kutoyatilia maanani sana. Madai haya ndiyo hasa kitovu cha utafiti huu ambapo tuna lengo la kutambua kasoro zinazojitokeza katika vipengele mbalimbali vya lugha katika makala yanayochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo*.

Kama vile anavyosema Mbaabu (1995), sababu ya kuwa na lugha sanifu ni kurahisisha mawasiliano katika mazungumzo na maandishi pia. Iwapo lugha itatumiwa bila kuzingatia usahihi wake, basi yaelekea kwamba mawasiliano yatakwama. Hivyo basi, kumekuwa na haja ya kuchunguza kasoro mahsusi zinazojitokeza katika matapo mbalimbali ya matumizi ya lugha katika makala yachapishwayo katika GTL. Utafiti huu unajibu swali: je, ni maumbo yapi ya lugha hutumiwa isivyostahili katika uandishi wa makala katika GTL?

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kudhihirisha matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo* (kuanzia sasa GTL). Uchunguzi umemulika hasa matumizi yasiyofaa ya lugha katika uandishi wa makala katika gazeti husika. Tumetimiza shabaha hii kwa:

(i). Kuchunguza matumizi mapungufu ya msamiati katika baadhi ya makala katika GTL.

(ii). Kutathmini tamathali za usemi zinazotumiwa katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL.

(iii). Kubainisha matumizi yasiyofaa ya methali na nahau katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL.

(iv). Kutambulisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL.

1.4 Nadharia Tete

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

(i) Baadhi ya msamiati unaotumika katika baadhi ya makala katika GTL ni mpungufu.

(ii) Baadhi ya tamathali za usemi hazitumiwi inavyostahiki katika baadhi ya makala ya GTL.

(iii) Baadhi ya methali na nahau hazitumiwi ipasavyo katika uandishi wa makala katika GTL.

(iv) Kanuni za kisarufi zinakiukwa katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL.

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Tunatumai kuwa matokeo ya utafiti huu yatakuwa mchango katika usomi wa lugha ya Kiswahili kwani yamefafanua na kuweka wazi taratibu na mikakati inayofungamana na uchanganuzi wa vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumiwa katika mawasiliano. Vipengele hivyo ni pamoja na: Sarufi, Msamiati, Methali, Nahau na Tamathali za Usemi.

Kwa wanafunzi ambao wanataalamia somo la Kiswahili katika viwango mbalimbali hasa katika Vyuo Vikuu, kazi hii itawaelekeza kuhusu matumizi ya lugha sahihi ili kufanikisha mawasiliano. Mifano ya makosa yaliyochanganuliwa, itawaongoza katika harakati zao za kuimarisha kiwango chao cha lugha kwa kujibidiisha kuepuka makosa yaliyodhihirishwa kupitia kwa tasnifu hii.

Walimu wa somo la Kiswahili katika ngazi mbalimbali nao huenda wakanufaika kutokana na utafiti huu, kwa kuwa umeweka wazi matumizi ya lugha isivyostahiki katika uandishi. Matapo ya lugha yaliyoshughulikiwa yatarahisisha kazi yao ya kuwaongoza wanafunzi wao ili waepuke makosa yaliyochanganuliwa katika kazi hii.

Kwa vyuo vinavyofundisha taaluma ya uandishi wa habari, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa na manufaa makubwa. Ugunduzi wa uchunguzi huu, utawaelekeza wahusika kuhusu haja ya kuwa makini katika matumizi yao ya lugha ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kikamilifu. Mifano halisi kutokana na kazi hii inaweza kutumiwa katika ufundishaji wa maumbo mbalimbali ya lugha ambayo ni muhimu katika juhudi za upashaji habari.

Tunatumai kuwa, matokeo ya utafiti huu yatanufaisha mashirika ya uchapishaji wa magazeti, hususan *Taifa Leo*, kwani inawezekana maoni yaliyotolewa yakawapa mwelekeo kuhusu njia za kuboresha matumizi ya lugha katika magazeti yao. Kwa waandishi wa habari na makala mbalimbali yanayochapishwa katika GTL, matokeo ya utafiti huu yameweka wazi mbinu zinazofaa kuzingatiwa ili kuimarisha kiwango chao cha uandishi hasa kwa kuepuka makosa ambayo yamechanganuliwa katika utafiti.

Utafiti huu umejaza pengo lililoachwa na tafiti za awali kama vile utafiti wa Onyango(1990). Mtaalamu huyu ametaja kwamba kuna kasoro katika lugha inayotumiwa katika magazeti ya Kiswahili. Hata hivyo, hakuyatambulisha makosa mahsusi yanayojitokeza namna ambavyo tumefanya katika utafiti huu.

Ubora wa GTL ukihakikishwa, wananchi wa Kenya watanufaika kwani haja ya mawasiliano kamilifu itakidhiwa. Gazeti hili litakuwa chombo muhimu nchini Kenya, kitakachopelekea usambazaji wa habari kufaulu zaidi. Ustawishaji na uenezaji wa Kiswahili kama lugha ya taifa, utasukumwa mbele. Pia tunatumai kuwa kazi hii itachochea utafiti zaidi katika nyanja hii.

1.6 Upeo wa Utafiti

Ingawa kuna magazeti mengi yanayochapishwa nchini Kenya kama vile *The Daily Nation, The East African Standard, Kenya Times* na *The People*, utafiti huu ulijikita katika gazeti la *Taifa Leo* tu na hivyo kutoyahusisha hayo mengine. Gazeti hili liliteuliwa kama chanzo cha data ya utafiti kutokana na hali kwamba ndilo gazeti la kipekee linalochapishwa na kusambazwa nchini kote. Hali hii inafuatia kukoma kuchapishwa kwa gazeti la *Kenya Leo* mnamo 1996 na hivyo kupelekea *Taifa Leo* kubaki kama gazeti la kipekee la kitaifa. Kutokana na makala mbalimbali yanayochapishwa katika gazeti husika, utafiti huu ulijihusisha na makala ya habari kuu, tahariri, maoni, na hadithi. Makala haya yalichaguliwa kwa misingi kwamba yana umuhimu mkubwa katika gazeti hilo kwa kuwa yanachangia utekelezaji wa malengo makuu ya vyombo vya habari ambayo ni: kufahamisha, kuelimisha na kuburudisha. Makala ya habari kuu hulenga katika kufahamisha na hivyo kutekeleza jukumu la kimsingi la gazeti lolote katika jamii. Kwa upande mwingine, tahariri na maoni ni makala yanayojikita katika kueleza na kufafanua habari kwa kina kwa lengo la kuwaelimisha wasomaji. Tahariri yaweza kufasiri, kuhakiki au kukubaliana na ujumbe unaotokea katika habari ichapishwayo katika gazeti hilo. Nayo makala ya hadithi, hunuiwa kuburudisha na kutoa mafunzo kwa wasomaji.

Ni wazi kuwa gazeti hujengwa na vipengele anuwai mbali na kile cha lugha mathalan: Muundo na yaliyomo. Aidha, ingawa kuna mambo mengine yanayoweza kuchangia kutosomwa kwa magazeti ya Kiswahili na watu wengi kama vile mvuto wa Kiingereza na sera ya lugha inayoelekea kupendelea Kiingereza, utafiti wetu uliochunguza kipengele cha matumizi ya lugha pekee. Hali hii inatokana na vikwazo vya wakati na haja ya kujikita katika lengo kuu la utafiti.

Utafiti huu umechanganua matumizi ya lugha katika nakala thelathini za gazeti husika. Nakala hizi ziliteuliwa kutokana na jumla ya zile ambazo zimechapishwa katika kipindi cha miaka mitano ya hivi majuzi (1999-2003). Idadi hii ilifikiwa kwa kuzingatia uwezekano kuwa matini inayoshughulikiwa ikichunguzwa katika kipindi cha urefu huo, itaonyesha ruwaza ya kipengele kilichozamiwa ili kutoa rai zenye mashiko.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumechunguza maandiko mbalimbali ambayo yanahusiana na mada ya utafiti inayoshughulikiwa. Tumejikita katika maandiko ambayo yanahusu vipengele vifuatavyo: lugha kama msimbo wa mawasiliano; matumizi ya lugha katika vyombo vya habari; methali na nahau; tamathali za usemi; sarufi na msamiati. Waaidha, tumeonyesha nadharia iliyouongoza utafiti wetu.

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Suala la matumizi ya lugha katika mawasiliano limepewa umuhimu mkubwa katika tafiti mbalimbali. Katika kupitia vitabu, majarida na tafiti, tulipata maandishi ambayo yameshughulikia matumizi ya lugha katika nyanja mbalimbali kama vile mawasiliano kupitia kwa vyombo vya habari na fasihi. Aidha, tulipitia maandishi ambayo yamefafanua vipengele muhimu vya lugha na matumizi yao katika miktadha mbalimbali. Hata hivyo hatukuona maandishi yoyote ambayo yameshughulikia matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya.

Tumegawa maandishi tuliyoyapitia katika matapo mbalimbali kwa lengo la kuweka wazi, kwa njia yenye mantiki zaidi sehemu zilizowahi kushughulikiwa. Matapo hayo yameshughulikiwa hapa chini, moja baada ya lingine.

2.2.1 Lugha kama msimbo wa mawasiliano

Ogechi (2002), amechunguza dhana ya mawasiliano na nyenzo mbalimbali zinazotumika katika usafirishaji wa ujumbe kutoka kwa mtuma-ujumbe hadi kwa mpokea-ujumbe. Anasema kuwa lugha ndiyo ambayo imefanikiwa zaidi katika suala la mawasiliano ya kufikisha ujumbe kati ya mtu na mtu, na kati ya taifa na taifa. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa inaonyesha umuhimu mkubwa wa lugha katika mawasiliano ya jamii yoyote ile, jambo ambalo tulilifuatilia katika utafiti huu. Ni bayana kwamba, lugha ni mhimili muhimu wa mawasiliano na matumizi yake ndiyo ambayo hutawala kufaulu au kutofaulu kwa upitishaji ujumbe. Hivyo basi, ni katika mkabala huu, ambapo tumechunguza jinsi lugha imetumiwa isivyofaa katika uandishi wa makala ya GTL. Misingi ya kazi hiyo inatofautiana na utafiti huu kwani, Ogechi (ibid) anajikita katika suala la lugha inavyotumika katika

kufanikisha mawasiliano baina ya watu kwa jumla ilhali sisi tulichunguza jukumu la lugha kama chombo cha mawasiliano kupitia kwa matumizi yake katika GTL.

Kuhusu umuhimu wa lugha, Lumwamu (1997), anasema kwamba lugha ni chombo cha mawasiliano ambapo mshiriki mmoja huwasilisha ujumbe kwa mwingine ili kutekeleza majukumu tofauti kama vile kuarifu, kuamrisha na kushawishi. Walkin (1982), naye anasema kuwa lugha huchukua nafasi kubwa katika mawasiliano baina ya binadamu. Anasisitiza kuwa mtu huamua ni kipi cha kusema, akiseme lini na namna ya kukisema ili kiwe na athari zaidi. Kazi hizi zinatoa mwanga kuhusu namna lugha inavyotumiwa na mwasilishaji ujumbe kwa njia mbalimbali ili kuleta athari anayoitaka kwa hadhira yake. Kutokana na kazi hizi, utafiti huu ulielekezwa hususan katika ugunduzi wa jukumu la lugha katika kufanikisha mawasiliano yanayonuiwa. Mawazo ya wataalam hawa, yamepelekea kuwepo kwa haja ya kuchunguza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ili kugundua namna ujumbe umewasilishwa katika matini mahsusi. Tofauti na kazi hizi ambazo zinatoa majukumu mbalimbali ya lugha katika mawasiliano, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza matumizi ya lugha kama kipengele muhimu kihusikacho katika uwasilishaji wa ujumbe kupitia kwa GTL.

Kwa mujibu wa Nkwera (1978), lugha ni chombo cha kupashana habari au kuwasiliana. Anaendelea kueleza kuwa matokeo ya kuwasiliana huku ni kuafikiana au kufarakana; kujenga au kubomoa; kuleta vita au kuleta amani. Anasisitiza kuwa matokeo hayo hutegemea taarifa na kweli zinazotolewa, pia namna nzuri au mbaya ya kuwasilisha taarifa hizo. Maelezo ya mtaalam huyu yanaweka wazi jukumu linalotekelezwa na lugha katika kufanikisha mawasiliano. Msisitizo wake kuhusu nafasi na athari ya mtindo ambao unatumiwa katika uwasilishaji wa habari, kwa mawasiliano husika, ulikuwa muhimu kwa uchunguzi wetu ambao ulijikita katika kudhihirisha namna kasoro mbalimbali zimejitokeza katika matumizi ya lugha kwa kurejelea GTL. Mawazo ya Nkwera (ibid), yalikuwa dira ambayo iliuongoza utafiti wetu hasa katika kuzamia makosa yahusuyo matumizi ya lugha katika makala teule ya GTL. Ni muhimu kutaja hapa kwamba, ingawa anayoyasema Nkwera yamechangia pakubwa katika kuuelekeza uchunguzi wetu, ni bayana kuwa mtazamo wake kuhusu umuhimu wa lugha ulikuwa wa kijumla mno, ilhali sisi tulijishughulisha na jinsi ambavyo lugha imetumiwa katika makala mahsusi.

Akizungumzia nafasi ya lugha katika uandishi, Mwamzandi (2002), anaelezea kwamba iwapo mwandishi atatumia maumbo ya lugha yanayokanganya, basi hadhira hukipatia kipande husika muda zaidi wa kufikiria ni nini kilichomaanishwa. Aidha, akimnukuu Leech (1969), anasema kuwa mwandishi atakuwa ametumia lugha vizuri ikiwa: Atatumia kwa njia nzuri mbinu za lugha zinazojulikana katika lugha husika; atahusisha katika

uandishi wake mbinu zisizokuwa zile zinazojulikana. Kazi hii ilitudhihirishia umuhimu wa lugha inayoeleweka na sahihi katika kufanikisha mawasiliano. Mawazo haya yameweka wazi kigezo cha kutumia ili kufikia uamuzi kwamba mwandishi ametumia lugha vizuri na kinyume chake. Kazi ya Mwamzandi (ibid) ilitusaidia kuelewa umuhimu wa maumbo ya lugha ambayo hutumiwa katika mawasiliano. Ni kwa msingi huo ambapo tumechunguza ni maumbo yapi ya lugha yaliyotumiwa kwa njia isiyo sahihi katika uandishi wa makala ya GTL.

Wilkins (1972), akielezea kuhusu jukumu la lugha kama msimbo wa mawasiliano, anasema kuwa makala ya gazeti huandikwa ili yasomwe na ni shuruti yawasilishwe kwa uzingatiaji wa sarufi na leksia. Uneni asilia waweza kuripotiwa ama kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kuzingatia kanuni za usemi wa taarifa au kunukuliwa kwa njia ya moja kwa moja kwa misingi ya usemi halisi. Katika hali zote mbili, mwandishi wa makala hayo, atateua maneno ambayo yatawasilisha hisia za msemaji katika uneni husika. Mawazo haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa yanaonyesha umuhimu wa uzingatiaji wa kanuni za kisarufi na za kileksia katika kuwasilisha ujumbe kupitia kwa lugha. Ni wazi kwamba, iwapo mwandishi atakiuka kanuni za kisarufi na kuteua maneno bila makini, huenda anayonuia kuwasilisha kwa hadhira yasieleweke alivyokusudia. Anayoyasema Wilkins (ibid), yalituongoza katika kuzamia vipengele vya sarufi na msamiati kama vinavyojitokeza katika GTL. Hata hivyo kazi hiyo inatofautiana na hii yetu, kwa kuwa Wilkins alishughulikia jukumu la sarufi na leksia katika uandishi wa makala katika magazeti kwa jumla ilhali sisi tulichunguza namna vipengele hivyo viwili vinavyojitokeza katika gazeti mahsusi, yaani *Taifa Leo*.

2.2.2 Matumizi ya lugha katika vyombo vya habari

Crystal na Davy (1969), wakielezea lugha inayotumiwa katika magazeti, wanasema kuwa waandishi wa makala hulenga kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye mvuto kwa hadhira ambayo wanaijua. Waandishi wawili au zaidi wa magazeti, wanaweza kuzungumzia jambo moja lakini kwa kutumia mitindo na taratibu tofauti kutegemea mambo yanayosisitizwa. Kazi ya Crystal na Davy (ibid), ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani inatoa mwanga kuhusu masuala yanayohusiana na mitindo ya lugha kwa ujumla. Mjadala kuhusu mitindo inayotumiwa katika uandishi wa magazeti ulikuwa muhimu kwa utafiti huu ambao ulichunguza matumizi ya lugha katika GTL. Mawazo haya yanaashiria kuwa, hata katika matumizi ya lugha, waandishi huenda wakadhihirisha tofauti waandikapo matini zao. Msingi

huu ulituwezesha kutathmini matumizi katika viwango mbalimbali vya lugha kwa lengo la kubainisha makosa yaliyojitokeza humo. Hata hivyo, kazi hiyo inatofautiana na utafiti huu kwa kuwa, Crystal na Davy (ibid), wameshughulikia mitindo ya waandishi inavyojitokeza katika magazeti ya Kiingereza ilhali sisi tulijikita katika matumizi ya Kiswahili katika GTL.

Mlacha (1995), akizungumzia kuhusu vyombo vya habari katika jamii, anasema kuwa tatizo lililopo hivi sasa ni kubwa mno kwani yapo magazeti mengi na redio nyingi; wapo waandishi na watangazaji wengi lakini utaalamu wa lugha ya Kiswahili haujawafikia waandishi na watangazaji hao. Anaendelea kueleza kwamba mafanikio ya vyombo vya habari katika kufikisha ujumbe kwa usahihi kwa watu, yanategemea sana uelewa mzuri wa waandishi wa habari wa istilahi zinazohusiana na mada anuwai wanazozishughulikia. Bila uelewa huo, vyombo vya habari vinaweza kuwapotosha wasomaji na wasikilizaji badala ya kuwafahamisha vilivyo. Mbali na maelezo haya kusisitiza kwamba kuna upungufu katika matumizi ya lugha katika uandishi wa magazeti na utangazaji redioni, pia yanaonyesha umuhimu wa kutumia istilahi sahihi ili kugonga ndipo katika uwasilishaji wa ujumbe. Aidha, msisitizo wa mtaalamu huyu kuhusu haja ya waandishi wa habari kutumia istilahi sahihi, umechangia uelewa wetu wa nafasi ya msamiati katika kufanikisha mawasiliano kupitia kwa GTL na hivyo kuweza kuweka wazi matumizi yasiyoafiki ya kipengele hicho katika matini husika. Mawazo anayoyapalilia mtaalam huyu, yanalandana na makisio yetu kuhusu matumizi ya maumbo mbalimbali ya lugha kwa kurejelea makala yachapishwayo katika GTL. Anavyosema, kuna ukosefu wa utaalamu wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa waandishi wa habari na hivyo kupelekea matumizi ya lugha isiyo na usanifu. Hata hivyo ingawa kazi ya Mlacha (ibid), imetoa mwanga kwa utafiti huu kwa kusisitiza umuhimu wa utaalamu wa lugha kwa uandishi na utangazaji, yeye hakuonyesha ni vipengele vipi vya lugha ambavyo vimetumiwa isivyostahili katika nyanja husika. Hili ndilo pengo linalofidiwa na utafiti huu ambao ulichunguza makosa mahsusi katika matumizi ya lugha kwa kurejelea GTL.

Kiganya (1995), akieleza kuhusu matumizi ya lugha katika magazeti ya Kiswahili, anasema kuwa rejista mbalimbali za lugha zinajitokeza kuambatana na aina ya habari au makala yanayoandikwa. Anasisitiza kwamba rejista rasmi na ambayo inazingatia kanuni zote za Kiswahili sanifu, ndiyo inayotumika katika kuandika habari, tahariri na makala maalumu. Maelezo haya yalitufaa katika utafiti huu hasa kwa kutuelekeza kuhusu kigezo cha kupimia lugha iliyotumiwa kuandikia makala tuliyoyachunguza. Ugunduzi kuhusu aina ya rejista

inayotarajiwa kujitokeza katika makala husika, ilikuwa muhimu kwetu katika kufikia uamuzi kuwa vipengele fulani vya lugha vilitumiwa isivyostahiki. Hii ilikuwa kazi ya kimsingi kwa ajili ya uchunguzi wetu, kwani ilitupa kigezo muhimu cha kutathminia matumizi ya lugha katika kazi yetu ili kutoa rai zinazoweza kuthibitishwa kutokana na ushahidi ulio wazi. Ingawa kazi ya Kiganya (ibid), ilikuwa na umuhimu wa kipekee kwa utafiti huu, ni wazi kwamba haikujihusisha kwa vyovyote vile na kasoro zinazodhihirika katika lugha itumiwayo katika magazeti hayo. Hili ndilo pengo linalozibwa na kazi yetu.

Naye Rweyememu (1995:76-77), akigusia matumizi ya lugha katika vyombo vya habari, anasema:

> *"... kutokana na imani ambayo wasomaji wa magazeti na wasikilizaji wa redio waliyojijengea kuwa chochote kile kinachozungumzwa katika redio au kinachoandikwa katika magazeti ni sahihi, huwafanya waige kwa haraka sana kila kitu kinachojitokeza katika vyombo hivyo vya habari hata kama ni makosa. ...Kwa kweli uandishi wa habari ni lugha: bila lugha, na lugha iliyo sahihi hakuna uandishi. Ujuzi wa lugha fasaha ni nyenzo kuu katika kazi hii. Kwani umuhimu wa lugha kwa mwandishi wa habari, ni sawa kabisa na bunduki kwa askari au jembe kwa mkulima...."*

Ingawa utafiti wetu haukujihusisha na lugha inavyotumiwa redioni, mawazo ya mwandishi huyu kuhusu haja ya kutumia lugha sahihi katika uandishi wa magazeti, yalitufaa sana. Msisitizo wa Rweyememu (ibid) kuhusu athari za matumizi ya lugha yasiyofaa katika vyombo vya habari, ulituonyesha haja iliyopo ya kuweka bayana makosa yanayojitokeza katika makala yanayolenga kupitisha ujumbe kwa hadhira. Uchanganuzi wetu wa matumizi ya lugha katika magazeti ya Kiswahili nchini Kenya ulipata msukumo kutokana na kazi hii kwa kuwa ulilenga kuchunguza makosa yaliyojitokeza humo. Aidha, katika za kutathmini uteuzi wa maneno ambayo yametumiwa kuwasilishia habari kupitia kusisitiza umuhimu wa lugha sahihi katika machapisho, Dadi (1995), anasema kuwa machapisho ambayo yanazidi kuongezeka siku hadi siku, hayana budi kuwa makini katika uteuzi mzuri wa maneno kwani yanayotoka kwa waandishi hao kwenda kwa wageni huchukuliwa kuwa ni bora na sahihi. Maelezo haya yalitupa changamoto katika juhudi zetu kwa makala teule ya GTL.

Onyango (1990), alichunguza kindani mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Anasema kuwa wasomi wengi hawapendi kuyasoma magazeti

yaandikwayo kwa Kiswahili kutokana na matumizi ya lugha yenye upungufu wa ufasaha. Kwa kuwa utafiti wa Onyango ulionyesha kuwa wasomi wana mielekeo hasi kuhusu magazeti ya Kiswahili kwa sababu ya lugha yenye kasoro itumikayo humo, utafiti huu ulinufaika kutokana na msingi huo ambapo tulizamia kipengele cha matumizi ya lugha na kuchunguza namna maumbo mbalimbali ya lugha, yalitumiwa isivyostahiki katika gazeti husika. Utafiti wa Onyango unatofautiana na huu wetu kwa kuwa yeye alichunguza mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali ilhali sisi tulichunguza matumizi ya lugha katika *Taifa Leo.* Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha madai ya Onyango (ibid), kuwa kuna matumizi ya lugha yaliyo na upungufu wa ufasaha katika magazeti ya Kiswahili nchini Kenya.

2.2.3 Methali na Nahau

Methali na nahau ni maumbo ya lugha ambayo huchukua nafasi muhimu katika mawasiliano andishi. Ujumbe mzito waweza kuwasilishwa kupitia kwa matumizi sahihi ya maumbo haya. Lugha ya mkato ambayo hutumika katika methali na nahau hupelekea ujumbe wa kina kupitishwa kwa ufupi na kwa njia inayoleta athari za kipekee kwa msomaji. Kwa mujibu wa Nkwera (1978:97):

> *"...Methali ni semi au kauli zenye busara na mafunzo kuhusu maisha na mahusiano ya watu. Ukweli na umuhimu wa methali yoyote hutegemea mazingira inamotumika. Methali ni kauli za mkato (fupi) na zenye kufikirisha. Methali zadai ujuzi wa kuzifafanua, maana pengine huwa ni mafumbo. Hutumika ili kumjuvya mtu ukweli fulani, au kumshitua apate kudadisi mambo au kujisahihisha anapokosa...."*

Msisitizo wa Nkwera kuwa umuhimu wa methali hutawaliwa na mazingira inamotumika ndicho kipengele ambacho kimetufaa sana katika uchunguzi wetu. Wazo hilo, lilituelekeza katika juhudi zetu za kutathmini ufaafu wa matumizi ya methali mbalimbali kwa kuzingatia muktadha ambamo zimetumika. Ni kutokana na maelezo ya mtaalam huyu ambapo tulipata kigezo kilichotuwezesha kufikia uamuzi kuwa baadhi ya methali hazikutumika inavyofaa katika matini tuliyochanganua.

Mtesigwa (1989), akizungumzia matumizi ya methali katika kuwasilisha ujumbe, anasema kuwa, mawasiliano katika lugha ya binadamu hayakidhiwi kwa kuwepo kwa mkururo wa msamiati au kanuni za kisarufi zinazolinda ufasaha wa tungo tu. Anaendelea kueleza kuwa, wakati mwingine maana hufutikwa kwa sanaa mahsusi ambayo huipa lugha uhai licha ya maana ambayo hubebwa na maneno yale yale katika hali ya kawaida. Methali

huvutia zaidi iwapo itatolewa kwa maneno machache au mafupi na hasa ikiwa, licha ya hayo, pia maneno hayo yanagonga ndipo katika kukisema kilichokusudiwa kusemwa. Mawazo haya yanatilia nguvu umuhimu wa methali katika kufanikisha mawasiliano katika jamii endapo zitatumiwa kwa njia mwafaka. Inabainika kuwa methali ni kiungo muhimu katika uwasilishaji wa habari hasa inapozingatiwa kwamba, ujumbe unaosheheni umbo hili huandamana na busara ya kipekee. Ni muhimu kuelewa maana ya maneno yatumikayo katika methali mbalimbali ili kuuelewa ujumbe uliomo vizuri. Kazi hii ilikuwa mchango kwa utafiti huu kwani ilituonyesha kuwa methali ni kipengele muhimu cha lugha ambacho huchangia katika kufanikisha mawasiliano. Tofauti iliyopo kati ya kazi hiyo na utafiti huu ni kuwa, Mtesigwa alichunguza matumizi ya methali katika fasihi wakati ambapo sisi tulitathmini jinsi methali zimetumiwa katika mawasiliano kupitia kwa GTL.

Maitaria (1991), akiandika kuhusu matumizi ya methali katika mawasiliano, anasema kuwa, methali za Kiswahili zinavyofahamika ni sehemu muhimu katika lugha na zinaweza kutumiwa popote lugha hiyo inapotumika. Nao Karama na Saidi (1983), wanasema kuwa methali ni pambo zuri sana la lugha ambalo hutumiwa katika mawasiliano kwa lengo la kuivutia hadhira. Kazi hizi zilitufaa sana katika kufafanua jukumu linalotekelezwa na methali katika mawasiliano. Ni kwa msingi huu ambapo utafiti wetu umejihusisha na namna methali zimetumiwa kwa njia isiyofaa katika uandishi wa baadhi ya makala ya GTL.

Petrenko (1986), amechunguza kwa undani dhana ya nahau, sifa za kuzitambulisha na sifa za umbo lao. Anafafanua nahau kama fungu la maneno lisilogawanyika kimaana kwani maana ya jumla haitokani na neno moja moja. Aidha nahau ni kauli yenye umbo na muundo maalum ambayo hutumika katika lugha kama kauli moja inayoleta taswira ya mafumbo. Maelezo haya yanaweka wazi aina mbalimbali za nahau zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili na jukumu la nahau hizo katika kuibua picha maalumu kuhusu mambo yanayozungumziwa. Msisitizo kuhusu muundo wa nahau ni kigezo kimojawapo kilichotuwezesha kuamua kwamba nahau fulani zilitumiwa isivyostahiki katika makala tuliyoyachunguza. Kauli anazotoa Petrenko (ibid), zilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa zilitusisitizia mchango mkubwa wa nahau katika kufanikisha mawasiliano kutokana na uwezo wake wa kujenga taswira mbalimbali kulingana na ujumbe unaonuiwa kuwasilishwa. Ingawa hivyo, kazi hiyo ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa Petrenko ameipalilia dhana ya nahau na sifa zake kwa mkabala wa matumizi yake katika lugha ya Kiswahili ilhali kwa upande wetu tulitathmini matumizi ya nahau katika makala ya GTL.

Naye Carter na wenziwe (1997), wanasema kuwa, nahau huwawezesha watumiaji wa lugha fulani kuwasilisha maana inayoeleweka na kukubalika; huipamba lugha na kuifanya

kutosheleza haja ya mawasiliano bila kuichosha hadhira. Aidha, nahau huwa na muundo mahsusi na wakati wa kuchanganuliwa, hupaswa kuchukuliwa kama maneno na wala siyo kama virai. Inabainika kwamba, matumizi sahihi ya nahau, hupelekea ujumbe unaowasilishwa kumfikia anayelengwa kwa njia yenye mvuto. Haya ni maelezo muhimu kwa kuwa yanaweka wazi jinsi nahau huweza kutumiwa ili kuhuisha lugha inayotumiwa katika mawasiliano. Utafiti huu ulinufaika kutokana na maelezo hayo kwa kuwa tulijikita katika kuchunguza jinsi nahau zimetumiwa isivyostahiki katika makala ya GTL.

2.2.4 Tamathali za Usemi

Wakieleza kuhusu tamathali za usemi (kuanzia sasa TZU), Mulokozi na Kahigi (1979), wanasema kuwa TZU ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana maalumu iliyokusudiwa na mtunzi au mzungumzaji. Wanaendelea kufafanua kuwa tamathali nzuri huyakinisha na kuipa uhai na uhalisi zaidi dhana inayoelezwa, huburudisha na kuzindua akili ya msomaji au msikilizaji na kuacha athari ya kudumu katika hisi na mawazo yake. Ili TZU ziweze kutekeleza majukumu mbalimbali kwa mujibu wa wataalam hawa, inamlazimu mwandishi husika kuteua na kutumia maumbo aliyo na uhakika nayo kimatumizi. Hali hii ndiyo itakayomwepushia matumizi yasiyofaa ya umbo hili na hivyo kutoa ujumbe anaokusudia kwa uwazi zaidi. Maelezo haya, ambayo yanaweka wazi dhana ya TZU na jukumu lake katika mawasiliano kwa jumla, yalikuwa muhimu kwa utafiti huu ambao ulizamia namna TZU zinavyotumiwa katika GTL. Mawazo makuu ya waandishi hawa kuhusu TZU yametoa mwanga kuhusu ni mambo yapi ya kuzingatiwa katika juhudi za kuchunguza iwapo TZU zimetekeleza jukumu lake katika mawasiliano. Mwanga huu, ulitusaidia kugundua mengi kuhusu kipengele husika katika utafiti huu.

Khatibu (1999:76-77), naye ameandika kuhusu umuhimu wa TZU katika fasihi. Anasema:

> *"...nazo tamthiliya zimeshehenezwa semi tumbitumbi ili ziweze kuteka masikizi na maoni ya watazamaji au wasikilizaji. Semi hizi ndizo zinazoipa hadhi na heshima sio fasihi ya Kiswahili tu katika fani yake bali pia zinaifungua uso lugha yenyewe na kuwapa ariha watunzi kutunga kile wakipendacho kwa kifua mbele. Utamu wa lugha haupo tu katika maudhui yaani kile kinachoelezwa, bali pia ladha ya lugha huzidi kwa ustadi wa kuyaeleza maudhui yenyewe ...."*

Ufafanuzi wa mwandishi huyu kuhusu matumizi ya TZU katika fasihi ili kupitisha ujumbe

kwa hadhira, yalichangia uelewa wetu wa umuhimu wa TZU katika kufanikisha mawasiliano. Utamu wa lugha unaosisitizwa hapa una jukumu kubwa katika kuwavutia wasomaji wa matini. Ni bayana kuwa iwapo TZU zitatumiwa kwa njia inayofaa, uwasilishaji wa habari utafaulu zaidi. Maelezo hayo yalitoa changamoto kwa utafiti huu ambao ulijihusisha na matumizi ya lugha katika GTL, ambapo kipengele cha TZU kilichunguzwa. Naye Ohly (1990), anawasifu sana waandishi wa Visiwani kwa sababu wana matumizi mazuri ya TZU na msamiati. Mtaalamu huyu hatosheki tu na hali kwamba TZU hutumiwa katika uandishi bali anasisitiza matumizi yake kwa usahihi. Msisitizo huu ndio ambao ulisisitizwa katika utafiti huu ambapo jukumu la TZU katika kufanikisha upitishaji ujumbe kupitia kwa GTL, lilizamiwa.

Miles na wenziwe (1991), wakidokezea jukumu la TZU katika uandishi, wanasema kuwa TZU huipamba kazi husika. Wanasisitiza mawazo ya Aristotle kuwa, TZU huvyaza weledi, msukumo na ulimbwende. Maelezo haya yanaonyesha kuwa TZU ni kipengele muhimu katika uandishi wa kazi yoyote kutokana na sifa yake ya kuleta uhai katika uwasilishaji wa ujumbe. Matumizi sahihi ya umbo hili ni muhimu katika juhudi za kuipamba kazi husika. Iwapo TZU zitatumiwa kwa njia isiyofaa, basi yaelekea kwamba mawasiliano yataathirika pakubwa. Hili ni wazo muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa linasisitiza jambo ambalo tulilishugulikia katika harakati za kudhihirisha namna lugha ilivyotumiwa katika GTL.

Kwa mujibu wa Musyoka (1996), matumizi ya TZU katika uandishi huweza kuondoa ukavu ama mfululizo wa ukawaida unaoweza kujitokeza katika lugha ya kawaida. Anaendelea kueleza kuwa maumbo haya ya lugha yanapotumiwa inavyohitajika na katika miktadha ifaayo, athari zake huwa ni kutia ujumi katika lugha iliyotumiwa, yakairemba na kuipa sura ya kupendelewa na msomaji. Naye Kamau (1992), anaongezea kwamba matumizi sahihi ya lugha ya kitamathali huibua picha inayonuiwa ilhali kinyume chake hupelekea ujumbe kutoeleweka. Kazi hizi, zilituelekeza katika uchunguzi wetu ambao ulilenga kuonyesha matumizi yasiyofaa ya TZU katika makala teule ya GTL. Msisitizo wa wataalam hawa ulitusaidia katika kupima usahihi wa TZU zilizotumiwa katika makala tuliyoyachanganua katika utafiti wetu.

2.2.5 Sarufi na Msamiati

Kuhusu sarufi, Pei na Gaynor (1969), wanasema kuwa hii ni sayansi ya muundo wa lugha pamoja na sheria na kanuni za matumizi yake ambayo, kwa kawaida, hukubalika kwa watumiaji. Maelezo ya waandishi hawa yanachukuana vizuri na yale yaliyotolewa na

Massamba na wenziwe (1999), ambao wanatoa mitazamo miwili katika kuelezea dhana ya sarufi. Kwanza, wanasema kuwa sarufi ni taaluma ya uchambuzi wa lugha inayojumuisha viwango vyote vya uchambuzi, yaani, kiwango cha umbo-sauti (Fonolojia); kiwango cha umbo-neno (Mofolojia); kiwango cha miundo-maneno (Sintaksia) na kiwango cha umbo-maana (Semantiki). Pili, sarufi ni kanuni, sheria au taratibu zinazotawala kila kimoja kati ya viwango vinne vilivyotajwa hapo juu na ambazo zinakifanya kila kiwango kikubalike katika taratibu za usemaji wa lugha inayohusika. Fafanuzi hizi kuhusu dhana ya sarufi zinachangiana na kukamilishana kwa kuwa jambo muhimu linalosisitizwa ni kuwa lugha huwa na viwango mbalimbali ambavyo hutawaliwa na kanuni fulani zinazofuatwa na watumiaji wa lugha hiyo. Maelezo ya wataalamu hawa yanatoa mwongozo kuhusu vipengele muhimu vinavyopaswa kuzingatiwa katika kuchunguza kukiukwa au kufuatwa kwa kanuni za kisarufi katika uandishi au mazungumzo. Umuhimu wa sarufi kama msingi wa lugha yoyote ile, hauwezi kupuuzwa. Kueleweka kwa ujumbe unaowasilishwa kunategemea kwa kiasi kikubwa uzingatiaji wa taratibu za kisarufi kwa mujibu wa vipengele vilivyoainishwa na wataalam tuliowataja. Utafiti huu, ulinufaika kutokana na mwongozo huu kwa kuwa tulichunguza kukiukwa kwa taratibu za kisarufi katika GTL.

Nkwera (1978), ameielezea sarufi kama mfumo au utaratibu wa kanuni unaomwezesha mzawa au mtumiaji yeyote wa lugha: (i) Kutoa tungo sahihi na zinazoeleweka na, (ii) kuelewa tungo zinazotolewa na mtu mwingine anayetumia lugha hiyo hiyo. Ufafanuzi huu umetoa mwanga kuhusu umuhimu wa tungo sahihi na zinazoeleweka kama kigezo cha kutathmini usarufi wa kauli zinazotolewa katika lugha yoyote ile kwa shabaha ya kufanikisha mawasilano. Haya yalikuwa maelezo muhimu kwa uchunguzi wetu ambao umebainisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi katika uandishi wa baadhi ya makala ya GTL. Tuliichukua tungo kama sehemu muhimu katika uchanganuzi wetu wa makosa ya kisarufi kwa mujibu wa matini husika.

Fries (katika Tumbo-Masabo, 1990), alipendekeza mbinu za kuutazama muundo wa lugha. Anasema kuwa sarufi ni uchunguzi wa maumbo ya lugha yaashiriayo maana katika muundo wake. Kuhusu uchambuzi wa sarufi, Fries (ibid) anasisitiza kwamba vipengele vinavyoweza kuchunguzwa ni pamoja na: Mpangilio wa maneno; vihusishi katika tungo; mnyambuliko wa maneno; maendelezo ya maneno na kiimbo (shadda, lafudhi, matamshi). Fries aliona kuwa, kutokana na njia hizo tano, tunaweza kupata muundo na maana katika lugha yoyote ile. Ingawa hajashughulikia vipengele vyote vinavyohusu sarufi, mwanga anaotoa ulitufaa katika utafiti huu hususan katika kuweka msingi wa kutambulisha makosa ya kisarufi katika matini iliyoshughulikiwa. Mambo aliyoyasisitiza, yalitusaidia katika kupata

vigezo vya kuamulia ni tungo zipi zilikiuka kanuni za kisarufi katika matini tuliyoichunguza. Hata hivyo ni muhimu kutaja kwamba kipengele cha kiimbo hakikuifaa kazi hii kwa kuwa kinahusu lugha ya mazungumzo ilhali tulishughulikia lugha inavyojitokeza katika maandishi.

Akielezea kuhusu sababu za kutaalamia kipengele cha sarufi, Kerrigan (1983), anasema kuwa, kwanza ni kumwezesha mhusika kuongea au kuandika kwa usahihi ili kutosheleza mahitaji ya miktadha mbalimbali ambapo namna ya kujieleza hutathminiwa. Pili, utaalamu kuhusu sarufi humfanya amaizi matapo ya lugha na uamilifu wao ili kumrahisishia kazi ya kusahihisha makosa yake katika uzungumzi na uandishi. Msisitizo huu kuhusu usarufi ulikuwa muhimu katika utafiti huu, kwani ulituangazia kuhusu umuhimu wa kuzingatia kanuni za kisarufi ili kurahisisha mawasiliano. Katika utafiti wetu tulijikita katika uwasilishaji wa habari kupitia kwa maandishi. Kwa hivyo mawazo haya ya Kerrigan (ibid), yalitufaa kwa kuwa yanaweka wazi jukumu la sarufi katika upitishaji wa ujumbe. Uchunguzi wetu umeonyesha namna kanuni za kisarufi zimekiukwa katika baadhi ya makala yachapishwayo katika GTL.

Mbaabu (1995), akiandika kuhusu usahihishaji wa makosa katika Kiswahili, anasema kuwa makosa ya kimaana kwa wingi yanasababishwa na upungufu wa msamiati. Anaendelea kusema kuwa makosa ya aina hii hujitokeza katika kiwango cha sentensi. Kueleweka kwa ujumbe wowote kunategemea uwezo wa sentensi wa kuweka wazi jambo linalozungumziwa. Matumizi ya msamiati unaofaa ni nguzo muhimu katika utunzi wa sentensi ambazo zinawasilisha habari kwa ukamilifu. Maelezo haya yanaonyesha wazi kwamba matumizi ya msamiati isivyostahiki, huathiri mawasiliano husika. Anayoyasema mwandishi huyu, yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa tulitathmini matumizi ya msamiati katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL.

Marius (1991) na Lannon (1983), wakizungumzia athari za matumizi yasiyo sahihi ya lugha, wanasema kuwa makosa ya kisarufi na ya kimsamiati husababisha kutoeleweka kwa ujumbe unaonuiwa kuwasilishwa. Wanaendelea kufafanua kwamba hadhi ya ujumbe huathiriwa na makosa ya kimsingi yanayojitokeza katika maandishi husika, hali inayopelekea hadhira kukanganywa. Yaelekea kwamba makosa katika vipengele hivi viwili huenda yakasababisha kutoeleweka kwa habari inayonuiwa kupitishwa. Msamiati na sarufi huchukua nafasi muhimu katika lugha yoyote ile hasa katika kufanikisha mawasiliano. Mawazo ya waandishi hawa, yalitoa mwanga kwa kazi yetu ambayo ilizamia namna makosa ya kisarufi na ya kimsamiati yamejitokeza katika baadhi ya makala ya GTL.

Wakieleza kuhusu makosa katika uandishi, Stewart na wenziwe (1978), wanasema kuwa, makosa ya kisarufi na matumizi yasiyofaa ya msamiati yanaweza kuzua utata na

kutoeleweka. Wanaendelea kueleza kuwa, ujumbe utatanishao husababishwa na mwandishi kushindwa kutumia neno, kirai au kishazi kwa njia inayofaa. Maelezo haya yalitufaa katika kazi yetu kwani yanadokeza kuhusu athari ya makosa mbalimbali pindi yanapotokea katika uandishi. Mawazo ya wataalamu hawa yanaonyesha haja iliyopo ya kuchunguza na kuweka wazi makosa yanayotokea katika matini mbalimbali kama tulivyofanya katika kazi hii kwa mujibu wa makala yachapishwayo katika GTL.

2.3 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo kama inavyofafanuliwa na Ngara (1982). Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, nadharia hii inasisitiza vigezo mbalimbali vya kutathmini mtindo wa matini yoyote ambayo inachanganuliwa. Vigezo anavyovisisitiza Ngara (ibid), ni pamoja na:

(i). Usomekaji wa kazi.
(ii). Lugha ya mwandishi.
(iii). Kufaa kwa sifa na vipengele vya kiisimu
(iv). Umuhimu wa maudhui na kiwango cha ujuzi wa mwandishi.
(v). Istilahi za mhakiki.
(vi). Heba na sifa za kibinafsi za mwandishi.
(vii). Tajriba ya mwandishi katika maisha.

Hata hivyo, utafiti wetu umeelekezwa na vigezo vitatu kati ya hivyo vilivyotajwa. Vigezo tulivyotumia ni: Usomekaji wa kazi; lugha ya mwandishi na kufaa kwa sifa na vipengele vya kiisimu. Kuteuliwa kwa vigezo hivi vitatu kulitokana na hali kwamba, utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa vipengele vya lugha huku kasoro zilizojitokeza katika matumizi zikiainishwa na kujadiliwa. Aidha, vigezo vinne vilivyosalia havikutumiwa kwa kuwa matumizi yake hujikita katika matini za kifasihi pekee. Vigezo hivyo ambavyo havikutumiwa katika utafiti huu ni: umuhimu wa maudhui na kiwango cha ujuzi wa mwandishi; istilahi za mhakiki; heba na sifa za kibinafsi za mwandishi na tajriba ya mwandishi katika maisha. Tumeshughulikia vigezo vitatu tulivyovitumia katika utafiti huu kimoja baada ya kingine katika sehemu inayofuata.

Usomekaji wa kazi. Katika kuchunguza kipengele hiki, mhakiki anapaswa kuzingatia mtindo wa mwandishi hususani anavyoitumia lugha ili kuvyaza muumano wa kazi yake yote. Kigezo hiki kilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa kilituongoza katika kugundua iwapo matini katika GTL imefumwa vizuri ili kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa, swali likiwa, je, lugha ya mwandishi kama kifurushi kimefungwa na kusukwa vizuri kiasi

kuwa kinatosheleza kimaelezo au ni pungufu? Kigezo hiki kilituongoza katika uchanganuzi wetu uliopelekea kuwekwa wazi kwa matumizi yasiyofaa ya vipengele mbalimbali vya lugha katika makala ya GTL. Katika mawasiliano hasa kupitia kwa maandishi, muumano huwa ni matokeo ya matumizi sahihi ya maumbo ya lugha na kuzingatiwa kwa kanuni za lugha husika. Umuhimu wa kigezo hiki ulitanda kote katika uchanganuzi wetu wa kasoro zilizojitokeza katika matini ambazo zilisababisha ukosefu wa muumano katika makala tuliyoyashughulikia.

Lugha ya mwandishi. Ngara (ibid), pia anasema kuwa lugha ya mwandishi ni kigezo kingine muhimu katika kuupima mtindo uliotumika katika uandishi wowote. Katika kigezo hiki, mnato wa lugha na uteuzi wa maneno ndiyo mambo muhimu ya kuzingatiwa. Kwa mujibu wa utafiti wetu, maumbo tuliyoyachanganua kwa kuzingatia kigezo hiki cha lugha ya mnato ni: methali, nahau na tamathali za usemi. Kwa kuwa kigezo hiki kinasisitiza matumizi ya lugha ya mnato, uchanganuzi wetu uliolenga kudhihirisha matumizi yasiyofaa ya maumbo hayo matatu, ulielekezwa katika kugundua kasoro zilizojitokeza. Muktadha wa kimatumizi ndio uliotumiwa katika kuonyesha kuwa maumbo hayo yametumiwa kwa njia yenye upungufu. Kigezo hiki kiliufaa utafiti huu kwa kuwa tulichunguza namna waandishi wa makala katika GTL wanavyotumia lugha katika harakati zao za kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji wa makala hayo.

Kufaa kwa sifa na vipengele vya kiisimu. Mambo yanayosisitizwa na kigezo hiki ni kama vile: uteuzi wa msamiati, mpangilio wa maneno na sauti zilizotumika. Wazo hili linaendelezwa na Barnet na Stubbs (1983), ambao wakishughulikia chimbuko na maana ya mtindo, wanasema kuwa mtindo hurejelea uteuzi wa maneno na mpangilio wake katika sentensi. Wanaendelea kueleza kuwa maneno yanayolenga ndipo na uakifishi sahihi ni kati ya mambo yanayovyaza weledi katika uandishi. Kwa maoni yao, weledi ndio msingi wa mtindo. Kigezo hiki kilituwezesha kutambulisha kasoro zilizojitokeza katika uteuzi wa msamiati na mpangilio wake katika sentensi zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe kupitia kwa GTL. Matumizi yasiyofaa ya msamiati katika makala teule ya GTL, yametambulishwa kwa msingi wa muktadha wa kimatumizi unaohusika.

Nadharia hii inasisitiza kwamba, mwandishi wa matini yoyote anapaswa kuteua maneno ambayo yataweka wazi ujumbe wake kwa kuwa hatakuwa na fursa ya kufafanua alichokusudia kwa hadhira kama inavyotokea katika mazungumzo ya ana kwa ana. Ili kuandika kikamilifu, mwandishi shuruti awe na umilisi wa lugha ambayo anaitumia katika mawasiliano husika. Upungufu wa umilisi katika lugha aliyoichagua mwandishi hupelekea kufungika kwake katika uteuzi wa msamiati, hali ambayo husababisha ufinyu katika

uwasilishaji wa ujumbe anaonuia. Kama anavyosisitiza, Wyrick (1987), uteuzi wa maneno huweza kusababisha tofauti kubwa katika ubora wa uandishi kwa kuwa iwapo neno lisilo sahihi au lililo tata litatumiwa badala ya neno mwafaka, basi ujumbe ulionuiwa hautamfikia mpokeaji. Anaendelea kusema kwamba ni shuruti aliye na ujumbe, kuuwasilisha akitumia maneno yanayofaa ili hadhira lengwa iuelewe kikamilifu. Hiki kilikuwa kigezo muhimu kwa utafiti huu kwani kilitoa mwanga kuhusu viwango mbalimbali vya kiisimu vinavyopaswa kuzingatiwa katika utathmini wa matini. Viwango hivyo ni kama vile msamiati na sarufi. Hivi ni kati ya vipengele ambavyo tulivihakiki katika utafiti huu ambapo makala ya GTL yalichanganuliwa ili kutambua ufaafu na usahihi wao kimatumizi. Kigezo hiki kilituwekea msingi wa kutambulisha makosa yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha kwa kurejelea vipengele hivyo viwili (msamiati na sarufi). Uchunguzi wetu umeegemezwa kwenye kigezo hiki kwa lengo la kufikia uamuzi kuwa kanuni fulani za kisarufi zimekiukwa katika uandishi wa makala ya gazeti husika.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumeonyesha njia za utafiti ambazo zilitumiwa katika kazi hii. Mambo ambayo yameshughulikiwa ni: njia ya utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli ya utafiti, vifaa vya utafiti, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

3.2 Njia za utafiti

Utafiti huu ulitumia njia ya uchanganuzi umbo-maana katika kukusanya data. Wakieleza kuhusu uchanganuzi-matini, Walizer na Weiner (1978), wanasema kuwa huu ni mfumo uliobuniwa ili kuchunguza kwa utaratibu ujumbe uliorekodiwa. Njia hii iliteuliwa na kutumiwa katika utafiti huu kutokana na ufaafu wake katika kutimiza lengo kuu la kazi hii, hasa ikikumbukwa kuwa tulijikita katika matini iliyorekodiwa kimaandishi. Kupitia kwa usomaji makini wa makala ya *Taifa Leo* yaliyoteuliwa, mtafiti aliweza kutathmini vipengele mbalimbali vya lugha vilivyonuiwa kuchunguzwa mathalan Sarufi, Msamiati, Methali, Nahau na Tamathali za Usemi.

3.3 Mahali pa utafiti

Ukusanyaji wa data ya utafiti huu kuhusu matumizi ya lugha katika magazeti ya Kiswahili nchini Kenya, ulifanyiwa maktabani. Mahali hapa paliteuliwa kutokana na imani kuwa data iliyotarajiwa kukusanywa ingepatikana humo na hivyo kutimiza lengo la utafiti. Mtafiti alisoma matini inayoshughulikiwa, vitabu, tasnifu na majarida mbalimbali ambayo yalitoa mwanga kuhusu namna ya kuchanganua vipengele anuwai vya lugha. Utafiti huu ulifanywa katika maktaba za Vyuo Vikuu vya Egerton, Kenyatta, Nairobi na kile cha Mashariki mwa Afrika, Baraton. Vyuo Vikuu hivi vilichaguliwa kwa misingi kwamba ni miongoni mwa vingine ambavyo vinafundisha taaluma ya lugha na isimu nchini Kenya. Aidha, vyuo hivi vilikuwa na matini iliyokidhi haja ya utafiti huu.

3.4 Uteuzi wa sampuli

Katika utafiti huu, uteuzi wa sampuli ulikuwa muhimu sana kwa kuwa idadi ya nakala za GTL ambazo zimechapishwa tangu kuanzishwa kwa gazeti hilo ni nyingi sana na hivyo mtafiti hakuwa na uwezo wa kuzichanganua zote kutokana na uhaba wa wakati. Uteuzi wa sampuli ulifanywa katika hatua tatu. Kwanza, mtafiti alitumia mtindo wa sampuli

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

azimiwa katika kuchagua ni magazeti ya miaka ipi yatakayohusishwa. Jumla ya miaka mitano ya hivi majuzi (1999-2003), ilihusishwa ili kutambua matumizi ya lugha katika *Taifa Leo* katika kipindi hicho. Kipindi hiki kilichaguliwa kutokana na imani kwamba magazeti yaliyochapishwa katika miaka hiyo, yataonyesha hali ya matumizi ya lugha ilivyo kwa wakati huu. Tumeuzingatia ukweli kwamba lugha hukumbwa na mabadiliko kiwakati ili kutosheleza haja iliyopo ya kimawasiliano. Aidha, kipindi cha miaka mitano kilichaguliwa kwa matarajio kuwa, kipindi cha urefu huo kitapelekea kudhihirika kwa ruwaza katika matumizi ya lugha ili kutuwezesha kutoa rai zenye mashiko. Katika hatua ya pili, mtafiti aligawa kila mwaka unaohusishwa katika jozi za miezi kulingana na mfuatano wake. Hatimaye, mtafiti alitumia mtindo wa sampuli shelabela katika kuteua nakala moja ya GTL kwa kila jozi husika. Idadi kamili ya sampuli ambayo iliteuliwa kwa uchanganuzi ni nakala thelathini kutokana na jumla ya zile zilizochapishwa katika kipindi kilichotajwa (1999-2003).

3.5 Vifaa vya utafiti

Utafiti huu ulitumia nakala za gazeti la *Taifa Leo* ambazo ndizo chanzo cha data iliyokusudiwa kukusanywa. Vitabu mbalimbali vinavyofafanua vipengele vya lugha ambavyo vilichanganuliwa kwa mujibu wa *Taifa Leo*, vilitumiwa. Hivi ni vitabu ambavyo vilielekeza kuhusu matumizi sahihi ya maumbo ya lugha yaliyochanganuliwa. Maoni ya wataalamu wa lugha ambayo yalijitokeza katika vitabu husika yalitumiwa katika kutathmini na kugundua kasoro katika vipengele vya lugha vilivyochunguzwa. Aidha, orodha kipimio ilitumiwa ili kuratibu vipengele vya lugha vilivyochunguzwa kama hatua ya kutambua umara-tokezi wa makosa mbalimbali yaliyojitokeza katika matini husika. Orodha ifuatayo ilitumiwa katika kutambua umara-tokezi wa makosa yaliyochunguzwa katika utafiti huu:

(a). **Sarufi**

(i). Mnyambuliko wa maneno.
(ii). Matumizi ya viambishi.
(iii). Upatanisho wa kisarufi katika sentensi.
(iv). Mpangilio wa maneno katika sentensi.
(v). Matumizi ya vihusishi.
(vi). Tahajia.
(vii). Matumizi ya viunganishi.
(viii). Ukamilifu wa sentensi
(ix). Matumizi ya herufi kubwa na ndogo.
(x). Uakifishi.

(xi). Matumizi ya vivumishi.

(xii). Matumizi ya vielezi.

(b). **Msamiati**

(i). Uteuzi wa maneno.

(ii). Maneno yaliyotoholewa.

(iii). Matumizi ya maneno ya jozi bainifu.

(c). **Methali na Nahau**

Methali

(i). Matumizi ya methali kimuktadha.

(ii). Matumizi ya umbo/maneno asilia ya methali.

(iii). Urundikaji wa methali.

Nahau

(i). Matumizi ya nahau kimuktadha.

(ii). Matumizi ya umbo/maneno asilia ya nahau.

(d). **Tamathali za Usemi**

(i). Matumizi ya tamathali za usemi kimuktadha.

(ii). Urundukaji wa tamathali za usemi.

3.6 Ukusanyaji wa data

Data ya utafiti huu ilijikita katika makala zilizoteuliwa kutokana na jumla ya zile ambazo zinachapishwa katika gazeti la *Taifa Leo*. Makala zilizohusishwa katika uchanganuzi ni habari kuu, tahariri na maoni, na hadithi. Data iliyolengwa ilijumuisha neno (katika kiwango cha chini), kishazi na kirai (katika kiwango cha kati), na sentensi (katika kiwango cha juu). Mtafiti alipitia nakala mbalimbali za gazeti husika huku akizingatia matumizi yasiyofaa ya maumbo ya lugha yaliyonuiwa kuzamiwa. Kutokana na usomaji wa kindani wa makala husika, tulitambulisha namna vipengele anuwai vya lugha vimetumiwa isivyostahiki. Kasoro zilizojitokeza ziliainishwa kwa misingi ya kanuni zinazokubalika katika lugha sanifu ya Kiswahili. Aidha matumizi ya vipengele vingine kama vile methali, nahau na tamathali za usemi, vilichunguzwa kwa kurejelea miktadha ya kimatumizi na ukubalifu wake kulingana na maoni ya wataalamu wa lugha.

3.7 Uchanganuzi wa data

Data ambayo ilikusanywa kutokana na upekuzi wa nakala za gazeti husika, ilichanganuliwa kwa kiasi kikubwa kwa kuzingatia uchanganuzi wa kithamano. Hali hii imetokana na msingi kwamba utafiti huu ni wa kithamano. Wakielezea kuhusu utafiti wa aina hii, Mugenda na Mugenda (1999), wanasema kuwa katika utafiti wa kithamano, data huweza kuwa matini au picha ambazo huelezea matukio. Uchunguzi wetu ulijikita katika matini ambapo tulidondoa makosa katika maumbo mbalimbali ya lugha tukirejelea makala ambayo yanachapishwa katika GTL.

Mugenda na Mugenda (ibid), wanaendelea kueleza kwamba mara nyingi katika utafiti wa kithamano, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake, hufanywa kwa mwambatano wa moja kwa moja. Kwa kutilia maanani wazo hili, tulipanga data iliyokusanywa katika viwango mbalimbali tukiongozwa na madhumuni ya utafiti. Katika uchunguzi wetu tuliibuka na viwango vinne, mathalan sarufi, msamiati, methali na nahau, na tamathali za usemi.

Kama hatua ya kuchunguza kasoro ambazo zinajitokeza katika matumizi ya lugha kwa kurejelea viwango vilivyotajwa hapo juu, tulitambulisha mawazo makuu kwa kila kiwango ambayo yalirahisisha jukumu la kuziainisha kasoro husika. Tulidondoa mifano ya makosa yaliyojitokeza katika matini tuliyoizamia na kuonyesha namna ambavyo maumbo hayo pungufu yanavyoweza kurekebishwa ili kutimiza kiwango cha usahihi kwa mujibu wa Kiswahili sanifu. Aidha, maelezo yametolewa ili kufafanua matokeo kuhusu vipengele vyote vilivyohusishwa katika utafiti huu.

Ingawa huu ni utafiti wa kithamano, mbinu za uchanganuzi wa kiwingidadi zilihusishwa kwa kiasi kidogo ili kuweka wazi zaidi matokeo yaliyoibuka. Majedwali na grafu kwa pau vilitumiwa kuonyesha usambao wa umara-tokezi wa makosa ambayo yanamulikwa katika kazi hii. Mtafiti aliorodhesha idadi kamili ya makosa yaliyogunduliwa katika kila kipengele na kuonyesha asilimia yake yanapolinganishwa na yale ambayo yamejitokeza katika vipengele vingine katika kiwango hicho hicho. Kwa kuwa data iliyokusanywa ilikuwa na vipengele vingi, utaratibu wa tarakilishi wa SPSS ulitumiwa ili kugundua umara-tokezi wa makosa na asili mia zao.

SURA YA NNE

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA GAZETI LA TAIFA LEO

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumejikita katika matumizi ya lugha kama yanavyodhihirika katika gazeti la *Taifa Leo.* Tumeonyesha viwango vya lugha tulivyovichunguza katika kazi yetu mathalani sarufi, msamiati, methali, nahau na tamathali za usemi. Makosa yaliyojitokeza katika vipengele hivyo vya lugha vilivyoshughulikiwa, yameainishwa na kujadiliwa huku mifano ikitolewa kutokana na matini iliyochanganuliwa kwa lengo la kuthibitisha matokeo ya utafiti.

Fauka ya kudondoa makosa yaliyogunduliwa katika matini husika, tumetoa marekebisho ambayo yamelenga kuelekeza matumizi yafaayo ya maumbo yaliyochanganuliwa. Utafiti huu umetumia ama kanuni za lugha sanifu ya Kiswahili au matumizi kimuktadha ili kufikia uamuzi kuhusu matumizi yanayostahiki ya lugha na kinyume chake.

Kama njia ya kuonyesha umara-tokezi wa makosa yaliyoshughulikiwa, tumetumia, majedwali na grafu ambazo zimeweka wazi ujumbe huo. Maelezo zaidi kuhusu matumizi haya ya majedwali na grafu yametolewa katika sura ya tatu (sehemu 3.7) ambayo imeshughulikia mbinu za utafiti. Ili kuwasilisha matokeo yetu kwa mtindo ambao tunaamini umeweka bayana zaidi ugunduzi wetu, tumeshughulikia kiwango kimoja baada ya kingine hapa chini.

4.2 Sarufi

Harris na Chomsky (katika Tumbo-Masabo and Kiango, 1990), wanasema kuwa sarufi ni mkusanyiko wa sheria maalum ambazo humwezesha mtumiaji wa lugha kuzalisha idadi ya tungo zisizo na kikomo katika lugha yoyote ile. Msisitizo wa wataalam hawa kuhusu kuwepo kwa sheria maalum katika lugha mbalimbali, ndio umekuwa mwongozo wetu katika kuonyesha ni kasoro zipi zinazojitokeza katika matini tuliyoichanganua. Makosa muhimu tuliyogundua katika kipengele hiki, tumeyaainisha katika sehemu ifuatayo.

4.2.1 Matumizi ya sentensi zisizokamilika

Sentensi iliyokamilika shuruti iwe na kiima na kitenzi kikuu (Robey na wenziwe, 1984; Wyrick, 1987). Katika uchunguzi huu, tumegundua kuwa kasoro nyingi zilizojitokeza

katika kiwango cha sentensi zilisababishwa na kutokamilika kwake, hali iliyopelekea kutoeleweka kwa ujumbe ulionuiwa kuwasilishwa. Kutokamilika kwa sentensi katika makala tuliyochanganua kumetokana na mambo mbalimbali kama yanavyobainishwa hapa chini.

4.2.1.1 Matumizi ya tungo tegemezi

Tungo tegemezi, kwa mujibu wa Mekacha (1987), ni sentensi iliyoshushwa hadhi na kutegemezwa katika sentensi nyingine. Anaendelea kusisitiza kuwa tungo ya aina hii haitokei peke yake bali hutokea kama sehemu ya sentensi, na kimuundo,tungo tegemezi huwa kiambajengo cha sentensi kuu. Naye Nkwera (1978), anaeleza kuwa, tungo tegemezi ni kifungu cha maneno chenye kiima na kiarifu, lakini maana yake siyo kamili. Anaongezea kuwa, hiyo ni tungo inayotawaliwa na tungo nyingine, yaani tungo sahili, kwa vile imekuwa ama moja ya vipashio vyake au sehemu ya kipashio cha hiyo tungo sahili. Mawazo haya, yanaonyesha wazi kuwa iwapo tungo tegemezi itatokea peke yake, basi ujumbe uliotarajiwa kumfikia msomaji wa matini, hautamfikia. Kwa kuzingatia kitengo hiki, baadhi ya sentensi ambazo hazikukamilika katika makala yachapishwayo katika GTL ni pamoja na:

1a.* Katika hekalu hiyo ya Albert Pike, kinara wa shirika hilo ambaye anasemekana alidai kwamba shetani ni Mungu.[1]

2a.* Sehemu ambako kuna vijana wenye vipawa vya kucheza kandanda lakini hawawezi kuvikuza kwa sababu wamekosa viwanja.[2]

3a.* Kuna watu wengi wanapopewa mamlaka wakaona kama wao ndio miungu.[3]

Kutokana na mifano hii ya sentensi zisizokamilika, ni bayana kuwa ukamilifu wa sentensi katika lugha yoyote ile haupimwi kutokana na idadi ya maneno yaliyotumiwa katika utunzi wake bali uwepo wa sehemu muhimu ambazo huchangia upashaji wa habari kamili. Tukichungua tungo hizo tatu, tunaona kuwa utegemezi wao unasababishwa na mambo mbalimbali. Tungo (1a) na (2a), ni tegemezi kutokana na matumizi ya viwakilishi vya kurejesha **amba-** yanavyotokea katika maneno **ambaye** na **ambako,** kwa mfuatano huo. Kwa upande mwingine, utegemezi wa tungo (3a), umetokana na matumizi ya kitenzi**, wakaona.** Matumizi ya neno hili (wakaona) linaifanya kauli hii ining'inie kufuatia matumizi ya kiambishi **-ka-** ambacho huashiria mfuatano wa matukio mbalimbali. Ili sentensi hiyo kuwa kamilifu, kitenzi **wakaona** kinapaswa kubadilishwa kwa lengo la kurejelea wakati maalum au hali ya mazoea. Sentensi kama hizi zinaweza kurekebishwa ama kwa kuziongezea tungo huru au kwa kuziunganisha na tungo zilizokurubiana kimfuatano (Barnet na Stubbs, 1983).

Muktadha ni mtikati katika kuandika sentensi za aina hii kwa usahihi unaokubalika katika Kiswahili sanifu. Sentensi kamilifu zitakuwa:

1b. Katika hekalu hiyo ya Albert Pike, kinara wa shirika hilo alisemekana alidai kwamba shetani ni Mungu.

2b. Sehemu hiyo ina vijana wenye vipawa vya kucheza kandanda lakini hawawezi kuvikuza kwa sababu wamekosa viwanja.

3b. Kuna watu wengi wanapopewa mamlaka, hujiona kama wao ndio miungu.

4.2.1.2 Sentensi zilizokosa viunganishi

Kiungansihi ni umbo linalochukua nafasi kubwa katika kuvyaza sentensi kamili katika mawasiliano. Kulingana na Masoko (1990), viunganishi huunga neno na neno; virai na vishazi au sentensi kadhaa. Kwa kuzingatia ufafanuzi huu, utafiti wetu umejihusisha na ukosefu wa viunganishi kati ya maneno, virai na vishazi kama kasoro inayosababisha kutokamilika kwa sentensi. Tumegundua kuwa, kuna makosa yanayotokana na hali hii katika matini tuliyochunguza inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

4a.* ... ufisadi pamoja ukosefu wa makini ....[4]

5a.* ... hawana imani kabisa vikosi vyetu ....[5]

6a.* ... kutambua wachezaji bora kuimarisha timu za kitaifa ....[6]

Ukamilifu wa sentensi hizi tatu (4a,5a,6a), unategemea kujalizwa kwa viunganishi vifaavyo. Katika mifano (4a,5a), kiunganishi **na** kilipaswa kutumiwa ili kuvyaza sentensi kamilifu. Aidha, katika mfano (6a), kiunganishi **ili** ndicho kilihitajika ili kuziba pengo ambalo lilipelekea sentensi hiyo kutokamilika. Sentensi sahihi zitakuwa:

4a. ... ufisadi pamoja na ukosefu wa makini ....

5a. ... hawana imani kabisa na vikosi vyetu ....

6a. ... kutambua wachezaji bora ili kuimarisha timu za kitaifa ....

Maneno yaliyopigiwa mistari ndiyo yanayotekeleza jukumu la kuunganisha mawazo katika sentensi husika na hivyo kuzifanya zikamilike. Ni muhimu kusisitiza katika kiwango hiki kwamba, sentensi nyingi zilizokosa ukamilifu kutokana na kutotumiwa kwa viunganishi. Hivyo basi, waandishi wanapaswa kumakinika zaidi katika matumizi ya viunganishi ili kuzalisha tungo zinazokubalika kisarufi.

4.2.1.3 Matumizi mabaya ya vihusishi

Vihusishi hutekeleza jukumu muhimu la kuonyesha uhusiano uliopo kati ya maneno, virai na vishazi katika sentensi. Wataalamu wa lugha ya Kiswahili kama vile Mdee (1988), na

Mkude (1987), wamesisitiza kuwa vihusishi huonyesha uhusiano baina ya neno na neno tu na aghalabu baina ya majina au kikundi jina. Wanakubaliana kwamba ingawa vihusishi vina ukuruba mkubwa na viunganishi, maumbo hayo mawili huwa na nafasi tofauti katika sentensi. Matokeo ya ukosefu wa vihusishi pale vinapohitajika, ni kuwa na sentensi iliyo na mawazo yaliyoning'inia kama inavyojitokeza katika tungo zifuatazo:

7a.* Mchango wa mishahara chini katika idara hiyo....[7]

8a.* Ni jambo lisilo la maana watu kuingilia ....[8]

9a.* ... kiongozi Rasmi upinzani Bungeni alilengwa shutuma kali na mawaziri....[9]

Kutokana na sentensi hizi zenye kasoro, tunaweza kuzisahihisha ili ziwe kamilifu kwa kutumia vihusishi pale vinapohitajika. Sentensi zilizorekebishwa zitakuwa:

7b. Mchango wa mishahara ya chini katika idara hiyo....

8b. Ni jambo lisilo la maana kwa watu kuingilia....

9b. ...kiongozi Rasmi wa upinzani Bungeni alilengwa kwa shutuma kali na mawaziri....

Vihusishi vilivyokosa katika mifano mitatu ya awali (7a,8a,9a), vimepigiwa mistari katika tungo zilizosahihishwa (7b,8b,9b). Ingawa kipengele hiki kinajumuisha maneno ya kawaida kabisa katika lugha ya Kiswahili, ni muhimu ikumbukwe kuwa kutokuwepo kwake katika utungo wowote ule, huilemaza sentensi husika kiasi kwamba ujumbe unaowasilishwa unatatizwa.

4.2.1.4 Kuachwa kwa (ma)neno katika sentensi

Sentensi kamilifu huundwa kwa maneno mbalimbali ambayo huchangia katika upashaji wa ujumbe. Endapo neno moja au zaidi yatakosa katika tungo fulani, basi hutokea pengo linalopelekea habari kutoeleweka. Utafiti wetu ulikumbana na hali kama hiyo ambapo baadhi ya sentensi zilipungukiwa kwa neno moja huku zingine zikidhihirisha kuachwa kwa zaidi ya neno moja. Mifano ifuatayo inabainisha kasoro hiyo.

10a. * ...itawaokoa wananchi wengi, hasa wenye watoto wengi, maskini na mapato ya chini ....[10]

11a. * ... kuungwa mkono kwa dhati na wapenzi wa misuli....[11]

12a. * Rais Kibaki wabunge wataruhusiwa tu kuwa wadhamini....[12]

Sentensi hizi zinaweza kurekebishwa kwa kutambua sehemu ambazo zinahitaji kujalizwa kwa neno au maneno ili kuleta maana iliyokusudiwa. Yafuatayo ni masahihisho ya tungo hizo.

10b. ...itawaokoa wananchi wengi, hasa wenye watoto wengi, maskini na wenye mapato ya chini....

11b. ...kuungwa mkono kwa dhati na wapenzi wa mchezo wa kujenga misuli.

12b. Rais Kibaki alisema kuwa wabunge wataruhusiwa tu kuwa wadhamini ....

Katika mifano hiyo ya sentensi zilizosahihishwa, maneno yaliyopigiwa mistari yana umuhimu mkubwa katika kuvyaza tungo kamilifu. Tukichukua sentensi (12a), na kuichunguza kwa kina, tunagundua kwamba kutokuwepo kwa maneno **alisema kuwa**, kunainyima sentensi hiyo sehemu ambayo ni muhimu katika kuzalisha muumano. Matokeo ya hali hii ni kutoeleweka kwa ujumbe unaokusudiwa na mtumaji.

(Kwa mifano zaidi ya sentensi zisizokamilika, rejelea kiambatisho C na D).

Fauka ya kuzamia kasoro mbalimbali zilizosababisha kutokamilika kwa sentensi katika makala tuliyochunguza, utafiti huu ulijihusisha na umara-tokezi wa aina za makosa zilizogunduliwa. Matokeo ya umara-tokezi huo yamewekwa wazi katika jedwali nambari 1.

Jedwali 1: Makosa yaliyopelekea sentensi kutokamilika

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Matumizi ya tungo tegemezi pekee	25	18
Sentensi zilizokosa viunganishi	18	13
Kutotumiwa kwa vihushishi inavyostahiki	56	40
Kuachwa kwa (ma)neno katika sentensi	41	29
Jumla	140	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Matokeo katika jedwali nambari 1, yanaonyesha wazi kuwa kosa la kutotumiwa kwa vihusishi inavyofaa, ndilo lililosababisha idadi kubwa ya sentensi kutokamilika. Takwimu zinaonyesha kuwa kipengele hicho kilipelekea sentensi asili mia arobaini (40%), kuwa na upungufu miongoni mwa zile zilizotambuliwa kuwa si kamilifu. Aina hii ya kasoro ilijitokeza kutokana na waandishi wa makala husika kukosa kutumia vihusishi katika baadhi ya tungo zao na hivyo kuacha pengo ambalo lilipaswa kuzibwa. Aidha, utafiti huu uligundua kuwa mazoea ya kuacha neno au maneno katika sentensi, yalichangia kutokamilika kwa asili mia ishirini na tisa (29%) ya sentensi. Vipengele ambavyo vilifanya idadi ndogo ya sentensi

kutokuwa kamilifu, ni kile cha matumizi ya tungo tegemezi pekee, asili mia kumi na nane(18%) na sentensi zilizokosa viunganishi, asili mia kumi na tatu (13%).

4.2.2 Ukosefu wa upatanisho wa kisarufi

Upatanisho wa kisarufi ni sifa muhimu inayotumiwa kama kigezo cha kutathmini kufaulu kwa sentensi katika kuwasilisha habari inayokusudiwa. Upatanisho wa kisarufi (au utawala mlinganifu wa maneno ya fungu moja), ni jambo linalopatikana katika lugha zote, (Kapinga, 1983). Katika juhudi za kuelezea sifa mbalimbali za sentensi za Kiswahili, Massamba na wenziwe (1999), wanasema kuwa sentensi husika, zina hali ya Kirai-Nomino kudhibiti Virai-Vitenzi na Virai-Vivumishi kupitia kwa njia ya viambishi. Wanasisitiza kwamba, katika kila sentensi, nomino hudhibiti kila kivumishi na kila kitenzi kupitia kwa kiambishi chake. Udhibiti huo ndio ambao, wataalam hawa wanautaja kama upatanisho wa kisarufi. Kwa mujibu wa Ashton (1989), upatanisho hutumiwa kuhusisha majina na maneno mengine katika sentensi kwa kuzingatia makundi mbalimbali ambamo maneno hayo yametolewa (tafsiri yetu). Ashton anatambulisha upatanisho wa aina mbili: kwanza, upatanisho wa viwakilishi na pili, ule wa vivumishi. Anasisitiza kwamba viwakilishi huambishwa katika mianzo ya mizizi ya vitenzi ilhali upatanisho wa vivumishi hudhihirika kupitia kwa viambishi vinavyotokea kabla ya mizizi ya vivumishi na baadhi ya maneno yanayobainisha idadi katika sentensi. Mbali na makundi haya mawili ya upatanisho ambayo yameelezwa na mtaalam huyu, utafiti huu pia umejihusisha na upatanisho wa viambishi virejeshi 'O', kama kipengele kingine ambacho kina nafasi ya kuleta muumano katika sentensi. Makosa yaliyotokea katika matini husika na kusababisha kasoro katika upatanisho wa kisarufi katika tungo mbalimbali yameainishwa na kujadiliwa hapa chini.

4.2.2.1 Matumizi mapungufu ya viwakilishi

Viwakilishi ni viambishi au maneno ambayo hutumiwa kuwakilisha jina katika sentensi. Viwakilishi hutekeleza jukumu la kujulisha kitu kinachohusika na maonyesho, ulizo au kitenzi kinachoarifu tukio fulani, ambapo jina la kitu chenyewe halitajwi (Kapinga, 1983). Katika uchunguzi wetu, tumejikita katika matumizi ya viambishi vinavyowakilisha majina katika matini iliyoshughulikiwa. Ukubaliano kati ya jina na kitenzi katika sentensi na viwakilishi vinavyotumiwa huvyaza ueledi wa maneno yanayowasilishwa (Baker na Dwight, 1981). Wataalamu mbalimbali wa lugha, wamesisitiza juu ya umuhimu wa kuwepo kwa ukubaliano kati ya jina na kiwakilishi chake katika tungo. Kiwakilishi shuruti kiwe na ukubaliano kiidadi na jina linalosimamiwa (Robey na wenziwe, 1984; Wyrick, 1987).

Tuligundua matumizi yasiyofaa ya viwakilishi katika makala yachapishwayo katika GTL kama inayodhihirishwa na mifano ifuatayo.

13a.*... hata kama umoja wa mataifa utawalipa ulimwengu mzima marupurupu....[13]

14a. * Matoleo ambayo walikuwa mengi ....[14]

15a.* Mazoea haya yalizidi kuendelea kwa muda mrefu licha ya jitihada za msichana huyu kuzikomesha ....[15]

Katika sentensi hizi tatu, sehemu zilizopigiwa mistari ndizo zinazorejelea viwakilishi ambavyo vimetumiwa isivyostahiki. Msingi wa ila zinazobainika katika mifano hiyo ni kutozingatiwa kwa ngeli za majina ambayo yametumiwa kuundia tungo husika. Kwa mfano, ingawa neno **ulimwengu** katika sentensi (13a), lina maana ya jumuiya ya watu, ni makosa kutumia kiwakilishi **wa** kurejelea dhana inayozungumziwa. Chanzo cha kosa hili ni kushindwa kwa mwandishi husika kutambua kwamba neno **ulimwengu** ni la ngeli ya **U** na hivyo matumizi ya kiwakilishi **wa** yana dosari. **Wa** ingetumiwa tu ikiwa neno **watu** lingetumiwa katika muktadha huo. Sentensi hizo kisahihi zitakuwa:

13b. ... hata kama Umoja wa Mataifa utaulipa ulimwengu mzima marupurupu....

14b. Matoleo ambayo yalikuwa mengi ....

15b. Mazoea haya yalizidi kuendelea kwa muda mrefu licha ya jitihada za msichana huyu kuyakomesha....

Katika tungo hizi zilizosahihishwa, sehemu zilizopigiwa mistari zinadhihirisha viwakilishi sahihi. Ni muhimu kusisitiza hapa kwamba, baadhi ya makosa katika kipengele hiki, hutokana na kuwekwa kwa neno la urejeleo mbali sana na jina linalorejelewa. Hali hii inathibitishwa na urejeleo katika sentensi (15a), ambapo neno **mazoea** linatumiwa mwanzoni mwa sentensi ilhali neno **kuyakomesha** ambalo linamrejesha msomaji katika neno la kwanza, limetumiwa mwishoni mwa sentensi. Uchanganuzi wa sentensi (14a), umedhihirisha kuwa kiwakilishi **wa** kilichotumiwa katika tungo hiyo hakioani na jina **matoleo** ambalo ndilo linalowakilishwa. Mtunzi huyo ametumia kiwakilishi cha ngeli tofauti (A- WA) mahali pasipofaa badala ya kutumia **ya** ya ngeli (LI- YA), ili sentensi hiyo iwe sahihi.

4.2.2.2 Makosa katika matumizi ya vivumishi

Vivumishi ni maneno ambayo hutumiwa kuelezea na kutoa maana zaidi kuhusu majina (Wyrick, 1987). Kuwepo kwa vivumishi katika sentensi hulenga kutoa maelezo zaidi kuhusu jina husika na hivyo kukamilisha jukumu la uwasilishaji wa habari kwa uwazi zaidi. Hata hivyo iwapo viambishi ambavyo vinatumiwa katika vivumishi husika vitakuwa na

kasoro, basi yaelekea kuwa ujumbe unaonuiwa kupitishwa utaathirika. Wakati mwingine kivumishi kizima chaweza kuwa na kasoro endapo kitatumiwa mahali pasipofaa. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya matumizi hayo yasiyofaa.

16a.* Kila mmoja wa wabunge wetu atangaze msimamo wao wa kisiasa.[16]

17a.* ...tatizo ndogo....[17]

18a.*....hakuna pingamizi wowote....[18]

Mfano unaojitokeza katika sentensi (16a), unabainisha matumizi ya kimilikishi **wao** isivyostahili. Kauli hiyo ilihitaji kimilikishi kiwe katika umbo lake la umoja ili kuwa sahihi. Katika sentensi (17a), kosa linasababishwa na uhamishaji wa neno **tatizo** kutoka kundi lake (LI – YA) hadi kundi lingine (I – ZI) na hivyo kuathiri kivumishi kinachofuata. Hali iyo hiyo inadhihirika katika sentensi (18a), ambapo neno **pingamizi** laelekea kuhamishwa kutoka kundi linalofaa (I - ZI) na kuingizwa katika kundi tofauti (U - I). Sentensi hizo tatu zaweza kurekebishwa na kuandikwa hivi:

16b. ...Kila mmoja wa wabunge wetu atangaze msimamo wake wa kisiasa.

17b. ... tatizo dogo....

18b. ... hakuna pingamizi yoyote ....

4.2.2.3 Matumizi ya viambishi virejeshi 'o' isivyostahiki

Kimsingi, viambishi virejeshi 'O' hutumiwa kulingana na kundi la jina linalorejelewa katika tungo husika. Aidha, ni muhimu kusisitiza kwamba, 'O' rejeshi huambishwa mwishoni mwa umbo **amba** ili kukamilika. Pia huweza kutumiwa katika fungu-tenzi ama kabla ya shina la neno husika au baada yake. Matumizi yake kisahihi ni muhimu katika kuimarisha ueledi wa tungo fulani. Uchunguzi wetu umegundua kuwa, virejeshi 'O' ni kati ya maumbo yaliyotumiwa vibaya katika matini tuliyoshughulikia na hivyo kutinga ukubaliano wa kisarufi. Katika sentensi zingine umbo hilo halikutumiwa ingawa lilifaa kuhusishwa katika baadhi ya maneno . Hali hiyo inajitokeza kupitia kwa mifano ifuatayo.

19a.* Tuna tukio kama hilo, walakini nitawasimulia moja ambayo ni mbaya zaidi.[19]

20a.* ... zana zilizotakikana ... ni zile za kawaida watumiao watunzi ....[20]

21a.*... itakavyotwaa ardhi na majengo zilinyakuliwa....[21]

Sehemu zenye kasoro ndizo zimepigiwa mistari katika sentensi hizo tatu.

Tungo (19a) na (20a), zinaonyesha matumizi ya virejeshi 'O' ambayo hayaambatani na majina yaliyotumiwa. Maneno **tukio** katika sentensi (19a) na **zana** katika sentensi (20a),

ndiyo yanayoelekeza kuhusu umbo la 'O' rejeshi linalohitajika ili kuvyaza tungo sahihi. Hivyo basi, matumizi sahihi ya umbo hilo yatazalisha sentensi hizi:

19b. Tuna tukio kama hilo, walakini nitawasimulia moja ambalo ni baya zaidi.

20b.... zana zilizotakikana... ni zile za kawaida watumiazo watunzi....

21b. ..... itakavyotwaa ardhi na majengo yaliyonyakuliwa....

Inavyobainika, katika tungo (21a), kirejeshi 'O' hakikutumiwa katika neno zilinyakuliwa na hivyo kulazimu kitiwe katika masahihisho ili sentensi hiyo ikubalike katika lugha sanifu ya Kiswahili. Huenda kosa hilo limesababishwa na ujumlishaji uliokithiri kwa mujibu wa Musau (1992). Mtaalam huyu anaeleza kwamba, wakati mwingine watumiaji wa lugha ya Kiswahili hudondosha kirejeshi 'O' mahali kinapohitajika na hivyo kuleta dosari katika sentensi husika. Iwapo mwandishi wa sentensi hiyo alinuia kutumia neno **zilinyakuliwa** lilivyo, basi lingetanguliwa na neno **ambazo** ili kupelekea ukubalifu wake. Marekebisho katika sentensi (19b), ambapo neno **ambalo** limetumika, yanaathiri neno **mbaya** linalofuatia. Neno hilo linadondosha kiambishi **m** na kuchukua umbo **baya** ambalo linaafiki matumizi ya neno **tukio** katika sentensi hiyo.

(Rejelea kiambatisho B, C, na D kwa mifano zaidi ya sentensi zilizokosa upatanisho wa kisarufi).

Kama hatua ya kuonyesha usambao wa umara-tokezi wa aina hizo tatu za makosa tulizozijadili kama vianzo vya ukosefu wa upatanisho wa kisarufi katika tungo mbalimbali, tumetumia jedwali nambari 2, kutimizia lengo hilo.

Jedwali 2: Kasoro zilizosababisha kutokuwa na upatanisho wa kisarufi katika sentensi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Matumizi pungufu ya viwakilishi	36	55
Makosa katika matumizi ya vivumishi	16	25
Matumizi ya virejeshi 'O' isivyostahiki	13	20
Jumla	65	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Kutokana na jedwali hili, inabainika kwamba makosa mengi ambayo yalisababisha sentensi kukosa upatanisho wa kisarufi yalitokana na matumizi pungufu ya viwakilishi. Kipengele hiki kilichangia asili mia hamsini na tano (55%) ya jumla ya makosa yaliyotokea katika kiwango cha upatanisho wa kisarufi. Vipengele viwili vilivyobaki vilichangia idadi ndogo ya makosa ambapo kile cha makosa katika matumizi ya vivumishi kilikuwa na

asilimia ishirini na tano (25%), ilhali matumizi ya virejeshi 'O' isivyostahiki kikiwa na asili mia ishirini (20%). Matokeo haya yanaonyesha kuwa viwakilishi ni mtikati katika utunzi wa sentensi za Kiswahili. Hivyo basi, kipengele hiki kinafaa kusisitizwa ili kuibuka na sentensi sahihi na ambazo zitarahisisha uwasilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, hatuna nia ya kuelekeza kuwa vipengele hivyo vingine ambavyo vinatia doa upatanisho wa kisarufi, vipuuzwe – kila kimojawapo chapaswa kutiliwa maanani ili kuvyaza sentensi sahihi.

4.2.3 Makosa katika mnyambuliko wa maneno

Unyambuaji ni hatua ya kuongeza viambishi mbalimbali katika neno ili kuleta maana tofauti tofauti kutokana na neno hilo moja husika. Anavyosema Nkwera (1978), mnyambuliko ni uwezo wa kufungiliwa silabi mahsusi mwanzoni au mwishoni mwa mzizi au shina la neno kwa lengo la kutanua maana ya neno hilo na kujenga mashina mapya na mizizi mipya. Anaongezea kuwa, mnyambuliko unahusisha viambishi vya namna mbili: (a) viambishi-maana ambavyo hutokea mwanzoni, kati au mwishoni mwa shina la neno. Viambishi hivi hutanua maana bila kubadilisha shina au mzizi wa neno; (b) viambishi-vijenzi ambavyo hutokea hasa mwishoni mwa shina la neno. Hivi vina kazi tatu: kutanua maana ya neno; kujenga mzizi au shina la mnyambuliko; huweza pia kubadilisha neno toka aina moja likaingia katika aina nyingine ya neno. Juhudi za unyambuaji zina umuhimu wa kipekee katika lugha yoyote ile kwani huvyaza iktisadi ambapo neno moja huweza kutumiwa kurejelea mambo kadha wa kadha kulingana na mnyambuliko unaotekelezwa. Lugha ya Kiswahili imedhihirisha ukwasi mkubwa katika kipengele hiki. Mnyambuliko wa maneno, ni hazina maridhawa kwa lugha iwapo utafanywa kwa kuzingatia misingi iliyowekwa katika lugha husika. Katika utafiti wetu, tumekumbana na unyambuaji wa maneno usiofaa katika baadhi ya makala ya GTL tuliyoyachanganua. Makosa yaliyojitokeza yanaweza kuainishwa na kujadiliwa ifuatavyo:

4.2.3.1 Unyambuaji usiofaa wa maneno

Katika kiwango hiki kasoro zilizojitokeza zinaweza kuwekwa katika makundi mawili. Tumeyajadili makundi hayo hapa chini.

4.2.3.1.1 Unyambuaji wa maneno kimakosa

Baadhi ya maneno ambayo kwa kawaida yanaruhusu mnyambuliko, yamenyambuliwa vibaya katika matini tuliyochunguza. Mifano inayofuata inadhihirisha hali hiyo.

22a.* ... lakini hakuna lolote <u>wanalofanyia</u> kuthibitisha madai hayo.... [22]

23a.* ... mgomo wa walimu kusimamizwa....[23]

24a.*... kiasi kusumbuliwa na kuangamia na pia kudidimika kwa huduma....[24]

Tukizingatia muktadha wa kimatumizi, tunang'amua kwamba mnyambuliko wa vitenzi katika tungo (22a) na (24a), umepotosha. Kwa upande mwingine, unyambuaji katika tungo (23a), siyo sahihi kutokana na ukiukaji wa kanuni za kunyambua neno **simama** ambapo kiambishi **sha** hutumiwa kuonyesha hali ya kutendesha na hivyo **shwa** kwa kutendeshwa. Sentensi hizo zinaweza kusahihishwa ifuatavyo.

22b... lakini hakuna lolote wanalofanya kuthibitisha madai hayo....

23b... mgomo wa walimu kusimamishwa....

24b... kiasi kusumbuliwa na kuangamia na pia kudidimia kwa huduma....

4.2.3.1.2 Maneno yasiyostahili, kunyambuliwa

Kuna maneno katika lugha ya Kiswahili ambayo hayapaswi kunyambuliwa. Mengi ya maneno hayo yaweza kuwa aina ya vivumishi, majina au vitenzi vyenye ukuruba mkubwa na majina yaliyovizaa. Aidha, kuna maneno mengine ambayo ingawa yanaweza kunyambuliwa, yatumikapo katika miktadha fulani hayaruhusu mnyambuliko. Uchunguzi wetu umetambulisha makosa yanayotokana na hali hizo katika mifano ifuatayo:

25a.* Limefadhilisha miradi....[25]

26a.*... alijizatitisha kwa kilimo....[26]

27a.*... walipotisha kuwashambulia kwa kuwashukia kwamba walitoka ....[27]

Maneno yaliyopigiwa mistari katika (25a) na (26a), yamenyambuliwa ingawa kisahihi yanatakiwa kutumiwa katika maumbo yao asilia hasa tunaporejelea muktadha wa kimatumizi unaohusika. Kitenzi **fadhili** katika mfano (25a), kingeruhusu mnyambuliko unaojitokeza iwapo neno lililoko katika nafasi ya shamirisho lingekuwa linarejelea binadamu. Hivyo basi, unyambuaji wa neno hilo unaitia dosari sentensi hiyo ambamo limetumiwa. Katika mfano (26a), ingawa neno **zatiti** linaweza kunyambuliwa ili kuzalisha maumbo yenye maana mbalimbali, mnyambuliko uliofanyiwa neno hilo unazua utata hasa ikizingatiwa kuwa kiambishi **sha** kinaonyesha hali ya kutendesha. Hali hii ni kinyume cha ukweli unaodhihirika katika tungo hiyo kwani mrejelewa ndiye aliyejitahidi katika shughuli (kilimo) inayozungumziwa. Aidha, katika mifano (27a), neno **shuku** limenyambuliwa kimakosa kwani mazingira ambamo limetumika hayaruhusu mnyambuliko huo. Sentensi husika imekuwa pungufu kutokana na unyambuaji wa neno hilo na hivyo kukosa kuwasilisha

ujumbe unaokusudiwa. Neno hilo lilipaswa kuachwa katika hali inayoonyesha kutenda ili sentensi hiyo iwe sahihi. Hivi ndivyo tunavyoweza kuzirekebisha kauli hizo:

25b. Limefadhili miradi....

26b. ...alijizatiti kwa kilimo....

27b. ... walipotisha kuwashambulia kwa kuwashuku kwamba walitoka....

4.2.3.2 Maneno yanayostahili, kutonyambuliwa

Makala mengine yalidhihirisha kasoro ambapo maneno ambayo yalipaswa kunyambuliwa yaliachwa katika maumbo yao asilia. Huenda makosa ya jinsi hii, yalisababishwa na waandishi husika kutozingatia muktadha ambamo vitenzi hivyo vimetumiwa. Miongoni mwa sentensi ambazo zilikuwa na upungufu huo ni hizi zifuatazo:

28a.*... lilitetemeshwa jana na gesi ya kutoa machozi.... [28]

29a.* ... wadhifa huo alioushika kwa mwaka....[29]

30a.* ... watu walipe maji....[30]

Vitenzi vilivyopigiwa mstari katika mifano hiyo mitatu, vilihitaji kunyambuliwa ili kupitisha ujumbe kifasaha. Kutokana na kutovinyambua vitenzi hivyo katika kauli (28a) na (30a), maana iliyonuiwa haijitokezi kwani sentensi hizo zinakuwa tata. Kwa mfano, katika kauli (28a), inaweza kuchukuliwa kimakosa kuwa **gesi** ndiyo iliyotoa machozi badala ya maana inayokusudiwa kwamba **gesi** iliwafanya waliotupiwa kutokwa na machozi. Tungo hizo zinaweza kusahihishwa kwa kunyambua vitenzi husika kwa kutilia maanani muktadha wa kimatumizi inavyobainika hapa chini.

28b... lilitetemeshwa jana na gesi ya kutoza machozi....

29b... wadhifa huo alioushikilia kwa mwaka ....

30b... watu walipie maji....

(Kwa mifano zaidi ya minyambuliko isiyofaa ya maneno, rejelea kiambatisho B).

Kwa kutumia jedwali nambari 3 linalofuata, tumeonyesha namna kasoro tulizozishughulikia katika sehemu hii zinavyojitokeza kiidadi katika matini iliyochunguzwa. Jedwali hili linaweka wazi, ni lipi kati ya makundi makuu mawili tuliyojihusisha nayo, lilikuwa na makosa mengi na kinyume chake.

Jedwali 3: Kasoro katika unyambuaji wa maneno

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Unyambuaji usiofaa wa maneno	40	70
Maneno yanayostahili, kutonyambuliwa	17	30
Jumla	57	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa makosa yaliyotokana na unyambuaji usiofaa wa vitenzi yalikuwa mengi kwani kipengele hicho kilichangia asili mia sabini (70%), ya makosa yote yaliyohusu mnyambuliko wa vitenzi. Ili kuepuka makosa kama haya katika uandishi, wahusika wanahitaji kumaizi kanuni zinazoongoza mnyambuliko wa vitenzi mbalimbali. Aidha, makini yahitajika katika kutambua mahitaji ya miktadha tofauti ya kimatumizi kwa nia ya kujimudu katika unyambuaji wa maneno anuwai. Pia matokeo katika jedwali nambari 3, yanaonyesha kuwa ni kasoro chache zilizotokana na vitenzi vinavyostahili, kutonyambuliwa. Sehemu hii ilikuwa na makosa yaliyofikia asili mia thelathini (30%).

4.2.4 Upungufu katika mpangilio wa maneno katika sentensi.

Mpangilio wa maneno huchukua nafasi muhimu katika utunzi wa sentensi. Mpangilio wa maneno katika sentensi unaonyesha utaratibu wa maneno yanavyowiana kisarufi (Kapinga, 1983). Lugha mbalimbali huwa na kanuni ambazo huongoza mtunzi juu ya namna ya kupanga maneno ili kuzalisha tungo sahihi. Akieleza kuhusu jambo hili, Mbaabu (1985:78), anasema:

> "...*Lugha zote ulimwenguni huwa na sehemu tatu muhimu za sentensi. Sehemu hizo ni kiima, kitendo na mtendewa. Sehemu hizi tatu, huwa zimepangwa kutegemea taratibu na sheria za sarufi ya lugha husika. Sentensi nyingi za Kiswahili hufuata mpangilio wa: kiima – kitendo – mtendewa...*."

Maelezo haya hasa kuhusu mpangilio wa maneno ufaao katika Kiswahili, yamesisitizwa na wataalam wengine wa lugha ya Kiswahili kama vile Sewangi (1997) na Kapinga (1983), ambao wanasema kuwa muundo wa msingi wa sentensi ya Kiswahili ni kiima mwanzo, kitenzi na shamirisho mwisho. Hivyo basi, ni bayana kuwa, ili kutunga sentensi zinazokubalika katika Kiswahili, mtunzi shuruti azingatie kanuni zilizowekwa. Ili kuvyaza ueledi, mfumo sahihi wa kupanga maneno katika tungo ni muhimu sana (Wyrick, 1987). Ingawa, mageuko katika mpangilio wa maneno hayabadilishi maana inayowasilishwa, wakati

mwingine huenda maana ikaathiriwa kutokana na aina ya maneno ambayo yanabadilishana nafasi. Kwa mfano, kwa mujibu wa Wales (1987), uamilifu wa jina na shamirisho mara nyingi hutegemea nafasi yake katika mkururo wa maneno katika sentensi husika.

Utafiti huu umetambulisha makosa yaliyotokea kuhusiana na mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kuzingatia viwango viwili. Makosa hayo yamejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

4.2.4.1 Nafasi za mtenda, kitendo na mtendewa, kutozingatiwa

Katika baadhi ya makala yachapishwayo katika GTL, tuligundua kasoro mbalimbali zinazotakana na mpangilio wa maneno katika sentensi. Mifano ifuatayo inathibitisha hali kwamba nafasi sahihi za mtenda, kitendo na mtendewa hazikutiliwa maanani katika tungo tulizozichanganua.

31a.*Kazi yao waliifanya usiku ....[31]

32a.*Wakazi wengi pombe imefyonza afya kiasi kwamba kazi haiwezi. [32]

33a.*Kuondoa chini ya usimamizi wake ardhi ilizopewa kutunza ....[33]

Katika sentensi (31a), neno **waliifanya**, linatakiwa kuja mwanzo kwa kuwa linasheheni kiambishi ambacho kinasimamia mtenda. Aidha, katika sentensi (32a), neno **pombe** ndilo linalopaswa kuanziwa sentensi kwa kuwa linaelekeza kuhusu chanzo cha athari zinazowakumba wahusika hao. Kwa upande wa sentensi (33a), neno **ardhi** limewekwa mahali si pake kwa kuwa neno **kuondoa** ambalo limeanziwa sentensi hiyo lapaswa kufuatwa na kile kilichoondolewa ili kuimarisha weledi wa tungo. Kwa hivyo, tungo hizo zinaweza kurekebishwa ifuatavyo:

31b. Waliifanya kazi yao usiku ....

32b. Pombe imefyonza afya ya wakazi wengi kiasi kwamba hawaiwezi kazi.

33b. Kuondoa ardhi ilizopewa kutunza, chini ya usimamizi wake.

4.2.4.2 Matumizi mabaya ya vielezi

Vielezi ni maneno ambayo hutumiwa kutoa ujumbe zaidi kuhusu vitenzi. Kuhusu nafasi ya vielezi katika mpangilio wa maneno katika sentensi, Wales (1989), anadokeza kuwa, vinaweza kutumiwa mwanzoni, katikati au mwishoni ingawa kwa kawaida hutumiwa mwishoni. Uchunguzi wetu uligundua matumizi yasiyofaa ya vielezi hasa pale ambapo vilitokea katika nafasi ambazo zingeafiki zaidi maneno mengine. Baadhi ya matumizi hayo yenye dosari yanadhihirika katika tungo zifuatazo:

34a. * Kenya itangojea <u>milele</u> maendeleo huku wananchi ....[34]

35a. * Serikali iliwapa jana ....[35]

36a. * ... wananyanyaswa na nani hapa kisiasa ....[36]

Kielezi **milele** ambacho kimetumiwa katika tungo (34a), kilipaswa kuwekwa baada ya neno **maendeleo**. Msingi wa maelekezo haya ni kuwa kitenzi **itangojea** hakihitaji kuelezewa zaidi kabla ya kutajwa kwa kile kinachongojewa (maendeleo). Na katika tungo (35a), kielezi cha wakati **jana** kinatakiwa kuanzia sentensi ili mawazo yanayofuatia yawe na muumano. Nacho kielezi **kisiasa** katika mfano (36a) kinahitaji kuwekwa baada ya kitenzi **wananyanyaswa** ili kuweka wazi aina ya unyanyasaji unaorejelewa kabla ya kuingilia wazo la wanaohusika. Sentensi sahihi zinapaswa kuwa:

34b. Kenya itangojea maendeleo milele huku wananchi....

35b. Jana, serikali iliwapa ....

36b. ... wananyanyaswa kisiasa na nani hapa....

(Rejelea kiambatisho B na D kwa mifano zaidi ya upungufu katika mpangilio wa maneno katika sentensi).

Tumetumia jedwali nambari 4, kudhihirisha umara-tokezi wa makosa ambayo yalijitokeza katika makundi mawili tuliyoyashughulikia hapo juu. Takwimu zinazojitokeza katika jedwali hili zinakusudiwa kuweka wazi ni kiwango kipi ambacho kilisababisha makosa mengi kuhusiana na mpangilio wa maneno katika sentensi.

Jedwali 4: Umara-tokezi wa makosa yahusuyo mpangilio wa maneno katika sentensi.

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Nafasi ya mtenda, kitendo na mtendewa kutozingatiwa	22	51
Kutumia vielezi mahali si pake	21	49
Jumla	43	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa, makosa kutokana na vipengele hivyo viwili vilivyochunguzwa yalikaribiana sana kiidadi. Kipengele cha kutozingatiwa kwa nafasi za mtenda, kitendo na mtendewa, kilichangia asilimia hamsini na moja (51%) ya jumla ya kasoro zilizojitokeza huku kile cha kutumia vielezi mahali si pake kikiwa na asilimia arobaini na tisa (49%). Jambo hili linatilia nguvu haja ya tahadhari wakati wa utunzi wa sentensi ambapo sehemu ndogo katika sarufi kama vile vielezi huweza kuchangia pakubwa katika kuvuruga tungo. Makini ya mwandishi ndiyo itakayomwepushia matatizo ambayo

yamebainika katika kiwango hiki na hivyo kupelekea utunzi wa tungo zinazokubalika kimpangilio katika lugha ya Kiswahili.

4.2.5 Makosa ya kitahajia

Tahajia ni sehemu muhimu katika lugha yoyote ile na yapaswa kusisitizwa kwa nia ya kuwasilisha habari kwa namna ya kueleweka zaidi. Uendelezaji wa maneno usio sahihi ni jambo mojawapo linalowaudhi wasomaji na kuwafanya wasizingatie ujumbe uliomo hata kama kazi itakuwa imepangwa vizuri (Agee na Kline, 1981). Pia, makosa ya kimaendelezo hupelekea kukwamakwama kwa msomaji na mara nyingine husababisha uwasilishaji wa ujumbe potofu (Peters, 1985). Wataalam hawa ni miongoni mwa wengine ambao wamesisitiza kuhusu haja ya kuendeleza maneno kisahihi ili ujumbe unaopitishwa ueleweke inavyostahili.

Makala yanayochapishwa katika GTL, yalidhihirisha kasoro katika kipengele hiki. Ili kuyashughulikia makosa haya kimantiki tumeyagawa katika makundi mbalimbali. Makundi hayo yamejadiliwa katika sehemu inayofuata.

4.2.5.1 Kuacha herufi katika neno

Upungufu wa herufi katika neno ni hali iliyojitokeza katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa na waandishi wa makala yachapishwayo katika GTL. Matokeo yake yalikuwa kutatiza kwa habari iliyoandikwa humo. Tumezidhihirisha kasoro hizo kupitia kwa mifano ifuatayo:

37a. * ... ushaidi ....[37]

238a. * ... kutanabai ....[38]

39a. * ... hustuki....[39]

Kutokana na mifano hii (37a, 38a, 39a), ni wazi kwamba maneno husika yana dosari za kimaendelezo kwa kukosa herufi **h**. Tunapozingatia mazingira ambamo herufi hiyo ilihitaji kutumiwa, tunachukulia kuwa huenda kutotumiwa kwake kulitokana na athari ya kimatamshi ya waandishi husika. Mara nyingi, utamkaji wa maneno hayo matatu hufanywa bila msisitizo wowote wa herufi **h.** Hivyo basi, hii yaweza kuwa sababu ya maneno hayo kuendelezwa kama yanavyotamkwa kimakosa mara kwa mara. Maneno yaliyoendelezwa vibaya katika mifano hiyo mitatu yaweza kusahihishwa hivi:

137b. ... ushahidi ....

38b. . ... kutanabahi ...

39b. ... hushtuki ....

4.2.5.2 Kutumia herufi isiyofaa

Herufi huwa sehemu mahsusi itumiwayo katika uundaji wa neno. Usahihi wa kimatumizi wa herufi hurahisisha uwasilishaji wa ujumbe unaokusudiwa. Hata hivyo, matumizi yenye kasoro ya kipengele hiki hutatiza upitishaji wa habari unaolengwa. Mifano ya maneno ifuatayo inathibitisha matumizi yasiyofaa ya herufi katika matini tuliyochanganua.

40a. *... kampi....[40]

41a. *Mkaso....[41]

42a. * ... ateteuliwa....[42]

Herufi zilizopigiwa mistari katika tungo (40a, 41a, 42a), zimetumiwa kimakosa na hivyo kutatiza maana inayokusudiwa. Kasoro zinazojitokeza katika tungo (40a na 41a) huenda zinatokana na hali kwamba herufi zilizopaswa kutumiwa (b na z), zina ukuruba mkubwa kimatamshi na hizi ambazo zimetumika (p na s). Tukirejelea sifa bainifu za konsonanti za Kiswahili, tunagundua kuwa sauti [p] na [b] ni vizuiwa na hutamkwa kwa kukutanisha midomo. Sifa ya kipekee inayozitofautisha sauti hizi mbili ni kuwa [p] si ghuna ilhali [b], ni ghuna. Kwa upande mwingine sauti [z] na [s] ni vikwamizwa viniavyotamkiwa kwenye ufizi. Sifa ya ughuna ndiyo huzitofautisha sauti hizi ambapo [z] ni ghuna kinyume cha [s] ambayo si ghuna. Yaelekea kuwa ukuruba huu wa kimatamshi ndio chanzo cha makosa yanayodhihirika katika mifano hiyo miwili. Wakati wa kutumia herufi kama hizi, kunahitajika makini ili kuepuka dosari za aina hii. Maneno katika mifano hiyo mitatu yanaweza kurekebishwa hivi:

40b. ...kambi....

41b. ...Mkazo....

42b. ...atateuliwa ....

4.2.5.3 Kutenganisha neno

Maana katika lugha, hujengwa na maneno ambayo yametumiwa ili kutoa habari inayokusudiwa. Ukamilifu wa neno ni sifa muhimu inayopelekea uandishi kufaulu katika lengo la kupasha ujumbe bila matatizo yoyote. Endapo neno moja litatengwa na kufanywa mawili au zaidi, basi hali hiyo itaathiri usomekaji wa matini husika. Katika kuchungua makala ya GTL, tulikumbana na upungufu uliohusu kutengwa kwa maneno ambayo kikawaida hutakiwa kuandikwa kama neno moja. Mifano ifuatayo inathibitisha uwepo wa makosa ya aina hiyo.

43a. * ... walio mshusha ....[43]

44a.* ... walivyo zipata ....[44]

45a.* ... kuzurura zurura ....[45]

Makosa katika mifano (43a na 44a), imetokea katika vitenzi ambamo viambishi virejeshi 'O' vimetumiwa. Msingi wa upungufu huu huenda ni dhana kwamba kitenzi na kirejeshi 'O' vinapaswa kuunda maneno tofauti kama inavyotokea pale ambapo kirejeshi 'amba' kinahusishwa. Kwa mfano, iwapo kirejeshi 'amba' kingetumiwa katika tungo ya kwanza (43a), tungepata maneno mawili – **ambao walimshusha**. Tunasisitiza kwamba ili neno ambamo 'O' rejeshi imetumika bila 'amba', kuwa sahihi, ni shuruti mwandishi kuliandika kama neno moja badala ya kulifanya kuwa maneno mawili. Tukitazama mfano wa tatu (45a), neno husika ni la uradidi. Maneno mengi ya aina hii, huandikwa kama maneno mawili kimakosa. Waandishi wapaswa kumakinika katika matumizi yao ya maneno ya uradidi ambayo mara nyingi hutumiwa ili kushadidia jambo linalozungumziwa. Kasoro zinazojitokeza katika mifano tuliyotoa, zinaweza kusahihishwa hivi:

43b. .... waliomshusha ....

44b. .... walivyozipata ....

45b. ... kuzururazurura ....

4.2.5.4 Kuunganishwa kwa maneno

Hali inayodhihirika katika kiwango hiki ni kinyume cha ile ambayo tumeizungumzia katika 4.2.5.3. Hapa maneno kamili ambayo yanatakiwa kuandikwa kama maneno tofauti, yanaunganishwa na hivyo kutokea kama neno moja. Tatizo hili limetanda kote katika makala tuliyoyachanganua katika kazi hii. Baadhi ya mifano inayoonyesha upungufu huo ni:

46a. * ...akasisitizahawakuwa ....[46]

47a. * ...katikaujenzi ....[47]

48a. * ... uwongozilikwisha ....[48]

Ili maneno katika mifano hii mitatu (46a, 47a na 48a) kuwa sahihi, shuruti yatengwe kwa kuwa yanajisimamia kimaana na hayahitaji kuunganishwa. Hivyo basi, yanaweza kurekebishwa kwa kutengwa hivi:

46b . ... akasisitiza hawakuwa ....

47b. ... katika ujenzi ....

48b. ... uwongo zilikwisha ....

Kutenganishwa kwa maneno husika, kunayafanya yawe na mantiki na hivyo kutowakanganya wasomaji wa makala ambamo yametumika.

4.2.5.5 Kuongeza herufi/ silabi isiyofaa katika neno.

Katika uandishi, ni muhimu kuzingatia uendelezaji wa maneno kisahihi ili matini ikubalike kwa wasomaji. Nyongeza iliyojitokeza ya herufi/silabi katika maneno yaliyotumiwa na waandishi wa makala mbalimbali ya GTL, ilipelekea maneno husika kuvurugika. Upungufu huu unaleta utata hasa kwa wasomaji ambao huenda wakakanganywa na maendelezo hayo potofu. Ili kudhihirisha namna ambavyo kasoro hizi zilivyojitokeza katika matini iliyochunguzwa, tumedondoa mifano ifuatayo:

49a. *... mwenyekitri ....[49]

50a. * ... waliapa kamawe ....[50]

51a. * ... kustaarabijika ....[51]

Huenda nyongeza zisizofaa za herufi/ silabi zikavuruga maana iliyonuiwa katika tungo. Hili linajitokeza bayana katika tungo (51a), ambapo neno **kustaarabika** limeongezewa silabi '**ji**' kabla ya kiambishi tamati. Matokeo ya hali hiyo ni kuwepo kwa neno ambalo haliwezi kueleweka moja kwa moja. Masahihisho ya maneno hayo yanafuata hapa chini.

49b. ... mwenyekiti ....

50b. ... waliapa kamwe ....

51b. ...kustaarabika ....

(Kwa mifano zaidi ya makosa ya kitahajia, rejelea kiambatisho C na D).

Ulinganisho wa makosa yaliyojitokeza katika vipengele mbalimbali ambavyo tumevishughulikia katika sehemu hii, unawekwa wazi katika jedwali nambari 5, linalofuata hapa chini.

Jedwali 5: Uainisho wa makosa ya kitahajia na umara-tokezi wake

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Kuacha herufi katika neno	69	32
Kutumia herufi isiyofaa	60	28
Kutenganisha neno	12	6
Kuunganisha maneno	18	8
Kuongeza herufi isiyofaa	54	25
Jumla	213	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Matokeo yanayojitokeza katika takwimu za jedwali hili, yanabainisha kuwa vipengele vya: kuacha herufi/ silabi katika neno; kutumia herufi isiyofaa na kuongeza herufi/ silabi isiyofaa, ndivyo vilivyochangia idadi kubwa ya makosa katika kiwango hiki cha tahajia. Umara-tokezi wa makosa katika vipengele hivyo unavyodhihirika katika jedwali nambari 5, ni huu ufuatao: kuacha herufi/ silabi katika neno – asili mia thelathini na mbili (32%); kutumia herufi isiyofaa – asili mia ishirini na nane (28%); kuongeza herufi/ silabi isiyofaa – asili mia ishirini na tano (25%). Hali hii ni tofauti kabisa kiidadi na ile iliyobainika katika vipengele vya: kutenganisha neno – asili mia sita (6%) na kuunganisha maneno – asili mia nane (8%). Ugunduzi huu unaonyesha kuwa vipo vipengele ambavyo kupuuzwa kwake huleta athari kubwa katika uandishi. Ni muhimu kuzingatia uandishi makini ili kuepuka makosa ya kitahajia yaliyobainika katika sehemu hii.

4.2.6 Makosa ya uakifishi

Uakifishi ni hali ya kutumia vituo anuwai katika uandishi. Sentensi ambamo vituo mwafaka vimetumika, zina uwezo wa kupitisha ujumbe ulionuiwa kuliko kinyume chake. Alama za kuakifisha hutumika ili kuweka wazi mawazo ya mwandishi, na kumwelekeza msomaji asomapo maandishi fulani (Wyrick, 1987). Kutokana na maoni ya mtaalam huyu, inabainika kuwa iwapo mwandishi anataka kueleweka vizuri, inamlazimu aakifishe kazi yake barabara. Naye Harmon na wenziwe (1972), wanasisitiza kuwa uakifishi ni sehemu muhimu ya uandishi kama zilivyo sehemu zingine kama vile uteuzi wa maneno, muundo wa sentensi na uteuzi wa mada. Wanaendelea kueleza kwamba uakifishi ni mbinu muhimu katika uandishi kama zilivyo mbinu zingine zinazohusika katika uwasilishaji wa habari. Fauka ya hayo, uakifishi huashiria maana ya maneno mbalimbali yatumiwayo katika uandishi (Baker na Wenziwe, 1981). Maelezo haya yote yanadhihirisha umuhimu wa kipengele cha uakifishi katika mawasiliano. Uchanganuzi wetu wa makala ya GTL, umegundua makosa mbalimbali yanayojitokeza katika kipengele hiki. Kasoro hizo zimejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

4.2.6.1 Kutotumiwa kwa vituo vya uakifishi

Uchunguzi wetu, ulikumbana na matatizo kadha wa kadha katika kipengele hiki cha uakifishi. Tungo zilizotumiwa katika baadhi ya makala yaliyochanganuliwa zilidhihirisha upungufu huo kama inavyobainika katika mifano hii:

52a.* Hongo ya Jaji wa Mahakama ya Rufaa huenda ikazidi Sh. 15 milioni, habari ....[52]

53a.* ...kutumia nyoka katika kuabudu unajisi na uchafuaji hasa wa watoto

....[53]

54a.*...namsamehe Bw Mulu Mutisya ....[54]

Upungufu katika tungo (52a), unasababishwa na kutotumiwa kwa alama za kunukuu (" "), ambazo zinahitajika ili kuonyesha kuwa kauli hiyo ni ya usemi wa dairekti. Katika tungo (53a), koma ilipaswa kutumiwa ili kutenga maneno **kuabudu** na **unajisi,** kwa kuwa ni dhana mbili tofauti na zinazorejelea matukio tofauti. Matokeo ya kutotumia kituo hicho, ni kuwepo kwa utata katika sentensi hiyo ambapo yaweza kuchukuliwa kuwa na maana ya unajisi kuabudiwa. Na tungo (54a) nayo ina kasoro katika neno Bw ambalo ni ufupisho wa bwana. Vifupisho vya aina hiyo vinatakiwa kufuatwa na nukta ili kuwa sahihi. Hivyo basi, kauli hizo zinaweza kusahihishwa hivi:

52b. "Hongo ya Jaji wa Mahakama ya Rufaa huenda ikazidi sh. 15 milioni," habari ....

53b. ... kutumia nyoka katika kuabudu, unajisi na uchafuaji hasa wa watoto ....

54b. ... namsamehe Bw. Mulu Mutisya ....

4.2.6.2 Matumizi yasiyofaa ya herufi kubwa/ ndogo

Baadhi ya makala tuliyoyachungua yalionyesha kasoro katika kiwango hiki. Kunayo maneno yaliyotakiwa kuanzwa kwa herufi ndogo lakini yakaanzwa kwa herufi kubwa na kinyume chake. Hali hiyo inadhihirishwa na mifano inayotolewa hapa chini.

55a.* ... tutakuwa Tumepuuza ....[55]

56a.* ...baada ya kuchapishwa kwa mswada wa Kupambana ....[56]

57a.* ...ametoka garissa ....[57]

Katika sentensi (55a) na (56a), maneno **Tumepuuza** na **Kupambana** yameanzwa kwa herufi kubwa ilhali yametumiwa katikati ya sentensi. Maneno haya yangeanzwa kwa herufi ndogo ili matumizi yao yakubalike katika tungo husika. Kwa upande wa sentensi (57a), neno **garissa** latakiwa kuanza kwa herufi kubwa kwa kuwa ni jina la mji. Kanuni za lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili, huelekeza kwamba majina yote ya miji yaanzwe kwa herufi kubwa bila kujali yanakotokea katika sentensi kwa kuwa yanajumuishwa katika kundi la nomino za pekee. Tungo hizo zinaweza kurekebishwa ifuatayo:

55b. ... tutakuwa tumepuuza ....

56b. ... baada ya kuchapishwa kwa mswada wa kupambana ....

57b. ... ametoka Garissa ....

(Rejelea kiambatisho C kwa mifano zaidi ya uakifishi pungufu).

Kupitia kwa jedwali nambari 6, linalofuata, tumeonyeshwa idadi ya makosa iliyojitokeza katika viwango viwili tulivyojihusisha navyo katika sehemu hii.

Jedwali 6: Makosa ya uakifishi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Ukosefu wa vituo	21	52
Matumizi mabaya ya herufi kubwa/ndogo	19	48
Jumla	40	100

Asili: Takwimu za Utafiti wetu, 2004.

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa idadi ya makosa ya uakifishi yaliyotokana na kasoro katika viwango hivyo viwili – ukosefu wa vituo na matumizi mabaya ya herufi kubwa/ndogo ilikaribia kuwa sawa. Makosa yaliyotokana na ukosefu wa vituo yalikuwa asili mia hamsini na mbili (52%) ilhali yale yaliyosababishwa na matumizi mabaya ya herufi kubwa/ ndogo, ni asili mia arobaini na nane (48%). Matokeo haya yanaonyesha kuwa viwango hivyo viwili vyahitaji kuzingatiwa na waandishi wa matini iliyochunguzwa ili kujiepusha na upungufu katika uakifishi.

4.2.7 Matumizi ya viambishi isivyostahiki

Kiambishi ni sehemu ya neno ambayo hubeba maana fulani katika tungo. Katika lugha ya Kiswahili, vitenzi, majina, vivumishi na vielezi aghalabu huwa na vipandesauti mbalimbali ambavyo husimamia hali tofauti katika sentensi husika. Matumizi ya viambishi sahihi ni msingi wa utunzi wa sentensi ambazo zinakubalika. Utafiti wetu umegundua dosari zinazojitokeza katika uambishaji wa baadhi ya maneno yaliyotumika katika uandishi wa makala ya GTL. Dosari hizo zimejadiliwa katika sehemu ifuatayo.

4.2.7.1 Kutumia viambishi visivyofaa

Katika kiwango hiki tumechunguza na kuonyesha namna viambishi fulani vimetumiwa mahali pasipo pake. Matokeo ya hali hii ni kuvurugika kwa kanuni za uambishaji na hivyo kupelekea tungo husika kutokuwa sahihi. Mifano ya matumizi hayo yenye kasoro yamebainika katika mifano hii:

58a* ...huku wananchi wa kawaida wa<u>na</u>teseka sana .... [58]

59a* ... magari yaingia<u>mo</u> hulipishwa ushuru .... [59]

60a* ... manyumbani mwetu .... [60]

Viambishi vilivyotumika kwa njia isiyo sahihi katika mifano hii mitatu, vimepigiwa mistari. Katika tungo (58a), kiambishi cha wakati **na** kimetumiwa kimakosa kwa kuwa wazo linalowasilishwa katika sentensi hiyo halijafungika kiwakati. Tungo (59a) nayo inanuiwa kuelezea hali ya magari kutozwa ushuru wakati yanapoingia mahali fulani. Hapo kinachopaswa kusisitizwa ni wakati na wala siyo mahali kama inavyotokea kutokana na matumizi ya **mo.** Kwa upande wa tungo (60a), neno **nyumbani** limeambishwa kwa **ma** ili kuonyesha wingi ilhali neno hilo linatakiwa kubaki lilivyo katika umoja na wingi. Hali hii huenda imesababishwa na ujumlishaji uliokithiri kama anavyosema Musau (1992), ambapo maneno ambayo hayahitaji viambishi awali vya wingi, hupachikwa viambishi hivyo kimakosa. Dosari hii imetokana na matumizi ya kiambishi cha wingi cha ngeli ya LI – YA mahali kisipohitajika kwani neno **nyumba** linapatikana katika ngeli ya I – ZI. Hivyo basi, kauli sahihi zilitakiwa kuwa:

58b. ... huku wananchi wa kawaida wakiteseka sana ....

59b ... magari yaingiapo hulipishwa ushuru ....

60b. ...nyumbani mwetu....

4.2.7.2 Ukosefu wa viambishi pale vinapohitajika

Iwapo viambishi vitakosa pale ambapo vinatakiwa kutumiwa, maneno yanayohusika huathiriwa pakubwa na hubaki yakining'inia na ujumbe kutowasilishwa kikamilifu. Makala tuliyochanganua yalidhihirisha kasoro katika kipengele hiki. Mifano ifuatayo inaonyesha hali hiyo.

61a*... watakaopatikana wakihusika wajilaumu .... [61]

62a*... nafasi zao zitachezwa na vijana wengi ambao .... [62]

63a*... hata mwaka mmoja hajakamilika .... [63]

Katika sentensi hizi (61a, 62a na 63a), maneno yaliyopigiwa mistari hayawasilishi ujumbe unaokusudiwa kutokana na ukosefu wa viambishi muhimu. Sentensi hizo zinaweza kusahihishwa kupitia kwa upachikaji wa viambishi vinavyofaa ili tungo hizo zieleweke. Hebu tutazame jinsi sentensi sahihi zinavyopaswa kuwa:

61b.... watakaopatikana wakihusika watajilaumu....

62b.... nafasi zao zitachezwa na vijana wengine ambao ....

63b.... hata mwaka mmoja hujakamilika ....

Viambishi vilivyopigiwa mistari ndivyo vimeongezwa ili kuondoa utata uliokuwepo katika sentensi za awali.

(Kwa mifano zaidi ya matumizi mapungufu ya viambishi, rejelea kiambatisho C na D).

Tumetumia jedwali nambari 7, kwa nia ya kuweka wazi umara-tokezi wa makosa katika viwango viwili ambavyo tumevichunguza katika sehemu hii.

Jedwali 7: Makosa yanayohusu matumizi ya viambishi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Kutumia viambishi visivyofaa	63	61
Ukosefu wa viambishi pale vinapohitajika	41	39
Jumla	104	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Matokeo haya yanadhihirisha kuwa makosa mengi yaliyohusu viambishi yalisababishwa na matumizi ya viambishi isivyostahili ambapo idadi ya kasoro zilizotokana na hali hiyo ilifikia asili mia sitini na moja (61%). Kwa upande mwingine, makosa yaliyotokana na ukosefu wa viambishi pale vinapohitajika, yalichangia asili mia thelathini na tisa (39%) ya makosa yote katika sehemu hiyo.

4.2.8 Kujirudia katika sentensi

Kujirudia katika sentensi ni hali inayosababishwa na uwasilishaji wa wazo moja kwa kutumia maneno yaliyo na maana sawa. Katika tungo zenye kasoro hii, mtunzi huwa ametaja jambo moja mara mbili na hivyo kuudhi wasomaji kwani maneno mengi yanayorejelea wazo lile lile moja, huwachosha (McMahan na Day, 1984). Kasoro hii ilijitokeza katika matini tuliyochanganua, hali iliyopelekea ujumbe kuwasilishwa kwa maneno mengi pasipo na haja ya kufanya hivyo. Makosa yaliyojitokeza katika kipengele hiki ndiyo tunayoyajadili katika sehemu hii.

4.2.8.1 Marudio ya (ma)neno katika sentensi

Uchanganuzi wa makala mbalimbali ya GTL, umeonyesha kuwa katika baadhi ya tungo, neno au maneno fulani yamerudiwa bila sababu maalum. Jambo hili limefanya sentensi zingine kuwa ndefu ilhali kulikuwa na uwezekano wa kutumia maneno machache ili kutosheleza haja ya mawasiliano iliyokusudiwa. Kasoro hii huenda ilisababishwa na usahaulifu wa mwandishi ambapo alirudia neno fulani bila kugundua kuwa amefanya hivyo. Ifuatayo ni mifano inayodhihirisha upungufu huo.

64a.* ... katika uajiri wa wafanyakazi wa mahakama na mchango wa mishahara ya chini katika idara hiyo inavyochangia ufisadi.[64]

65a.* ... wakimbizi hao kweli wanasalimisha usalama wao ....[65]

66a.* ... ni lazima tujilazimishe kudumisha usafi ....[66]

Maneno yaliyopigiwa mistari katika mifano hii (64a, 65a na 66a), yamerudiwa katika tungo pasipo haja. Ili kusahihisha tungo hizo, inatubidi tudondoshe yale maneno ambayo yamerudiwa na hivyo kuwa na tungo hizi ambazo zinakubalika katika Kiswahili sanifu:

64b. ... katika uajiri wa wafanyakazi wa mahakama na mchango wa mishahara ya chini katika idara hiyo kwa ufisadi ....

65b. ... wakimbizi hao kweli wanajisalimisha ....

Au

... wakimbizi hao kweli wanakimbilia usalama wao....

66b. ... ni lazima kudumisha usafi ....

4.2.8.2 Matumizi ya maneno yenye maana sawa

Ingawa visawe hutekeleza jukumu muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe, vinapotumiwa katika tungo moja, huifanya iwe ndefu na inayowachosha wasomaji. Ili tungo ieleweke vizuri, shuruti mtunzi atumie maneno yanayowasilisha ujumbe bila kuongeza mengine ambayo yanarejelea wazo hilo moja ambalo linazungumziwa. Matumizi ya visawe katika tungo moja yalibainika katika baadhi ya makala ya GTL. Mifano ifuatayo inadhihirisha jambo hilo.

67a.* ... wanawake ajuza ....[67]

68a.* ... huzuzua hasara ... kutoa uamuzi ama hukumu zisizo za haki ....[68]

69a.* ... wanasiasa wasithubutu kujaribu kurudisha ....[69]

Katika tungo (67a), neno **ajuza** ambalo linamaanisha mwanamke mzee sana, lilistahili kutumiwa pekee bila kutangulizwa na neno **wanawake**. Tungo (68a) nayo inaonyesha matumizi ya visawe, **uamuzi** na **hukumu** katika kauli moja badala ya kutumia neno mojawapo ambalo lingetoshelesha haja ya kimawasiliano. Hali kama hiyo inajitokeza katika tungo (69a), ambapo maneno **wasithubutu** na **kujaribu** yana maana sawa tukirejelea muktadha wa kimatumizi husika. Sentensi sahihi zinaweza kuwa:

67b. ... wanawake wazee sana ....

68b. ... huzuzua hasara ... kutoa uamuzi usio wa haki ....

69b. ... wanasiasa wasithubutu kurudisha ....

Au

67b. ... ajuza....

68b. ... huzuzua hasara ... kutoa hukumu zisizo za haki ....

69b. ... wanasiasa wasijaribu kurudisha ....

(Rejelea kiambatisho C na D kwa mifano zaidi ya kasoro ya kujirudia katika sentensi).

Kama njia ya kulinganisha idadi ya makosa yaliyotokana na vipengele viwili ambavyo tumevijadili katika 4.2.8.1 na 4.2.8.2, tumetumia jedwali nambari 8, linalofuata.

Jedwali 8: Makosa yahusuyo kujirudia katika sentensi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Marudio ya (ma)neno katika sentensi	12	27
Matumizi ya visawe	33	73
Jumla	45	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Ni bayana kutokana na takwimu za jedwali nambari 8, kuwa makosa mengi katika sehemu hii yalisababishwa na matumizi ya visawe katika tungo moja. Kipengele hicho kimechangia asili mia sabini na tatu (73%) ya jumla ya makosa yaliyogunduliwa katika sehemu hiyo. Idadi ya makosa yaliyotokana na marudio ya (ma)neno katika sentensi, yamechangia asili mia ishirini na saba (27%). Matokeo haya yameweka wazi haja ya waandishi kutathmini visawe wanavyonuia kutumia katika uandishi wao kwa lengo la kuepuka marudio yasiyofaa katika uwasilishaji wa ujumbe.

4.2.9 Matumizi yasiyofaa ya vihusishi

Kihusishi hutumiwa kuonyesha uhusiano uliopo baina ya maneno au dhana mbalimbali katika sentensi. Ili kutimiza jukumu hili, ni muhimu vihusishi vinavyofaa vitumike katika tungo husika. Katika kuchungua makala yachapishwayo katika GTL, tumekumbana na matumizi yasiyo sahihi ya vihusishi katika baadhi ya sentensi. Kasoro zilizojitokeza zimewekwa wazi katika sehemu hii.

4.2.9.1 Vihusishi visivyostahiki, kutumiwa

Katika baadhi ya makala tuliyoyachunguza, vihusishi fulani vilitumiwa kimakosa badala ya vingine ambavyo ndivyo vingefaa kutumiwa. Jambo hili wakati mwingine hupotosha habari inayonuiwa kupitishwa. Tumedondoa mifano ifuatayo ili kuthibitisha

kuwepo kwa kasoro hii.

70a.* ... utafikiria wana wajibu wa udongo na sio roho ya watu ....[70]

71a.* Hata vyoo vya hospitali za umma na za baadhi ya shule ....[71]

72a.* ... alizirai huku kwa chumba jirani ....[72]

Kasoro katika tungo hizo tatu (70a, 71a na 72a), zinasababishwa na kutumiwa kwa vihusishi ambavyo siyo sahihi. Hali hii inaweza kurekebishwa kupitia kwa matumizi ya vihusishi sahihi badala ya vile vyenye upungufu. Sentensi sahihi zitakuwa hivi:

70b. ... utafikiria wana wajibu wa udongo na sio roho za watu ....

71b. Hata vyoo vya hospitali za umma na vya baadhi ya shule ....

72b. ... alizirai huku katika chumba jirani ....

4.2.9.2 Kutotumiwa kwa vihusishi, vinapostahili

Hali ambapo vihusishi havikutumiwa mahali vinapohitajika ilidhihirika katika utafiti wetu. Kunazo sentensi ambazo zilipungukiwa na vihusishi muhimu, jambo lililopelekea kuathiriwa kwa ujumbe uliokusudiwa kupitishwa. Mifano ifuatayo inathibitisha upungufu huo.

73a.* ... serikali haitafanikiwa kuwa na sifa nzuri nchi za kigeni ....[73]

74a.* ... haitakuwa lazima kuwa mmojawapo makamu ....[74]

75a.* ... wataingia karne mpya ....[75]

Ili kurekebisha tungo hizi tatu, inabidi mtunzi atumie vihusishi mwafaka kulingana na muktadha wa kimatumizi unaohusika. Tungo (73a na 75a), zinapaswa kuongezewa kihusishi **katika** ilhali tungo (74a), inahitaji kihusishi **wa** ili kuwasilisha habari inayojitosheleza. Hivyo basi, sentensi sahihi zitakuwa:

73b. ... serikali haitafanikiwa kuwa na sifa nzuri katika nchi za kigeni ....

74b. ... haitakuwa lazima kuwa mmojawapo wa makamu ....

75b. ... wataingia katika karne mpya ....

Maneno yaliyopigiwa mistari, ndiyo vihusishi ambavyo vilikuwa vimekosa katika sentensi tatu za awali (73a, 74a na 75a). Matumizi ya vihusishi hivyo yanavyaza muumano katika tungo husika, na hivyo kurahisisha uelewekaji wa habari inayopitishwa.

4.2.9.3 Kupachikwa kwa vihusishi visipostahili

Upachikaji wa vihusishi visipostahili ni kasoro nyingine iliyojitokeza katika matini iliyochunguzwa. Wakati mwingine, kihusishi kiliongezwa mahali ambapo tayari kulikuwa na kingine sahihi huku mara zingine kikiwekwa pale kisipohitajika kabisa. Tumedondoa kauli

zifuatazo kuthibitisha hali hiyo.

76a.* ... mkutanoni wa Mombasa ....[76]

77a.* ...apumzike kwa sababu ya umri nao si mdogo ....[77]

78a.* ...isipokuwa kuwapandisha vyeo vya viongozi wake ....[78]

Maneno yaliyopigiwa mistari katika tungo hizi tatu (76a, 77a na 78a), yanatakiwa kudondoshwa ili sentensi husika ziwe sahihi. Matokeo ya udondoshaji huo ni kauli hizi sahihi:

76b. ... mkutanoni Mombasa ....

77b. ... apumzike kwa sababu umri nao si mdogo ....

78b. ... isipokuwa kuwapandisha vyeo viongozi wake ....

(Kwa mifano zaidi ya matumizi yasiyofaa ya vihusishi, rejelea kiambatisho B, C na D).

Jedwali nambari 9, limetumiwa kuonyesha umara-tokezi wa matumizi yasiyofaa ya vihusishi kwa kurejelea vipengele vitatu tulivyovishughulikia katika sehemu hii.

Jedwali 9: Matumizi yasiyofaa ya vihusishi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Vihusishi visivyostahiki, kutumiwa	34	72
Ukosefu wa Vihusishi vinapostahili	5	11
Kupachikwa kwa Vihusishi visipostahili	8	17
Jumla	47	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Matokeo yaliyomo katika jedwali nambari 9, yanadhihirisha kuwa makosa mengi yahusuyo vihusishi yalisababishwa na matumizi ya vihusishi visivyostahiki. Kipengele hiki kilisababisha asili mia sabini na mbili (72%) ya kasoro zote zilizotokea katika sehemu hiyo. Vipengele hivyo vingine – ukosefu wa vihusishi vinapostahili na upachikaji wa vihusishi visipostahili, vilichangia asili mia kumi na moja (11%) na asili mia kumi na saba (17%) ya makosa, kwa mfuatano huo. Takwimu hizi zimeweka wazi ugunduzi kuwa matumizi ya vihusishi visivyostahiki ndiyo yaliyolemaza matini nyingi zilizochunguzwa na hivyo kuna haja ya kusisitiza kwamba waandishi wamakinike zaidi ili kuyaepuka makosa husika.

4.2.10 Makosa katika matumizi ya viunganishi

Viunganishi hutumiwa kwa nia ya kuleta mshikamano katika sentensi kupitia kwa kuweka maneno, virai na sentensi pamoja (Miller na Wenziwe, 1978). Wanaendelea kueleza

kuwa maneno ambayo hutumiwa kama viunganishi huwa ishara kwa wasomaji kuhusu namna sentensi moja inavyohusiana na nyingine. Umuhimu wa viunganishi umetanda kote katika uandishi wa matini mbalimbali. Baadhi ya makala yachapishwayo katika GTL, yalidhihirisha matumizi yasiyofaa ya viunganishi katika viwango mbalimbali. Viwango hivyo ndivyo vinavyojadiliwa katika sehemu hii.

4.2.10.1 Matumizi ya viunganishi visivyofaa

Katika makala tuliyochanganua, tuligundua kuwa matumizi mengine ya viunganishi hayakuwa mwafaka. Hali hii huenda ilitokana na kutoeleweka kwa baadhi ya viunganishi kwa watumizi wake, jambo lililopelekea kutumiwa vibaya kwa viunganishi husika katika sentensi anuwai. Kilichobainika ni kuwa iwapo viunganishi sahihi vingetumiwa badala ya hivyo potofu, basi sentensi zilizovisheheni, zingewasilisha ujumbe kikamilifu. Yafuatayo ni matumizi ya viunganishi yenye dosari katika matini tuliyochunguza.

79a * ... hawana maslahi ya kitaifa moyoni bali hali ya baadaye ya nchi hii ni ya kila mtu ....[79.]

80a * Elimu ina manufaa mengi bali na kuajiriwa....[80]

81a * ...kwa hivyo kina mama msirudi nyuma hata kidogo lakini mjitokeze zaidi ....[81]

Maneno ambayo yamepigiwa mistari ndiyo yametumiwa kama viunganishi katika tungo hizo tatu (79a, 80a na 81a). Hata hivyo matumizi haya siyo sahihi kwa kuwa viunganishi hivyo vimetumiwa badala ya vile mwafaka tunapozingatia muktadha wa kimatumizi. Tungo hizo zinaweza kurekebishwa kwa kutumia viunganishi vinavyofaa kama inavyojitokeza katika sentensi hizi:

79b. ... hawana masilahi ya kitaifa moyoni ilhali hali ya baadaye ya nchi hii ni ya kila mtu ....

80b. Elimu ina manufaa mengi mbali na kuajiriwa ....

81b. ... kwa hivyo kina mama msirudi nyuma hata kidogo bali mjitokeze zaidi ....

4.2.10.2 Kutotumiwa kwa viunganishi vinapohitajika

Ukosefu wa viunganishi pale vilipohitajika ni kasoro nyingine iliyojitokeza katika makala yachapishwayo katika GTL. Upungufu katika kipengele hiki ulisababisha sentensi zilizoathiriwa kukosa mshikamano ambao, ni muhimu katika uandishi. Mifano ifuatayo imedondolewa ili kudhihirisha kasoro zilizojitokeza katika kiwango hiki.

82a. * Ufisadi pamoja __ ukosefu wa umakini ....[82]

83a. *... alidai mawaziri ... Uhuru Kenyatta __ ateuliwe ....[83]

84a. *... kutokana __ rekodi ....[84]

Mapengo yaliyoachwa katika tungo hizo tatu (82a, 83a na 84a) yanawakilisha sehemu ambazo zinahitaji viunganishi ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kikamilifu. Tungo sahihi zilitakiwa kuwa hivi:

82b. Ufisadi pamoja na ukosefu wa makini....

83b... alidai mawaziri ... Uhuru Kenyatta ili ateuliwe ....

84b... kutokana na rekodi ....

Ni muhimu kutambua kuwa kunayo maneno katika lugha ya Kiswahili ambayo yanapotumika, mara nyingi hufuatiwa na kiunganishi moja kwa moja. Maneno hayo ni kama vile **pamoja** na **kutokana** ambayo aghalabu hufuatiwa na kiunganishi **na** kama inavyodhihirika katika sentensi hizo zilizosahahihishwa.

4.2.10.3 Kuwekwa kwa viunganishi visipohitajika

Katika baadhi ya makala ya GTL, viunganishi vilipachikwa mahali ambapo havikuhitajika na hivyo kusababisha upungufu katika tungo husika. Kwingineko, viunganishi viliongezwa katika sehemu ambazo tayari zilikuwa na viunganishi mwafaka na hivyo kutatiza uwasilishaji wa habari kupitia kwa sentensi hizo. Tungo zifuatazo zinabainisha kasoro zilizojitokeza katika kiwango hiki.

85a.*... mbabe na ambaye alikaidi amri ya....[85]

86a.*... kashfa inayohusisha na Land Rover ....[86]

87a. *... mbolea madukani ilhali huku mbolea ....[87]

Usahihisaji wa tungo hizo tatu (85a, 86a na 87a) utahusisha kudondoshwa kwa viunganishi vilivyopigiwa mistari kwa kuwa havitekelezi jukumu lolote katika muktadha huo. Tungo sahihi zitakuwa:

85b... mbabe ambaye alikaidi amri ya ....

86b... kashfa inayohusisha Land Rover ....

87b....mbolea madukani huku mbolea ....

(Rejelea kiambatisho B kwa mifano zaidi ya matumizi yasiyofaa ya vuinganish).

Katika juhudi za kutambulisha ni kipengele kipi ambacho kilisababisha makosa mengi kuliko vingine katika sehemu hii inayojikita katika matumizi ya viunganishi, tumetumia jedwali nambari 10.

Jedwali 10: Makosa yahusuyo viunganishi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Matumizi ya viunganishi visivyofaa	22	63
Kutotumiwa kwa viunganishi vinapohitajika	7	20
Kuwekwa kwa viunganishi visipohitajika	6	17
Jumla	35	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Takwimu za jedwali nambari 10, zinaonyesha kuwa makosa mengi yahusuyo viunganishi yalisababishwa na matumizi ya viunganishi visivyofaa. Kipengele hiki kilichangia asili mia sitini na tatu (63%) ya makosa yote yaliyojitokeza katika kiwango hiki. Kwa upande mwingine, kipengele cha kutotumiwa kwa viunganishi vinapohitajika kilichangia asili mia ishirini (20%) ya makosa huku kile cha kuwekwa kwa viunganishi visipohitajika kikiwa na asili mia kumi na saba (17%).

4.2.11 Miundo changamano

Katika uandishi, wakati mwingine makosa mengi huweza kujitokeza katika sentensi kiasi cha kushindwa kuyawekea mipaka kimatapo (McMahan na Day, 1984; Robey na wenziwe, 1984). Wataalam hawa wanashikilia kuwa miundo changamano huwa matokeo ya mwandishi kutanguliza sentensi kwa wazo fulani, akapoteza mtazamo katikati na kuikamilisha kwa njia nyingine. Aidha, tungo za aina hii zaweza kutokea ikiwa mtunzi ama atachanganya kauli na swali katika sentensi moja au kuhusisha mawazo mawili tofauti katika sentensi, hali inayowakanganya wasomaji. Katika utafiti wetu, tulikumbana na sentensi zilizokuwa na kasoro nyingi kiasi kwamba mawazo yaliyowasilishwa hayakueleweka. Upungufu huo ndio tunaoushughulikia katika sehemu hii.

4.2.11.1 Mawazo yasiyowiana katika sentensi moja

Mawazo ambayo kimsingi ni tofauti yakiwekwa katika sentensi moja, hupelekea kuvurugika kwa tungo husika. Uchunguzi wetu uligundua kuwa baadhi ya sentensi zilizotumiwa kuwasilishia ujumbe kupitia kwa makala ya GTL, zilisheheni zaidi ya wazo moja, hali iliyosababisha upungufu wa ufasaha. Tumetumia mifano ifuatayo kubainisha kasoro hii.

88a* Utamaduni wa jamii fulani haingekuwa vizuri jamii nyingine kuingilia mpaka isababishe kupigwa marufuku.... [88]

89a*... wanaotumia vipaza sauti kutojali na kuwagoa wavukaji, ambao huchanganyikiwa kutokana na sera mbovu ya kampuni .... [89]

90a* Hata hivyo, hatuelewi jinsi mahakama hiyo ingefikia uamuzi wa kuadhibu mama huyu, aliyesemekana katika ripoti ya probesheni kuwa mlevi, angepata faini ya Sh. 20,000 kama adhabu ya kosa lake .... [90]

Tunapochungua mifano hii ya sentensi (88a, 89a na 90a), tunaona kwamba uchanganyaji wa mawazo umeziathiri tungo hizi kwa kiasi kikubwa na hivyo kutatiza ujumbe unaonuiwa kupitishwa. Katika mfano (88a), mawazo matatu yamewekwa pamoja bila kuhusishwa ipasavyo. Tungo hiyo inazungumzia: utamaduni wa jamii ulioingiliwa; jamii iliyoingilia na athari ya mwingilio huo (kupigwa marufuku kwa utamaduni husika). Mawazo haya yalipaswa ama kutengwa katika tungo tofauti au kuhusishwa ipasavyo ili kuvyaza sentensi sahihi. Hali kama hiyo inajitokeza katika mfano (89a), ambapo mawazo matatu yamejitokeza katika sentensi moja. Tungo hiyo inajumuisha mawazo haya: matumizi ya vipaza sauti na kutojali wavukaji; kuchanganyikiwa kwa wavukaji na sera mbovu ya kampuni. Sentensi hii inazua utata kutokana na wazo la pili (kuchanganyikiwa kwa wavukaji), kwani haieleweki kama hali hiyo inatokana na vipaza sauti au sera mbovu ya kampuni. Mfano (90a), nao unahusisha mawazo matatu – mahakama kufikia uamuzi wa kumwadhibu mama; ripoti ya probesheni na faini ya Sh. 20,000 kama adhabu ya kosa. Ni bayana kuwa mawazo haya hayajawasilishwa kwa njia yenye mshikamano na hivyo kutoeleweka kikamilifu kwa habari inayopitishwa. Aidha, ni muhimu kutaja kwamba matumizi ya angepata faini katika mfano (90a), yana kasoro kwani katika Kiswahili sanifu tunasema, angepigwa/angetozwa faini

4.2.11.2 Tungo lemavu

Tungo zingine zilizotumika katika makala tuliyoyachanganua zilikuwa lemavu kutokana na kuwepo kwa aina mbalimbali za makosa. Tumedondoa mifano ifuatayo ili kubainisha kasoro zilizogunduliwa katika kipengele hiki.

91a.*... hairidhishi baadhi ya wengi .... [91]

92a.* Maji yakatwe, ndivyo, lakini maafisa hao .... [92]

93a.* ...hawajapiga hatua yoyote kuondoka nje ya maskani zaidi tangu Marekani .... [93]

Matumizi ya maneno **baadhi** na **wengi** katika mfano (91a), yanakanganya. Kasoro hii yaweza kurekebishwa kwa kudondosha neno mojawapo hasa **wengi** iwapo nia ya mwandishi

ni kuelezea kutoridhika kwa sehemu ya wahusika. Katika mfano (92a), neno **ndivyo** linalemaza sentensi hiyo kwani halichangii chochote katika kupitisha ujumbe uliomo. Yaelekea kuwa mfano (93a), umepungikiwa na maneno muhimu ambayo yangeiwezesha tungo hiyo kueleweka kikamilifu. Maneno hayo huenda yanahusu wakati uliopita bila wahusika kuondoka nje ya maskani.

Jedwali nambari 11, limetumiwa kuonyesha umara-tokezi wa makosa katika vipengele vilivyoshughulikiwa katika sehemu hii.

Jedwali 11: Makosa yanayohusu miundo changamano

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Mawazo yasiyoambatana katika sentensi moja	17	47
Tungo lemavu	19	53
Jumla	36	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004


Kutokana na takwimu za jedwali nambari 11, ni wazi kuwa vipengele viwili vilivyoshughulikiwa vilikuwa na makosa yaliyokaribiana sana kiidadi. Mawazo yasiyoambatana katika sentensi moja, yalichangia asili mia arobaini na saba (47%) ya makosa huku tungo lemavu zikichangia asili mia hamsini na tatu (53%).

Katika hatua ya kuhitimisha sehemu hii ambayo imejikita katika kubainisha makosa mbalimbali ya kisarufi ambayo yamejitokeza katika makala ya GTL, tuliyoyachanganua, tumetumia jedwali nambari 12 na grafu A kutimizia lengo hilo. Vipengele vyote vilivyochunguzwa, vimeshughulikiwa huku umara-tokezi wa makosa ukidhihirishwa.

Jedwali 12: Umara-tokezi wa makosa katika vipengele anuwai vya kisarufi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Kutokamilika kwa sentensi	140	17
Ukosefu wa upatanisho wa kisarufi	65	8
Upungufu katika mnyambuliko wa vitenzi	57	7
Kasoro za mpangilio wa maneno katika sentensi	43	5
Makosa ya kitahajia		
Kasoro katika uakifishi	213	26
Matumizi yasiyofaa ya viambishi	40	5
Kujirudia katika sentensi	104	13
Matumizi ya vihusishi isivyostahiki	45	5
Matumizi ya viunganishi yasiyofaa	47	6
Miundo changamano	35	4
	36	4
Jumla	825	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004



Grafu A: Makosa katika vipengele mbalimbali vya kisarufi

Ufunguo

Ks - Kutokamilika kwa sentensi

Uuk - Ukosefu wa upatanisho wa kisarufi

Umm – Upungufu katika mnyambuliko wa maneno

Kmms –Kasoro za mpangilio wa maneno katika sentensi

Mk - Makosa ya kitahajia

Kku - Kasoro katika uakifishi

Myv - Matumizi yasiyofaa ya viambishi

Kks - Kujirudia katika sentensi

Mvi – Matumizi ya vihusishi isivyostahiki

Mvy – Matumizi ya viunganishi yasiyofaa

Mc - Miundo changamano

Kama inavyodhihirika katika jedwali nambari 12 na grafu A, vipengele vya makosa ya kitahajia; kutokamilika kwa sentensi na matumizi yasiyofaa ya viambishi, ndivyo vilivyochangia idadi kubwa zaidi ya makosa katika sarufi. Vipengele hivyo vilikuwa na makosa kiasi cha asili mia ishirini na sita (26%); asili mia kumi na saba (17%) na asili mia kumi na tatu (13%), kwa mfuatano huo. Makosa yaliyojitokeza kuhusiana na ukosefu wa upatanisho wa kisarufi yalichangia asili mia nane (8%) ilhali yale yahusuyo upungufu katika mnyambuliko wa maneno yalikuwa asili mia saba (7%). Kwa upande mwingine, kiasi kidogo cha makosa kilitokana na matumizi ya vihusishi isivyostahiki (asili mia sita); kujirudia katika sentensi (asili mia tano); kasoro za mpangilio wa maneno katika sentensi (asili mia tano); kasoro katika uakifishi (asili mia tano); miundo changamano (asili mia nne), na hatimaye matumizi yasiyofaa ya viunganishi (asili mia nne).

4.3 Msamiati

Msamiati ni jumla ya maneno yatumikayo katika lugha ili kufanikisha mawasiliano. Kufaulu katika upashanaji wa habari hutegemea uteuzi wa maneno kwa kiasi kikubwa. Uteuzi wa maneno huweza kusababisha tofauti kubwa katika ubora wa uandishi kutokana na hali kwamba iwapo neno ama lisilo sahihi au lenye utata litatumiwa badala ya lile sahihi, basi ujumbe unaowasilishwa hautaeleweka (Wyrick, 1987). Mtaalam huyu anaendelea kusisitiza kwamba haitoshi tu mwandishi kujua anachomaanisha bali ajizatiti kupitisha ujumbe wake kwa kutumia maneno yanayofaa ili wasomaji waelewe anachoeleza kwa uhakika. Sentensi nzuri yaweza kuharibiwa ikiwa neno lisilofaa litatumiwa (Robey na wenziwe, 1984). Hivyo basi, ni jukumu lisiloepukika kwa mwandishi awaye yeyote kuteua maneno sahihi ambayo yataeleweka bila kumwacha msomaji na tashwishi kuhusu kinachokusudiwa katika matini anayoisoma.

Aidha, katika kuteua maneno, inambidi mwandishi kutumia yale ambayo yanalenga ndipo. Ni muhimu kuteua neno mahsusi ambalo litawasilisha wazo ulilonalo akilini (Agee na

Kline, 1981). Katika utafiti huu, tumetambulisha makosa mbalimbali ambayo yametokea katika uteuzi wa maneno yaliyotumika kuwasilishia ujumbe katika GTL. Kasoro za aina hii zimechangia kwa njia moja au nyingine ukosefu wa ueledi katika sentensi zilizotumika. Sehemu ifuatayo inashughulikia makosa ya kimsamiati ambayo yaligunduliwa katika viwango mbalimbali vya kimatumizi.

4.3.1 Matumizi ya maneno yasiyofaa

Ufaafu wa neno ni sifa inayopelekea matumizi yake kukubalika katika mazingira fulani ya kimatumizi. Uteuzi na matumizi ya maneno yasiyofaa huvyaza sentensi ambazo hazieleweki na hivyo kumtatiza msomaji. Makala tuliyoyapitia yalidhihirisha kuhusishwa kwa maneno yasiyofaa katika utunzi wa baadhi ya sentensi kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

94a. *... kutolewa hukumu za malipo hadi kutayarisha stakabadhi .... [94]

95a*... akikwepa kwenye bweni .... [95]

96a*... waliofanya vyema aidha wapatiwe fursa ya kujiunga na masomo ya ufundi ama .... [96]

Maneno yaliyopigiwa mistari katika tungo hizo tatu (94a, 95a na 96a), hayafai. Maana inayokusudiwa inatatizwa kutokana na matumizi ya maneno hayo potofu. Kwa mfano, tukichungua tungo (96a), tunagundua kuwa neno **aidha** limetumiwa kimakosa. Huenda chanzo cha kasoro hii, ni tafsiri sisisi kutoka neno **either** la Kiingereza, muundo ambao hauko katika Kiswahili. Katika Kiswahili, neno **aidha** lina maana ya – isitoshe au zaidi ya hayo, na mara nyingi huwa mwanzoni mwa sentensi (Idarus, 1983). Ili kusahihisha tungo hizo, ni shuruti mtunzi atumie maneno ambayo yatawasilisha ujumbe unaohusika kwa uhakika. Tungo hizo zinaweza kurekebishwa hivi:

94b. ... kutolewa hukumu za faini hadi kutayarisha stakabadhi ....

95b. ... akijificha kwenye bweni ....

96b. ... waliofanya vyema ama wapatiwe fursa ya kujiunga na masomo ya ufundi au ....

4.3.2 Matumizi ya maneno ya jozi bainifu isivyostahiki

Katika lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili, kunayo maneno ambayo yana ukuruba mkubwa kimaandishi na kimatamshi. Kwa mujibu wa TUKI (1990), jozi bainifu ni maneno mawili yanayotofautiana kutokana na fonimu moja tu. Hata hivyo, maneno kama hayo huwa

na maana tofauti kabisa. Katika Kiswahili, mifano ya maneno ya jozi bainifu ni pamoja na: Baa na paa; sura na fura; baka na bata; mahari na mahali; saa na zaa.Sauti zilizo pigiwa mstari katika mifano hiyo ndizo huitwa fonimu kwa kuwa zinasababisha tofauti katika maana zinazowasilishwa na maneno husika. Kutokana na hali hiyo ya ukuruba, waandishi wengine hukanganyikiwa wanapotumia maneno hayo ambapo neno moja linatumiwa badala ya lile lingine ambalo ndilo sahihi. Matokeo ya matumizi haya ni sentensi ama zisizoeleweka au zinazowasilisha ujumbe tofauti na ule uliokusudiwa. Uchunguzi wetu, uligundua kasoro za aina hii katika baadhi ya makala tuliyoyachanganua. Tumedondoa tungo zifuatazo ili kubainisha upungufu huo.

97a.*... nani atakayemridhi, atakapong'atuka ....[97]

98a.* ... baraza lolote linalodhamini amani na utangamano....[98]

99a.* ... juzi nililengwa na majonzi ....[99]

Maneno yaliyopigiwa mistari katika mifano hii, yametumiwa kimakosa badala ya yale sahihi ambayo yana ukuruba nayo. Matumizi ya maneno yaliyo na sauti 'dh' badala ya 'th' katika tungo (97a) na (98a), yamesababisha tofauti kubwa kati ya maana inayojitokeza na ile iliyokusudiwa. Hali kama hiyo inajitokeza katika tungo (99a), ambapo neno lililotumiwa lina maana tofauti na ile iliyonuiwa na mwandishi. Tukizingatia maelezo yaliyotolewa na TUKI (1981), maneno hayo matatu yaliyotumiwa isivyofaa yana maana zifuatazo: **ridhi** – kubali au pendezwa na jambo; **dhamini** – chukulia ahadi mtu kuwa atatimiza jambo fulani; okoa mtu kutoka kifungoni au weka fedha au mali kama rehani kwa ajili ya kufidia mkopo iwapo utashindwa kuulipa; **majonzi** – hali ya kutokuwa na furaha kutokana na tukio la kusikitisha; huzuni, sikitiko, simanzi. Hivyo basi, ni wazi kutokana na maana hizi zilizotolewa kuwa maneno husika hayakustahili kutumiwa katika tungo hizo hasa tukitilia maanani muktadha wa kimatumizi.Tungo sahihi zilipaswa kuwa:

97b. ... nani atakayemrithi, atakapong'atuka....

98b. ... baraza lolote linalothamini amani na utangamano....

99b. ... juzi nililengwa na machozi ....

Ingawa tumejihusisha na matumizi yasiyofaa ya maneno ya jozi bainifu,ni muhimu kusisitiza kwamba neno **nililengwa** katika mfano (99a na 99b) linatia kauli hizo dosari.Mwandishi husika angetumia neno **nililengwalengwa** ili kuvyaza tungo sahihi.

4.3.3 Matumizi ya maneno yenye maana finyu

Matumizi mengine yaliyojitokeza katika matini tuliyochunguza ni yale ya maneno yenye maana finyu. Hali hii ilielekea kusababishwa na ukosefu wa makini katika uteuzi wa

maneno yaliyotumiwa katika baadhi ya makala. Maneno ambayo hukubalika yatumikapo katika mazingira yasiyo rasmi yalihamishiwa mazingira rasmi ambapo hayakubaliki. Matumizi ya aina hii hutatiza ujumbe unaowasilishwa kwani huenda usieleweke kwa hadhira pana. Upungufu huo unajitokeza katika kauli zifuatazo:

100a* ... amekalia tena kiti cha urais .... [100]

101a* ... viwanda vinaanguka kila siku .... [101]

102a*... Askofu mkuu Ndingi alisema baadhi yao wamelengwa kidole kwa kuwapa wahalifu bunduki zao .... [102]

Msamiati uliopigiwa mistari katika mifano hii, unabainisha hali ambapo maana ya kijuujuu ya maneno husika, imepewa umuhimu na hivyo kutumiwa katika tungo hizo isivyostahili. Tukichukua neno **amekalia** katika tungo (100a), tunaona kuwa limehamishwa kutoka mazingira ya kawaida ambapo linamaanisha kuweka makalio juu ya kitu; keti (TUKI, 1981), na kutumiwa katika muktadha tofauti. Tungo hizo zinaweza kusahihishwa ifuatavyo:

100b... amechukua tena wadhifa wa urais ....

101b... viwanda vinaporomoka kila siku

102b... Askofu mkuu Ndingi alisema baadhi yao wameelekezewa kidole kwa kuwapa wahalifu bunduki zao....

4.3.4 Kutohoa maneno pasipo haja

Utohoaji ni mfanyiko wa kifonolojia ambapo neno linakopwa kutoka lugha moja na kuendelezwa kwa kufuata utaratibu unaokubalika katika lugha kopaji. Ingawa mbinu hii ya uundaji wa maneno inakubalika katika lugha mbalimbali ulimwenguni, ni muhimu kusisitiza hapa kwamba, uhuru wa utohoaji unaongozwa na haja ya kimatumizi iliyopo. Hivyo basi, utohozi wa maneno kurejelea dhana ambazo tayari zina msamiati asilia unaotumika katika lugha husika, ni hatua isiyohitajika. Katika baadhi ya makala ya GTL tuliyoyazamia, tuligundua matumizi ya maneno yaliyotoholewa pasipo na haja ya kufanya hivyo. Mifano ifuatayo inaonyesha kasoro hiyo.

103a.* ... majaji wengi wanawake na wabunge ni madivosii .... [103]

104a.*... bodi ya ushauri .... [104]

105a.* ... tairi .... [105]

Katika mifano hii mitatu (103a, 104a na 105a), maneno yaliyopigiwa mistari yametoholewa. Hata hivyo, tunashikilia kwamba utohozi huo umefanywa pasipo na haja kwa kuwa tuna maneno mengine katika Kiswahili ambayo yangetumiwa ili kuwasilisha ujumbe uo huo. Kauli hizo zinaweza kusahihishwa kupitia kwa matumizi ya maneno asilia ya

Kiswahili hivi:

103b.... majaji wengi wanawake na wabunge ni watalaka....

104b.... halmashauri ....

105b.... gurudumu....


(Kwa mifano zaidi ya kasoro katika matumizi ya msamiati,rejelea kiambatisho C na D).

Kwa kutumia jedwali nambari 12 na grafu B, tumeonyesha umara-tokezi wa makosa yalivyodhihirika katika vipengele mbalimbali ambavyo tumevishughulikia katika sehemu hii.

Jedwali 13: Msambao wa makosa yahusuyo msamiati

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Matumizi ya maneno yasiyofaa	85	50
Matumizi ya maneno ya Jozi Bainifu isivyostahiki	16	10
Matumizi ya maneno yenye maana finyu	55	32
Maneno yaliyotoholewa pasipo na haja	14	8
Jumla	170	100

Asili:Takwimu za utafiti wetu, 2004



Grafu B: Makosa katika vipengele mbalimbali vya msamiati

Ufunguo

Mmy - Matumizi ya maneno yasiyofaa

Mjbi - Matumizi ya maneno ya Jozi Bainifu isivyostahiki

Mmymf – Matumizi ya maneno yenye maana finyu

Takwimu zinazotokea katika jedwali nambari 12 na grafu B, zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya makosa yahusuyo msamiati, yalitokana na matumizi ya maneno yasiyofaa. Kipengele hiki kilichangia makosa asili mia hamsini (50%); kikifuatiwa na kile cha matumizi ya maneno yenye maana finyu, asili mia thelathini na mbili (32%). Vipengele viwili vilivyosalia vilichangia kiasi kidogo sana cha makosa – matumizi ya maneno ya Jozi Bainifu isivyostahiki (asili mia tisa), na maneno yaliyotoholewa pasipo na haja (asili mia nane). Hivyo basi, ni wazi kuwa kuna haja ya waandishi kumakinika zaidi katika matumizi yao ya msamiati hususan wakizingatia vipengele hivyo ambavyo vilichangia idadi kubwa ya makosa.

4.4 Methali na Nahau

4.4.1 Methali

Kwa mujibu wa TUKI (1981), methali ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kisanii kwa njia ya kufumba na kupigia mfano ambacho kinachukua maana ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Fasili hii inaweka wazi umbo la methali na uamilifu wake katika mazungumzo au uandishi. Ili matumizi ya methali kuwa sahihi, inamlazimu mtumiaji kuelewa maana yake ya ndani kwa uhakika. Kama zilivyo aina zingine za lugha ya kitamathali, methali huhitaji kueleweka vizuri kwa mtumaji ujumbe na mpokeaji ujumbe ili maana iliyonuiwa kufasiriwa kisahihi (Kiai, 1996). Jambo hili linaweka wazi haja ya matumizi ya methali kuegemezwa kwenye ujuzi wa wahusika katika mawasiliano. Utafiti wetu umechanganua matumizi ya methali katika makala ya GTL na kudondoa mifano inayobainisha kasoro zilizojitokeza katika kipengele hicho. Makosa hayo yaliyogunduliwa katika matumizi ya methali, ndiyo tunayoyajadili katika sehemu hii inayofuata.

4.4.1.1 Methali kutoafiki muktadha

Mazingira ambamo methali hutumiwa ni muhimu katika uwasilishaji wa habari inayokusudiwa. Endapo methali fulani itatumiwa bila maana yake ya ndani kueleweka, basi matokeo yake huwa ukosefu wa ufaafu. Matumizi ya methali katika muktadha usiofaa, yalijitokeza katika baadhi ya makala tuliyoyachungua. Methali zilizotumiwa kimakosa zinabainika katika mifano ifuatayo:

106a * Walipomaliza masomo yao na kupata kazi, walilowea mjini wakamsahau mama yao. Ama kweli, sahau ni dawa ya waja ….[106]

107a * ...Uhuru amepigania kiti cha Gatundu kusini mara mbili bila kufaulu, Wakenya walimaizi kuwa mcheza kwao hutuzwa, asipotuzwa hushangiliwa ....[107]

108a * ... Ole wako basi. Jihadhari sana kwani utakapojaribu, utakiona. Nitajua tu, pale mbiu za mgambo zitakapolia kutakuwa na jambo." [108]

Methali hizo tatu zilizopigiwa mistari haziambatani na miktadha hiyo zilimotumiwa. Tukichukua mfano (106a), **sahau ni dawa ya waja** ni methali ambayo hutumiwa kusisitiza umuhimu wa kusamehe na kusahau mabaya uliyotendewa. Hivyo basi, ni wazi kuwa methali hiyo haikufaa kutumiwa katika muktadha ilimotumiwa. Aidha, katika mfano (107a), **mcheza kwao hutuzwa** ni methali inayomaanisha kuwa, mtu huthaminiwa na hata kusaidiwa mahali anapojulikana. Hali inayoelezewa katika muktadha ambamo methali hiyo imetumika, inaonyesha kuwa mhusika hakuthaminiwa wala kusaidiwa ingawa aliwania kiti cha ubunge katika eneo alikozaliwa. Matokeo ya uchaguzi huo, yalidhihirisha kinyume cha methali hiyo iliyotumiwa. Tukirejelea mifano (108a), methali **mbiu ya mgambo ikilia ina jambo**, hutumiwa kuelezea kuwa litukiapo jambo fulani, huwa ni ishara inayoelekeza wahusika kwenye tukio lingine ambalo aghalabu huwa kubwa. Tunashilikia kuwa methali hii haifai tukizingatia muktadha ilimotumika kwani msemaji anatahadharisha mtu fulani kwamba asipotahadhari, atakuja kujuta. Tahadhari ya aina hii ingefaa itolewe kwa matumizi ya methali kama vile, majuto ni mjukuu, huja baadaye.

4.4.1.2 Urundikaji wa Methali

Methali kama pambo la lugha, hutakiwa kutumiwa kwa kiasi ili kuleta taathira inayokusudiwa. Matumizi ya methali zaidi ya moja kuelezea jambo moja, ndiyo tunayorejelea kama urundikaji katika tasnifu hii. Uchunguzi wetu ulikumbana na hali ambapo methali zaidi ya moja zimetumiwa pamoja pasipo na haja kwani moja tu ingetosheleza jukumu la kusisitiza jambo lililokuwa likishughulikiwa. Kasoro hii inathibitishwa na mifano ifuatayo ambayo tumeidondoa kutokana na makala tuliyoyazamia.

109a * Hebu tanzukieni na uneni kuwa kumzaa mwana si kazi, kazi ni kumlea. Aidha kumvua nubi si kazi, kazi ni magawioni. [109]

110a * Wahenga walisema,"Ajuaye hakawi" na pia "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" na "atakaye cha mvunguni sharti kuinama...." [110]

111a * Hatimaye, hayawani hao wakahisi kwamba ngoja ngoja huumiza matumbo na chelewa chelewa utamkuta mwana asiye wako ....[111]

Katika mifano hii mitatu, methali zilizotumiwa zimepigiwa mistari. Tukitazama mifano (109a) na (111a), watumizi wametumia methali mbilimbili ambazo zina maana sawa. Kulikuwa na uwezekano wa kutumia methali moja moja ili kutosheleza haja ya mawasiliano yaliyokusudiwa. Kudondoshwa kwa methali ya kwanza au ya pili katika mifano hiyo hakutaathiri habari inayowasilishwa kwa vyovyote vile. Kwa upande mwingine, ingawa methali tatu zilizotumiwa katika mifano (110a) zina maana tofauti, uelewekaji wa ujumbe ungeimarishwa zaidi endapo mtunzi angetumia methali moja kwa wakati mmoja. Hali hii inatokana na ukweli kwamba methali hizo tatu zinawasilisha dhana tofauti, hatua inayopelekea kuvurugika kwa habari iliyonuiwa na mwandishi.

4.4.1.3 Ubadilishaji wa maneno asilia ya methali

Maneno yatumiwayo katika methali mbalimbali hulenga kuwasilisha habari maalumu na kwa njia fiche. Hatua ya kubadilisha baadhi ya maneno yanayojitokeza katika methali asilia, hupelekea upotoshaji wa ujumbe. Katika kiwango hiki, makosa yaliyogunduliwa yamedhihirika katika mifano hii:

112a.* ... kusahau msemo "raha mbele, mauti nyuma ...." [112]

113a.* ... cha kunuka hasikii udi .... [113]

Maneno yaliyopigiwa mistari katika methali hizi, yamechukua nafasi za maneno asilia na hivyo kutatiza maana iliyokusudiwa. Methali hizo zinaweza kusahihishwa kwa kutumia maneno asilia kama inavyojitokeza hapa:

112b. ... kusahau msemo, "tamaa mbele, mauti nyuma...."

113b. ...cha kunuka hakina udi ....

Ni muhimu kutaja hapa kwamba, methali " Cha kunuka hakina udi," haitumiwi sana siku hizi kwani nafasi yake imechukuliwa na methali, "La kuvunda halina ubani."

Kama hatua ya kulinganisha idadi ya makosa yaliyotokea katika kila kipengele kilichoshughulikiwa katika sehemu hii, tumetumia jedwali nambari 14.

Jedwali 14: Makosa katika vipengele vinavyohusu matumizi ya methali

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Methali kutoafiki muktadha	7	44
Urundikaji wa methali	7	44
Ubadilishaji wa maneno asilia ya methali	2	12
Jumla	16	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa makosa yaliyojitokeza kutokana na methali kutoafiki muktadha yalikuwa sawa kiidadi na yale yaliyotokana na urundikaji wa methali – kila kipengele kilichangia asili mia arobaini na nne (44%) ya jumla ya makosa. Kipengele cha ubadilishaji wa maneno asilia ya methali kilikuwa na idadi ndogo ya makosa ambayo ilichangia asili mia kumi na mbili (12%). Jedwali nambari 14, limeweka wazi sehemu zinazopaswa kusisitizwa na waandishi wa makala ya GTL, katika juhudi za kutumia methali ifaavyo. Sehemu hizo ni zile ambazo zimeathiriwa zaidi na makosa yaliyotokea.

4.4.2 Nahau

Nahau ni fungu la maneno ambayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ya kuonekana wazi (TUKI, 1981). Ufafanuzi huu unasisitiza kuwa nahau huvyaza maana iliyofichika. Hivyo ni muhimu kutumia umbo hili kisahihi kwa lengo la kuweka wazi ujumbe unaowasilishwa. Katika kazi hii, tumeangazia matumizi ya nahau kimakosa katika matini tuliyochanganua. Baadhi ya makosa yaliyojitokeza katika kipengele hiki ni haya yafuat

4.4.2.1 Matumizi ya nahau isivyofaa

Kufanikiwa katika matumizi sahihi ya nahau kunategemea ujuzi wa mwandishi husika kuhusu maana ya nahau anazonuia kutumia. Iwapo mwandishi atatumia umbo hili mahali pasipofaa katika tungo zake, basi matini inayoandikwa itakuwa pungufu. Kasoro katika kiwango hiki zilidhihirika katika makala tuliyochunguza inavyothibitishwa na mifano hii:

114a.* Kuchuma riziki kulikuwa kwa <u>shingo upande</u> siku hii apate siku nyingine akose .... [114]

115a.* Asili mia zote 11, 12 na 15, wafanyakazi hawa wote hawafai <u>kuambulia nunge</u> pasina kupewa maelezo sahihi .... [115]

116a.* ... zingenufaika na nyongeza hizo ila tu kuelezewa kuwa asili mia hizo haziwahusu <u>ndewe wala sikio</u> .... [116]

Katika mfano (114a), **shingo upande**, ni nahau ambayo inamaanisha bila kupenda. Tukizingatia maana hii, ni wazi kuwa matumizi yake katika sentensi hiyo yana dosari kwa kuwa kinachomaanishwa ni ile hali ya kufanikiwa kupata riziki siku moja na kukosa siku nyingine. Matumizi ya nahau hii katika muktadha husika yanaleta utata katika ujumbe unaopitishwa. Nahau hii yaweza kutumiwa hivi katika sentensi: *Yohana alikubali <u>shingo upande</u> kutumwa dukani na mamake.* Mfano (115a) na (116a), inahusisha nahau **kuambulia nunge** na **ndewe wala sikio** kwa mfuatano huo, bila kuzingatia muktadha. **Kuambulia**

nunge, ni nahau inayotumiwa kwa maana ya kutopata chochote ilhali sentensi hiyo inaelekea kuonyesha kuwa wafanyakazi husika walipata asili mia 11, 12 na 15. Mfano wa matumizi wa nahau hiyo ni: *Fatuma aliambulia nunge katika mtihani wake*. Kwa upande wa nahau **ndewe wala sikio,** kwa kawaida hutumiwa kueleza hali ya jambo kutomhusu mtu na wala siyo kitu anachopata kama vile asili mia ya nyongeza fulani. Kwa hivyo, nahau hiyo haikutumika kisahihi kwa kuwa imetumiwa kuelezea asili mia inayozungumziwa isivyowahusu watu husika. Matumizi sahihi ya nahau hii yanadhihirika katika mfano huu wa sentensi:
Mambo aliyoambiwa mwanafunzi huyo hayakumhusu ndewe wala sikio

4.4.2.2 Kubadilishwa kwa umbo/neno asilia la nahau

Msingi wa matumizi sahihi ya nahau anuwai, ni kuzingatia umbo na maneno yake asilia. Katika uchunguzi wetu, tuligundua kuwa baadhi ya nahau ama zimebadilishwa kiumbo au maneno fulani yamechukua nafasi ya yale asilia. Tumedondoa mifano ifuatayo kuthibitishia kasoro hii.

117a * ... kuzungushwa mbuyu .... [117]

118a*... wengine wamekuwa na mguu wa nje.... [118]

119a* ... popote walipo tujikaze moyo ili tuweze angalau kupunguza maovu haya.... [119]

Katika mfano (117a) na (119a), maneno yanayounda nahau yamebadilishwa kiumbo ilhali mfano (118a), unaonyesha nahau ambamo neno moja limebadilishwa. Nahau sahihi zilitakiwa kuwa:

117b. ... kuzunguka mbuyu ....

118b. ... wengine wamekuwa na macho ya nje....

119b. ... popote walipo tukaze moyo ili tuweze angalau kupunguza maovu haya ....

Umara-tokezi wa makosa yaliyobainika katika kiwango cha matumizi ya nahau, umeonyeshwa katika jedwali nambari 15. Ulinganisho wa makosa hayo kiidadi katika vipengele viwili vilivyoshugulikiwa katika sehemu hii, umedhihirika.

Jedwali 15: Makosa yaliyotokeza katika matumizi ya nahau

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Matumizi ya nahau isivyofaa	7	64
Kubadilishwa kwa umbo / neno asilia la nahau	4	36
Jumla	11	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Ni bayana kutokana na takwimu hizi kwamba, kipengele cha matumizi ya nahauisivyofaa, ndicho kimesababisha idadi kubwa ya makosa kikilinganishwa na kile cha kubadilishwa kwa umbo / neno asilia la nahau. Kipengele cha kwanza kimechangia asili mia sitini na nne (64%) ya makosa yote yaliyotokeza ilhali kasoro zilizotokana na hicho cha pili ni asili mia thelathini na sita (36%). Hali hii huenda imesababishwa na ukosefu wa ujuzi wa kutumia nahau mbalimbali kwa kuzingatia muktadha miongoni mwa baadhi ya waandishi wa makala yaliyochanganuliwa.

4.5 Tamathali za Usemi

Lugha ya kitamathali huleta taswira akilini mwa msomaji kupitia kwa ulinganisho wa kitu kisichozoeleka na kingine ambacho kimezoeleka (Wyrick, 1987). Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa tamathali za usemi humsaidia mwandishi kuwasilisha maneno yake kwa njia yenye ueledi, mashiko na iktisadi na hivyo kupelekea habari kukumbukwa zaidi. Hali hii hutokea tu iwapo mwandishi atavyaza taswira ambayo ina mnato. Wyrick (ibid), anaelekeza kuwa tamathali za usemi zapaswa kutumiwa kwa kiasi ili zisipoteze ladha. Ni muhimu kukumbuka kwamba lugha ya kitamathali haipaswi kutumiwa kuipamba kazi tu, bali kumsaidia mwandishi kuyajenga mawazo yake na kuweka wazi maana iliyokusudiwa kwa msomaji (Rosa na wenziwe, 1982). Maelezo ya wataalamu hawa yanaonyesha namna bora ya kutumia tamathali za usemi ili kuimarisha mawasiliano husika. Uchanganuzi wetu wa makala ya GTL, umeonyesha kwamba baadhi ya TZU hazikutumiwa kisahihi, hali iliyopelekea ujumbe kukwazwa. Makosa yaliyobainika katika kipengele hiki ndiyo tunayoyashughulikia katika sehemu inayofuata.

4.5.1 Matumizi ya TZU isivyostahiki

Katika kufikia hatua ya matumizi sahihi ya TZU, inamlazimu mwandishi kuelewa kwa kina umbo analonuia kulitumia katika kazi yake. Upungufu uliojitokeza hapa huenda ulitokana na ama waandishi kutoyaelewa maumbo husika kikamilifu au kuzua ulinganisho

finyu. Tungo zifuatazo zinadhihirisha kasoro zilizojitokeza katika kiwango hiki.

120a. * ... vichwa vyao ni vigumu mithili ya Abeli na Kaini nyakati za Adamu na Hawa ....[120]

121a. * Huduma aliyokuwa akiwatolea wateja ilikuwa ya haraka na ya ari mithili ya mchwa ....[121]

122a. * ... wengi wao hufikiri maisha ya abiria ni kama ya mbuzi ....[122]

Katika mifano hii mitatu, tashbihi zilizotumiwa zimepigiwa mistari. Ulinganisho unaojitokeza katika tungo hizo una dosari mbalimbali. Matumizi ya wahusika waliotajwa katika mfano (120a), yanazua utata kwani yaelekea kutoa tuhuma zisizoungwa mkono na ushahidi wowote katika Biblia ambayo ndiyo chanzo chake. Matokeo ya matumizi haya ni upotoshaji wa ujumbe unaonuiwa kupitishwa. Tukiangalia mfano (121a), maneno **haraka** na **ari** ambayo yametumiwa katika ulinganisho huo yana maana zinazotofautiana. Ni wazi kwamba neno haraka linapinga hali inayotakiwa kudhihirishwa na tashbihi hiyo kwani mchwa wana ari lakini mwendo wao siyo wa haraka. Hivyo basi, udondoshaji wa neno **haraka** kutoka kwa tashbihi hiyo, utapelekea ulinganisho uliokusudiwa kuwa wazi na wa kueleweka. Katika mfano (122a), maisha ya abiria yanapolinganishwa na yale ya mbuzi, ujumbe unaosisitizwa hauonekani wazi. Hali hii inasababishwa na mtazamo kwamba hata maisha ya mbuzi ni ya thamani hususan kwa mfugaji wake. Ulinganisho ambao ungefaa ni ule ambao pengine ungehusisha viumbe duni zaidi kuliko mbuzi na ambavyo havina thamani kwa mwanadamu.

4.5.2 Urundikaji wa TZU

Sehemu zingine za makala tuliyoyapitia, zilibainisha matumizi ya TZU zaidi ya moja katika mahali pamoja. Matumizi ya aina tofauti za TZU yalijitokeza kama hatua ya kusisitiza jambo moja ilhali kwingineko aina moja ya TZU, ilitumiwa zaidi ya mara moja pasipo na haja. Tumedondoa mifano ifuatayo kuthibitishia kuwepo kwa kasoro hizo katika matini husika.

123a* Sababu zilizonifanya nitoroke ni nyingi kama mchanga wa bahari au nyota za angani....[123]

124a*... alianza kulia kwa kwi kwi, na baadaye machozi yakaanza kumtiririka tiriri – njia mbili mbili....[124]

125a* Wengi wa watawaliwa huwa hawaambiwi, hawasemezeki, hawaliki, hawatafuniki....[125].

TZU zilizotumika katika mifano hiyo mitatu, zimerudufishwa na kupelekea kupungua kwa ubora wake. Tukiangalia mfano (123a), tashbihi mbili zilizotumiwa zinaleta maana sawa. Hakukuwa na haja kwa mwandishi kuzitumia pamoja ilhali moja ingetekeleza jukumu la ulinganisho uliokusudiwa kikamilifu. Hali ya marudio ya TZU kama hayo yamejitokeza katika mfano (124a), ambapo tanakali za sauti zaidi ya moja zinaelezea jambo moja ambalo lingeweza kuwekwa wazi kupitia kwa tanakali ya sauti moja tu au mbili.Aidha, katika mfano (125a), takriri mbili zimetumiwa ilhali moja ingetosheleza haja. Matumizi sahihi ya TZU katika mifano hiyo ni tatu (123a, 124a na 125a) yatakuwa:

123b. Sababu zilizonifanya nitoroke ni nyingi kama mchanga wa bahari ....

Au

Sababu zilizonifanya nitoroke ni nyingi kama nyota za angani.

124b... alianza kulia kwa kwi kwi, na baadaye machozi yakaanza kumtiririka tiriri.

Au

... alianza kulia kwa kwi kwi, na baadaye machozi yakaanza kumtoka njia mbilimbili....

125b. Wengi wa watawaliwa huwa hawaambiwi, hawasemezeki....

Au

Wengi wa watawaliwa huwa hawaliki, hawatafuniki....

Tumeweka bayana umara-tokezi wa makosa yahusuyo tamathali za usemi kwa mujibu wa vipengele viwili tulivyovishughulikia, kupitia kwa jedwali nambari 16 linalofuata.

Jedwali 16: Makosa yahusuyo matumizi ya tamathali za usemi

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Matumizi ya TZU isivyostahiki	9	69
Urundikaji wa TZU	4	31
Jumla	13	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

Inavyodhihirika katika jedwali nambari 16, makosa mengi katika kiwango hiki yalitokana na matumizi ya TZU isivyostahiki. Kipengele hiki kilisababisha asili mia sitini na tisa (69%) ya makosa yote yaliyohusu matumizi ya TZU. Urundikaji wa TZU ulichangia asili mia thelathini na moja (31%) ya kasoro zilizogunduliwa katika utafiti wetu. Takwimu hizi

zinaonyesha kuwa uelewa wa maana ya TZU anuwai ni muhimu kwa waandishi katika juhudi zao za kuandika makala yenye mvuto kwa wasomaji wao.


4.6 Muhtasari wa matokeo

Kutokana na utafiti huu, tumegundua kuwa kuna makosa yanayojitokeza katika maumbo mbalimbali ya lugha kwa mujibu wa makala teule ya GTL. Imedhihirika kuwa kipengele cha sarufi ndicho kilichoathiriwa zaidi kwani kilikuwa na idadi kubwa sana ya makosa. Matokeo haya huenda yametokana na ukweli kwamba, sarufi ndiyo msingi wa lugha yoyote ile ikiwemo Kiswahili na uchanganuzi wake hutanda kotekote katika matini. Makala yote yaliyoteuliwa kwa uchanganuzi yalibainisha kasoro katika kipengele hiki. Msamiati ulikuwa na makosa kiasi kwa kuwa uchanganuzi wake ulihusu maneno mahsusi yalivyotumiwa katika kuwasilishia ujumbe. Hatimaye, methali, nahau na tamathali za usemi ndivyo vipengele vilivyokuwa na makosa machache kabisa. Hali hii huenda ilitokana na matumizi ya vipengele husika katika makala machache miongoni mwa yale yaliyochanganuliwa. Maumbo hayo yalijitokeza katika makala ya hadithi na kwa kiasi kidogo katika makala ya barua / sauti ya wasomaji. Aidha, imebainika kuwa kati ya maumbo yote ya lugha tuliyoyachunguza, hayo maumbo matatu yalitumiwa kwa makini zaidi katika makala husika na hivyo kusababisha kasoro chache. Umara-tokezi wa makosa katika vipengele vya lugha tulivyovichunguza yamedhihirishwa katika jedwali nambari 17 na grafu C.

Jedwali 17: Makosa katika vipengele anuwai vya lugha vilivyoshughulikiwa

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Sarufi	825	80
Msamiati	170	16
Methali na Nahau	27	3
Tamathali za usemi	13	1
Jumla	1035	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004



Grafu C: Makosa katika vipengele mbalimbali vilivyoshughulikiwa

Ufunguo

S - Sarufi

M - Msamiati

Mn -Methali na Nahau

Tzu -Tamathali za usemi

Kwa ujumla, inavyobainika kutokana na jedwali nambari 17 na grafu C, makosa ya sarufi yalikuwa asili mia themanini (80%) ya jumla ya kasoro zote zilizogunduliwa katika utafiti huu. Makosa ya msamiati yalichangia asili mia kumi na sita (16%) ilhali upungufu katika matumizi ya methali na nahau ulikuwa na asili mia tatu (3%) ya kasoro zote. Kipengele kilichochangia idadi ndogo kabisa ya makosa ni kile cha TZU, ambacho kilikuwa na asili mia moja (1%) pekee.

Hatimaye, kuhusu msambao wa makosa katika makala tuliyoteua kwa ajili ya uchanganuzi wetu, tuligundua kuwa idadi kubwa zaidi ya makosa (48%), ilijitokeza katika makala ya maoni. Makala ya habari kuu yalichangia kasoro (21%); tahariri (20%) na hadithi (11%) ya jumla ya makosa yote yaliyojitokeza. Matokeo haya yamewekwa wazi zaidi katika jedwali nambari 18, linalofuata.

Jedwali 18: Msambao wa makosa katika makala mbalimbali yaliyochanganuliwa

Vipengele	Umara-tokezi	Asili mia
Habari kuu	222	21
Tahariri	202	20
Maoni	497	48
Hadithi	114	11
Jumla	1035	100

Asili: Takwimu za utafiti wetu, 2004

4.7 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha makosa mbalimbali yaliyojitokeza katika makala ya GTL tuliyoyachungua huku tukitoa mifano mahsusi ya kasoro hizo na jinsi ya kuzisahihisha. Tumetambulisha makosa yaliyojitokeza katika maumbo makuu ya lugha tuliyoyachunguza ambayo ni: Sarufi, Msamiati, Methali, Nahau na Tamathali za usemi. Katika kipengele cha sarufi tumeainisha na kujadili makosa yafuatayo: matumizi ya sentensi zisizokamilika, ukosefu wa upatanisho wa kisarufi; mnyambuliko usiofaa wa maneno; kasoro za kitahajia; uakifishi pungufu; matumizi yasiyofaa ya vihusishi; matumizi mapungufu ya viunganishi na kuwepo kwa miundo changamano. Kwa upande wa msamiati, tumeyashughulikia makosa mbalimbali yaliyojitokeza ambayo ni pamoja na: matumizi ya maneno yasiyofaa; matumizi ya maneno ya jozi bainifu isivyostahiki; matumizi ya maneno yenye maana finyu na utohoaji wa maneno pasipo haja. Kasoro tulizozichanganua kwa mujibu wa methali ni: methali kutoafiki muktadha; urundikaji wa methali na ubadilishaji wa maneno asilia ya methali. Aidha, tumeeleza kuhusu matumizi ya nahau isivyofaa na kubadilishwa kwa umbo/neno asilia la nahau, kama kasoro zilizobainika katika kipengele cha nahau. Mwishoni, tumeyajadili makosa yaliyojitokeza katika kipengele cha tamathali za usemi katika viwango viwili: kwanza, matumizi ya TZU isivyostahiki na pili, urundikaji wa TZU. Katika juhudi za kuonyesha na kulinganisha idadi ya makosa yaliyotokea katika kila kiwango, tumetumia msambao wa umara-tokezi.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imejihusisha na muhtasari wa tasnifu yetu kwa kumulika malengo na makisio ya uchunguzi huu. Tumejadili namna tulivyotimiza madhumuni ya utafiti na pia kuthibitisha makisio yaliyoiongoza kazi hii. Mwishoni tumeonyesha vikwazo vilivyotukumba na kutoa mapendekezo anuwai kwa mujibu wa mambo yaliyoibuka kutokana na uchunguzi wetu.

5.2 Hitimisho.

5.2.1 Malengo na makisio ya utafiti.

Katika utafiti huu tumechunguza swala la matumizi ya lugha katika gazeti la *Taifa Leo*. Malengo ya uchunguzi huu yalikuwa:

Kwanza, kuchunguza kasoro za kimsamiati zilizojitokeza katika makala yaliyoteuliwa ya GTL. Msamiati uliotumika isivyostahili kulingana na kanuni za lugha sanifu ya Kiswahili umedondolewa na usahihi wake ukaonyeshwa kwa kuzingatia muktadha husika.

Mbali na msamiati, utafiti huu ulinuia kutathmini namna tamathali za usemi, zinavyotumiwa katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL. Katika kipengele hiki, mawazo ya wataalamu wa lugha kuhusu umbo hili la lugha yamezingatiwa katika harakati za kutoa kauli zenye mashiko juu ya matumizi yasiyofaa ya TZU.

Aidha, tulilenga kubainisha matumizi yasiyofaa ya methali na nahau katika baadhi ya makala ya GTL. Maumbo haya mawili ni muhimu katika uwasilishaji habari katika miktadha kadha wa kadha, ukiwemo huu wa uandishi wa makala katika gazeti hili. Mazingira ya matumizi ya methali na nahau yamepewa umuhimu wa kipekee katika kupima ufaafu wa maumbo haya na kinyume chake.

Isitoshe, uchunguzi huu ulidhamiria kutambulisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL. Katika tasnifu hii, tumedondoa makosa yanayojitokeza katika makala yaliyoteuliwa kwa kuzingatia kanuni za kisarufi za Kiswahili sanifu kama mwongozo wa kutimizia jukumu hili.

Tuliteua makala ya kuchanganuliwa kutokana na jumla ya yale yachapishwayo katika gazeti husika ili kufanikisha malengo yetu. Makala tuliyoyateua ni: habari kuu, tahariri na maoni, na hadithi. Tumetimiza madhumuni ya kazi hii kwa kuzamia vipengele vya lugha vilivyolengwa, ambavyo ni: sarufi, msamiati, methali, nahau, na tamathali za usemi.

Uchunguzi wetu uliongozwa na makisio yafuatayo ambayo tuliyaibua kutokana na malengo ya tasnifu hii.

i). Baadhi ya msamiati unaotumika katika baadhi ya makala katika GTL ni mpungufu.

ii). Baadhi ya TZU hazitumiwi inavyostahiki katika baadhi ya makala ya GTL.

iii). Baadhi ya methali na nahau hazitumiwi ipasavyo katika uandishi wa makala katika GTL.

iv). Kanuni za kisarufi zinakiukwa katika uandishi wa baadhi ya makala katika GTL.

Makisio yote ya utafiti huu yamethibitishwa. Kuhusu sarufi, imedhihirika kuwa kanuni za kisarufi zilikiukwa katika makala tuliyoyazamia. Tuligundua makosa katika vipengele mbalimbali vya sarufi ambayo yamechangia katika kuvurugika kwa ujumbe uliowasilishwa na makala husika. Kama anavyosema, Mbaabu (1995), sababu ya kuwa na lugha sanifu ni kurahisisha mawasiliano katika mazumgumzo na maandishi pia. Ugunduzi wetu kuhusu kutozingatiwa kwa sheria za kisarufi katika matini tuliyochanganua ni ushahidi kuwa mawasiliano yaliyokusudiwa huenda yalitingwa. Kasoro zilijitokeza katika ukamilifu wa sentensi, upatanisho wa kisarufi, mnyambuliko wa vitenzi, mpangilio wa maneno katika sentensi, tahajia, uakifishaji, viambishi, kujirudia katika sentensi, vihusishi, viunganishi na miundo changamano. Makosa yote yaliyojitokeza, tumeyaainisha na kuyajadili katika sura ya nne ya tasnifu hii.

Katika kipengele cha msamiati, utafiti huu umebainisha upungufu ulioonekana katika uteuzi wa maneno. Matumizi ya maneno yasiyoambatana na muktadha wa kimatumizi yalisababisha kasoro nyingi katika makala mbalimbali yaliyochunguzwa kwa kuchangia asili mia hamsini ya jumla ya makosa katika kiwango hicho. Hapa tunasisitiza kuwa iwapo ujumbe unatarajiwa kueleweka kikamilifu inamlazimu mwasilishaji kuteua maneno anayotumia kwa makini. Uteuzi sahihi wa maneno ni jambo linalowashughulisha wataalamu mbalimbali wa lugha kama vile, Wyrick (1987), ambaye anasisitiza kuwa ili kuepuka matumizi ya maneno tata, mtumiaji anapaswa kutumia maneno ambayo anafahamu maana na matumizi yake. Mbali na matumizi ya maneno yasiyoambatana na muktadha, tumebainisha pia jinsi maneno ya jozi bainifu, yalivyotumiwa isivyostahiki na kusababisha asili mia tisa ya

makosa; kutumiwa kwa maneno yenye maana finyu, asili mia thelathini na mbili ilhali kutoholewa kwa baadhi ya maneno pasipo na haja kukachangia asili mia nane ya makosa. Hali hizi mbalimbali zimechangia katika kuonyesha kuwa msamiati uliotumiwa katika makala teule ya GTL, ulikuwa pungufu.

Katika kuchunguza matumizi ya methali na nahau kwa mujibu wa makala yachapishwayo katika GTL, tumebainisha makosa yaliyojitokeza. Kuhusu methali, kasoro nyingi ziligunduliwa katika viwango vya methali kutoafiki muktadha na urundikaji wake katika baadhi ya sehemu za makala husika. Matokeo ya kutotumiwa kwa umbo hili kikamilifu yalikuwa kupotoshwa kwa habari iliyokusudiwa. Kwa upande mwingine, kosa la urundikaji wa methali lilipelekea hali ambapo umbo hili lilidhihirika katika sehemu chache za makala huku zingine zikiwa kavu. Kwa maoni yetu, ufaafu wa kimatumizi wa methali ni kiungo muhimu katika uwasilishaji wa habari. Aidha, katika uchunguzi wetu, imedhihirika kuwa matumizi ya nahau katika matini iliyochanganuliwa, yalikuwa na kasoro anuwai. Matumizi ya nahau isivyofaa na kubadilishwa kwa umbo/ neno asilia la nahau ndivyo viwango viwili vilivyosababisha upungufu katika kipengele hiki. Maumbo haya ya lugha (methali na nahau), huchukua nafasi muhimu katika mawasiliano ambapo yanatekeleza jukumu la kuweka wazi mawazo yanayopitishwa na hivyo, kuna haja ya watumizi kumakinika wanapoyahusisha katika kazi zao.

Fauka ya hayo, uchunguzi wetu ulizamia matumizi ya tamathali za usemi katika makala husika. Tumeonyesha kuwa TZU zingine zimetumiwa kwa njia yenye kasoro na hivyo kukosa kutimiza uamilifu wake katika uandishi. Kilichojitokeza wazi ni kuwa makosa mengi yahusuyo umbo hili la lugha yalitokana na matumizi yake isivyostahiki. Hali hii ilionyesha kuwa watumizi wa TZU, walitumia umbo hili bila kuwa na uhakika kuhusu matumizi sahihi ya vipengele husika. Aidha, ilielekea kuwa ni aina chache sana za TZU zilizotumika huku zingine zikipuuzwa. Tulikumbana na tashbihi, takriri na tanakali za sauti katika matini tuliyoyachanganua huku aina zingine za TZU zikitumiwa kwa tukizi tu. Ugunduzi huu ni muhimu kwani unatoa mwanga kuhusu mwegemeo wa waandishi katika matumizi yao ya TZU katika makala ya GTL na haja iliyopo ya kuchanganya aina mbalimbali za TZU ili kuleta mvuto zaidi katika uwasilishaji wao wa habari.

Imedhihirika kutokana na utafiti huu, kwamba idadi ya makosa katika kiwango cha sarufi ilikuwa kubwa sana inapolinganishwa na ile iliyotokea katika viwango vingine vilivyochunguzwa mathalan msamiati, methali, nahau na tamathali za usemi. Ingawa ni wazi kuwa sarufi ndicho kipengele ambacho uchanganuzi wake umetanda kote katika makala yote tuliyoteua kwa ajili ya uchunguzi wetu, hii huenda isiwe sababu ya kipekee iliyopelekea

kugunduliwa kwa kasoro nyingi za kisarufi katika matini husika. Ukosefu wa makini ulibainika katika kiwango hicho kwani makosa mengine yaliyotokea yalikuwa madogo na ya kawaida sana kiasi kwamba tunaamini, yangeweza kurekebishwa iwapo makala hayo yangehaririwa kwa uangalifu. Kwa upande mwingine, kasoro zilizohusu methali, nahau na tamathali za usemi zilikuwa chache mno. Matokeo haya huenda yalisababishwa na hali kwamba, maumbo hayo yalijitokeza katika makala chache sana mathalan maoni na hadithi. Makala ya habari kuu na tahariri hayakuonyesha matumizi yoyote ya maumbo hayo na hivyo kupunguza umara-tokezi wake katika uchanganuzi wetu. Aidha, makala ya hadithi yalielekea kuandikwa kwa utaalam mkubwa, na hivyo kupelekea kiasi kidogo cha makosa kugunduliwa humo.

Kupitia kwa uchanganuzi wa makosa ambayo yamejitokeza katika makala teule ya GTL, tumegundua kuwa makala ya maoni yaliibuka na kasoro nyingi kuliko makala mengineyo. Hali hii huenda ilisababishwa na kuchapishwa kwa makala hayo moja kwa moja vile yalivyopokelewa kutoka kwa wanamaoni mbalimbali. Ni muhimu kutaja kwamba, makala hayo yanahitaji kuhaririwa kwa makini kwa kuwa yanayotokea humo huenda yakawapotosha wasomaji hasa ikiwa lugha inayotumiwa ina upungufu mkubwa. Makala haya kwa kawaida hutokea katika ukurasa mmoja na tahariri ambayo huonyesha sera rasmi ya gazeti husika, hali inayotilia nguvu haja ya uangalifu mkubwa kuelekezwa kwayo. Hatua hii itapelekea kugunduliwa kwa upungufu na kurekebishwa kabla ya uchapishaji.

Kwa ujumla data tuliyoikusanya imetuwezesha kuthibitisha madai ya Onyango (1990), kuhusu matumizi ya lugha katika magazeti yaandikwayo kwa lugha ya Kiswahili. Mtaalam huyu anaeleza kwamba wasomi wengi hawapendi kuyasoma magazeti husika kutokana na matumizi yake ya lugha yenye upungufu wa ufasaha. Makosa tuliyoyagundua katika viwango mbalimbali vya lugha tulivyovichunguza ni ithibati tosha ya ukweli wa madai hayo.

5.2.2 Vikwazo

Utafiti wetu ulitegemea nakala za gazeti la *Taifa leo* kama chanzo cha data iliyohitajika. Ukosefu wa baadhi ya nakala zilizojumlishwa katika sampuli ya utafiti, ulitukwaza na kucheleweshe shughuli zetu za kukusanya data. Hali hii hasa ilisababishwa na uhifadhi pungufu wa GTL, uliodhihirika katika baadhi ya maktaba ambamo utafiti huu ulifanyiwa. Maktaba zingine hazikuwa na nakala za miaka ya kitambo kidogo ya gazeti hilo na wahusika walithibitisha kuwa GTL limeanza kuhifadhiwa humo katika miaka ya hivi majuzi kabisa. Tulilazimika kutembelea maktaba za umma ili kufidia upungufu huo ingawa

mwanzoni hatukunuia kuzishirikisha katika kazi yetu. Mbali na tatizo hilo la ukosefu wa nakala nyingi, pia tulishuhudia hali ambapo nakala mojamoja zilikosa miongoni mwa zile zilizohifadhiwa pamoja. Matokeo ya kikwazo hiki yalikuwa kubadilisha nakala iliyokwishateuliwa katika sampuli na kuchukua nyingine ambayo ilipatikana. Aidha, kulikuwa na dosari katika uhifadhi wa kijumla wa nakala za gazeti hilo kwani katika maktaba zingine, zilirundikwa pamoja badala ya kupangwa kulingana na vipindi mbalimbali vya uchapishaji. Muda mrefu sana ulitumiwa katika harakati za kutambua na kuweka pamoja nakala zile zilizotakiwa kwa ajili ya uchanganuzi wetu.

Kama hatua ya kuepuka kikwazo hiki katika tafiti zitakazotumia nakala za gazeti wakati wa ukusanyaji wa data, tunapendekeza kuwa juhudi zielekezwe katika uhifadhi kamilifu wa nakala husika. Wanaohusika na kitengo cha maktaba katika taasisi mbalimbali wanahitajika kuhakikisha kuwa, uhifadhi wa magazeti umetekelezwa kwa njia ifaayo. Wanaweza kutimiza jambo hili kwa:

a). Kuhakikisha kuwa nakala za kila siku za magazeti mbalimbali zinahifadhiwa.

b). Kuzitafuta nakala ambazo hazijahifadhiwa kutokana na sababu moja au nyingine na kuzihifadhi.

c). Kuzipanga nakala za magazeti kulingana na vipindi vyao vya uchapishaji na ikiwezekana ziimarishwe ili mara zote ziwe pamoja kwa nia ya kurahisisha kutambuliwa kwake.

d). Kuhifadhi nakala husika kwa mpango maalum badala ya kuzirundika pamoja ili kurahisisha utafutaji wa magazeti hayo panapozuka haja.

5.3 Mapendekezo

Imebainika, kutokana na utafiti huu, kwamba lugha inayotumiwa katika uandishi wa makala anuwai ya GTL ina kasoro. Tunapomulika makosa yaliyotokea katika makala husika hususan yale ya maoni (sauti ya wasomaji na barua), tunapendekeza kuwa, kwanza, uhariri wa kina ufanywe kabla ya uchapishaji. Ni kweli kwamba makala hayo huwakilisha maoni ya wasomaji kuhusu mambo kadha wa kadha. Lakini ni muhimu kukumbusha hapa kwamba, iwapo lugha watumiayo imetawaliwa na dosari za hapa na pale, ni jukumu la wahariri kuipiga msasa ili inapomfikia msomaji iwe katika usahihi wake. Hatua hii ni muhimu hasa tuking'amua kuwa ikiwa lugha yenye dosari itaruhusiwa kupenya na kuifikia hadhira, huenda ikapotosha na kupelekea wasomaji wengine kuiiga na kuisambaza bila kutambua kwamba ni lugha pungufu. Waaidha, makala mengine yote yachapishwayo katika GTL yanapaswa kuhaririwa kwa makini ili kutambua na kuyasahihisha makosa yanayojitokeza kabla ya

kuelekezwa kwenye hatua ya uchapishaji. Kukosolewa kwa waandishi, kusiwavunje moyo bali kuchukuliwe kama changamoto ya kumakinika zaidi kwani mchango wao katika kufanikisha uwasilishaji wa habari ni mtikati katika shughuli nzima ya mawasiliano kupitia kwa vyombo vya habari.

Pili, utafiti wetu, umegundua kuwa maumbo mengine ya lugha yalijitokeza katika makala fulani tu. Maumbo yaliyodhihirisha hali hii ni methali, nahau na tamathali za usemi. Tulipata matumizi yake katika makala ya hadithi na maoni pekee. Kwa kuwa haya ni mapambo muhimu ya lugha, tunapendekeza kuwa waandishi wa makala mengine kama vile tahariri wayashirikishe ili kazi zao zivutie zaidi. Lugha ya mnato kama hiyo huifanya habari husika kuganda akilini mwa msomaji kwa muda mrefu na hivyo kuleta athari inayonuiwa. Makala ya tahariri ambayo kimsingi yana jukumu la kumwelimisha msomaji kuhusu mambo yanayomzunguka katika jamii anamoishi, yanaweza kuboreshwa kupitia kwa matumizi ya maumbo husika.

Tatu, kutokana na utafiti huu, kumeibuka haja ya ushirikishi makini wa taaluma ya uandishi wa habari. Tunapendekeza kuwa vyuo vinavyowafundisha waandishi wa habari, vibuni mikakati imara inayolenga kuimarisha kiwango cha lugha cha wanafunzi wao. Taaluma ya uandishi wa habari yafaa iimarishwe zaidi hususan katika mafunzo yahusuyo matumizi ya lugha katika uandishi wa makala mbalimbali. Isisitizwe kwamba lugha sanifu siyo tu zana muhimu katika kufanikisha mawasiliano bali pia matumizi yake ni hatua ya kuhifadhi taadhima ya taaluma hiyo muhimu katika jamii. Matokeo ya uchunguzi wetu yanaweza kuwafaa katika juhudi za kuainisha vipengele tata katika lugha na hivyo kuvisisitiza katika ufundishaji wao. Makosa halisi yaliyochanganuliwa katika kazi hii, huenda yakawa na umuhimu mkubwa katika kuelekeza kuhusu namna bora ya kuepukana na kasoro ambazo hutokea mara kwa mara katika uandishi wa habari. Katika kiwango hiki tunayaafiki mawazo ya Williams (1985), ambaye anaeleza kuwa mara nyingi chanzo cha uandishi mbaya, ni waandishi kutojifunza jinsi ya kuzua ueledi katika kazi zao, jambo litakalowawezesha kuandika kwa njia isiyozua utata. Anaendelea kusisitiza kuwa huenda waandishi hawa hawakuongozwa vizuri, kuhusu haja ya kuhariri kazi zao ili kuondoa kasoro mbalimbali. Hivyo basi, tunasisitiza kwamba, taaluma ya uandishi wa habari yapaswa kuwaonyesha wanafunzi, mbinu za kuhariri makala wayaandikayo, kwa lengo la kuisarifu lugha yao ili ikubalike katika mawasiliano.

Nne, sera ya lugha nchini Kenya haijakipa Kiswahili hadhi kinachostahili. Ingawa ni kweli kuwa mfumo wa elimu nchini unahimiza matumizi ya Kiswahili na hata kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa, bado Wakenya wengi wana mielekeo hasi kuihusu lugha hii. Mara

nyingi, makosa yatokeayo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili hayachukuliwi kama jambo kubwa kama inavyotokea katika lugha ya Kiingereza. Tunatuhumu kwamba huenda hali hii ndiyo ambayo imejipenyeza katika uandishi wa magazeti ya Kiswahili kiasi kwamba makosa mengi yanaruhusiwa kutokea katika machapisho hayo. Tunapendekeza kuwa sera ya lugha nchini Kenya ipigwe msasa ili lugha ya Kiswahili ipewe nafasi inayostahiki kwa lengo la kuiwezesha itekeleze jukumu lake kama lugha ya taifa. Anavyosema Mbaabu (1995b), kupitia kwa sera yake ya lugha, Kenya imezua hali ambapo mahitaji ya kuiendeleza lugha ya taifa hayajatimizwa. Hivyo basi, wanaobuni sera kuhusu lugha nchini, wanahitaji kuelekeza juhudi zao katika uimarishaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wananchi kwa lengo la kuboresha matumizi yake katika mawasiliano. Tunatumai kuwa, juhudi hizi zitaleta changamoto kwa taaluma zinazojihusisha na matumizi ya lugha ya Kiswahili ikiwemo ile ya uandishi wa habari ili ziimarishe viwango vyao vya lugha.

Kuhusu utafiti zaidi, kwanza, kuna maeneo mbalimbali ambayo yanaweza kuhusishwa. Ni bayana kuwa utafiti wetu umejikita katika kasoro zinazojitokeza katika makala teule ya GTL, hususan katika kipengele cha lugha. Hatukujihusisha kwa kina na sajili zinazotumiwa katika uandishi wa makala anuwai yanayochapishwa katika gazeti hilo. Kwa hivyo utafiti wa kina utakaolenga kuzitambulisha na kuzijadili sajili zinazotumika humo, unahitajika. Utafiti wa aina hii, utaweka wazi matumizi ya lugha katika viwango husika kwa lengo la kufanikisha uandishi wa makala mahsusi yanayohusika.

Pili, kwa kuwa utafiti huu umerejelea makosa yanayojitokeza katika GTL, ambalo ni gazeti la Kiswahili, uchunguzi zaidi kwa mkabala huu, unaweza kufanywa kwa mujibu wa magazeti yaandikwayo kwa lugha ya Kiingereza nchini. Utafiti huo, utasaidia kuibua vipengele ambavyo vinakumbwa na upungufu utokanao na matumizi ya lugha katika magazeti hayo. Inawezekana pia, vyombo vingine vya habari kama vile redio na runinga kufanyiwa uchunguzi kwa mkabala huo. Matokeo ya tafiti hizo huenda yakaonyesha haja ya ushirikiano wa wahusika katika kitengo cha usambazaji wa habari, katika uhimizaji wa matumizi ya lugha katika usahihi wake, hali itakayopelekea uwasilishaji kamilifu wa ujumbe.

Tatu, kwa kuwa lugha ni mhimili mmojawapo tu katika mawasiliano, uwezekano upo wa utafiti zaidi kufanywa ukilenga mihimili mingine. Muundo na yaliyomo ni baadhi ya mambo mengine ambayo yanaweza kuchunguzwa kwa mujibu wa magazeti yachapishwayo nchini. Utafiti wa aina hii utaonyesha nafasi ya vipengele husika katika kufanikisha au kukwaza mawasiliano yanayokusudiwa. Matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuziba mapengo yaliyoachwa na utafiti wetu ambao umejikita katika uchanganuzi wa matumizi ya lugha tu bila kugusia vipengele hivyo vingine

MAREJELEO

Adams, M. (1984). The Writers Mind: Making Writing Make Sense. Texas: Scott, Foresman & Company.

Agee, A. na Kline, G. (1981). The Basic Writer's Book. Englewood Cliffs, New Jersey: Prentice-Hall Inc.

Alfred, R. na Eschholz, P. (Wah. 1982). Models for Writers. New York: St. Martin's Press.

Asher, R. E (Mh. 1994). The Encyclopedia of Language and Linguistics vol. 2. Oxford: Pergamon Press.

Ashton, E. O. (1989) katika Waititu, F. (1995). Functional Writing in Kiswahili: An Investigation of Secondary School Students' Ability in Writing a Letter of Application for a Job. Chuo Kikuu cha Moi: Tasnifu ya M. Phil. (Haijachapishwa).

Aswani, F. O. B. (2001). Uswahilishaji Kifonolojia wa Maneno-mkopo yenye asili ya Kiingereza katika Kiswahili Sanifu. Chuo Kikuu cha Egerton: Tasnifu ya Ph.D (Haijachapishwa).

Baker, S. (1977). The Practical Stylist. New York: Thomas Y. Crowell Company.

Baker, S. na Stevenson, D. (1981). Practice in Exposition: Supplementary Exercises for The Practical Stylist – 5th Edition. New York: Harper & Row, Publishers.

Baran, S. J., McIntyre, J. S. na Meyer, T. P. (1984). Self, Symbols and Society: An Introduction to Mass Communication. California: Addison – Wesley Publishing Company Inc.

Barnet, S. na Stubbs, M. (1983). Practical Guide to Writing. Boston: Little, Brown and Company.

Besha, R. M. (1994). Utangulizi wa Lugha na Isimu. Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.

Brown, G. na Yule, G. (1983). Discourse Analysis. Cambridge: Cambridge University Press.

Burgen, A. D. na Burgen, J. M. (1984). Focus: Key Concepts in General Studies. Leckhampton – England: Stanley Thornes Publishers ltd.

Buyonge, E. (1995). Presuppostion and Implicature in the use of Modal constructions, Conditionals and Honorifics in Ekegusii. Chuo Kikuu cha Egerton: Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa)

Carter, R. na Nash, W. (1990). Seeing Through Language: A Guide to Styles of English Writing. Oxford: Blackwell Publishers.

Carter, R., Goddard, A., Reah, D., Sanger, K. na Bowring, M. (1997). Working with Texts: A core book for Language Analysis. London: Routledge.

Chai, J. F. (1991). Matumizi ya Lugha mjini Malindi: Jinsi Mielekeo inavyoathiri Uteuzi wa Lugha. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Chimerah, R. (1998). Kiswahili: Past, Present and Future Horizons. Nairobi: Nairobi University Press.

Chomsky, N. (1957) katika Wilkins D.A. (1972). Linguistics in Language Teaching. London: Edward Arnold (publishers) Ltd.

Cruse, D. A. (1986). Lexical Semantics. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D. na Davy, D. (1969). Investigating English Style. London: Longman Group Ltd.

Dadi, K.S. (1995). " Dhima ya Vyombo vya Habari katika Matumizi ya Msamiati," Katika Mlacha, S. K. (Mh. 1995). Kiswahili na Vyombo vya Habari. Dar es Salaam: TUKI.

Darbyshire, E. A. (1971). A Grammar of Style. London: Andre Deutsch Ltd.

Dietrich, J. na Kaiser, M. M. (1986). Writing: Self- Expression and Communication. New York: Harcourt Brace Jovanovich, Publishers.

Dominick, J. (1983). The Dynamics of Mass Communication. Massachusetts: Addison – Wesley Publishing Company.

Firbas, J. (1992). Functional Sentence Perspective in Written and Spoken Communication. Cambridge: Cambridge University Press.

Gall, M. D., Borg, W. R. na Gall, J. P. (1996). Educational Research: An Introduction – 6th Edition. New York: Longman Publishers.

Gleason, H. A. (1965). Linguistics and English Grammar. New York: Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Greene, H. A. (1965). Building Better English: Text and Grammar Handbook. New York: Harper and Row, Publishers.

Halliday, M. A. K. (1985). An Introduction to Functional Grammar. London: Edward Arnold.

Harmon, G. L. na Dickinson, R. F. (1972). Write Now! Substance, Strategy & Style. New York: Holt, Rinehart & Winston Inc.

Heine, C. na Kanyogonya, K. K. (Wah. 1979). Rural Press for Village Post-Literacy Literature. Nairobi: Afrolit Society.

Hogan, R. na Bogart, H. (1967). The Plain style: A Rhetoric and Reader. New York: America Book Company.

Idarus, A. S. (1983). "Makosa yanayofanywa mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili," katika TUKI (1983). Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1. Dar es Salaam: TUKI.

Inglis, F. (1990). Media Theory: An Introduction. Oxford: Blackwell Publishers.

Kamau, N. I. (1992). A Stylistic Analysis of Okot P'Bitek's Song of Lawino, Song of Ocol and Song of Prisoner. Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Kane, T. S. na Peters, L. J. (1986). Writing Prose: Techniques & Purposes. New York: Oxford University Press.

